

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 29 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatoo Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLAGYO - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: -**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako kabla sijaweka Hati Mezani, naomba uniruhusu nitoe pole sana kwa familia ya marehemu Mwalimu Bilango ambaye leo tutamuaga na nitoe pole pia kwa Mheshimiwa Spika pamoja na Wabunge wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha mezani:-

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba tuzingatie Kanuni ya 154 kuhusiana na salamu za pole. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):-**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Makujukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Hassan Suleiman Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini. Kwa niaba yake Mheshimiwa Mpakate.

Na. 321

**Taarifa ya Mgogoro Kati ya Kijiji cha Mkwaya na Mwekezaji**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE (K.n.y HASSAN S. KAUNJE)**  
aliuliza:-

Kuna mgogoro wa ardhi wa muda mrefu kati ya wananchi wa kijiji cha Mkwaya na mwekezaji Durbali:-

Je, ni lini mgogoro huo utapatiwa ufumbuzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu tafadhalii.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)  
alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Selemani Kaunje, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mgogoro unaowahuisha baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Lindi ambao wako kwenye Mitaa ya sokoni, Makonde na Mtere ambayo zamani ilikuwa ni sehemu ya Kijiji cha Mkwaya ambao wanensemeka kuvamia na kugawana mashamba yanayomilikuwa na Kampuni ya *Indo-African Estate Limited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu si kati ya wananchi hao na bwana Amin Durbali ambaye ni mmoja kati ya Wakurugenzi wa Kampuni ya *Indo-African Estate Limited* bali ni kati ya wananchi na Kampuni ya *Indo-Africa Estate Limited* ambayo ndiyo ina hatimiliki za mashamba hayo yenye ukubwa wa ekari 3,601.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Indo-African Estate Limited* ilifungua Kesi Na.17 ya mwaka 2015, ambayo hukumu yake imetolewa Februari, 2018 na kuipa Serikali ushindi. Kinachoendelea sasa ni taratibu za kufuta miliki za mashamba hayo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Kanuni zake za mwaka 2001. Baada ya kufutwa kwa miliki za mashamba hayo, Serikali itaweka utaratibu mzuri wa ugawanaji wa mashamba hayo kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kwa Serikali imekirii kwamba mgogoro upo katika eneo hili, je, haioni haja ya kuharakisha kufuta eneo hili ili wananchi wale wapate maeneo ya kulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wananchi wale wana mahitaji makubwa ya ardhi, Serikali haioni haja sasa kupitia mipaka ya eneo ille ili kuongeza eneo la kijiji?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi atakubaliana na mimi kwamba hukumu ndiyo imepatikana Februari, 2018 na bado kuna tetesi kwamba huyu ambaye ameshindwa ni kama vile tayari ametuma *application* kwa ajili ya kukata rufaa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wale ambao wanahitaji eneo wanapatiwa lakini kwa kufuata sheria. Naomba tuvute subira taratibu zote zifuatwe ili wananchi wapate haki lakini na yule mwingine ambaye alikuwa anamiliki asije akasema kwamba haki yake imeporwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati wananchi wa Mkwaya hawajajua mmiliki halali wa eneo hilli ni nani kwa kuwa kulikuwa na mgogoro baina ya Serikali na mwekezaji, wakati fulani Machi, 2017 wananchi waliamua...

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Ahsante. Kuna watu wameshtakiwa wakati wanaomba hilli eneo liweze kuchukuliwa na bado kesi ziko mahakamani lakini Serikali imeshinda kesi. Sasa Mheshimiwa Waziri, anasemaje kuhusu

hawa watu walioshtakiwa wakati wanalipigania eneo hili?  
Ni hatua gani Serikali itachukua ili kuwasaidia wale watu?  
(Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi tu  
Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la  
Mheshimiwa Bobali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge  
anajua historia ya mgogoro huu kwamba inaanzia miaka ya  
1995 na kwamba kuna wakati ambapo wananchi walivamia  
maeneo yale ya mwekezaji wakachukua ndizi na wengine  
wakaenda kutikisa mikorosho. Kwa hiyo, haiwezekani  
tukasema kwamba sasa hao ambao walivunja sheria Serikali  
iwatetee, ni vizuri sheria ikafuata mkondo wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea,  
swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Zainabu Nuhu  
Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa Waziri  
wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Na. 322

**Miundombinu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum –  
Shule ya Msingi Kipela**

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Shule ya Msingi Kipela, Wilayani ya Iringa, inahudumia  
wanafunzi wenye mahitaji maalum (*albinism*) lakini haina  
miundombinu rafiki, watumishi wa kutosha, huduma za afya  
stahiki na umeme:-

Je, lini Serikali itarekebisha mapungufu hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Kandege.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Nuru Mwamwindi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Kipela ina jumla ya wanafunzi 701 wakiwemo wanafunzi 93 wenye mahitaji maalum ambao wote wanakaa bweni. Shule hii ina hitaji la walimu wataalam wa elimu maalum 17 ambapo kwa sasa wapo walimu 7 na hitaji la watumishi wasio walimu 13, kwa sasa wapo 7. Vilevile shule hii ina mahitaji ya vyumba vyaya madarasa 16 kwa sasa vipo 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Kipela ipo umbali wa kilometra 8 toka Makao Makuu ya Kata ya Mziki ambapo ndiko kuliko na umeme wa gridi ya Taifa kwa sababu hiyo, kwa sasa shule hii inatumia umeme wa jua (*solar*). Aidha, shule inapata huduma za afya kwenye Zahanati ya Kanisa Katoliki iliyopo jirani na shule. Huduma hii, huchangiwa kwa malipo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na miundombinu ya shule hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepeleka jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bweni rafiki na la kisasa kwa ajili ya wanafunzi hao. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu itaendelea kuboresha miundombinu hiyo pamoja na shule zingine za aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ajira, Serikali ipo kwenye mchakato wa kuajiri walimu wa shule za msingi

4,785 wakiwemo walimu wa mahitaji maalum. Shule ya Msingi Kipela ni mionganini mwa shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum zitakazopangiwa baadhi ya walimu hao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamwindi.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa mahitaji ni walimu 17, kwa sasa wapo walimu 7, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha ikama ya walimu inakamilika katika Shule ya Msingi Kipela? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, watumishi wasio walimu wapo 7, mahitaji ya shule ile ni watumishi 13. Je, Serikali haioni wakati sasa umefika wa kuhakikisha idadi ya watumishi wasio walimu inakamilika kutokana na uhitaji wa shule? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Mwamwindi kwa jinsi ambavyo amekuwa akiwapigania wananchi wake wa Mkoa wa Iringa katika kuhakikisha kwamba wanapata huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kutaka kujua Serikali ina mkakati gani, kwanza naomba nitumie fursa hii kuagiza Wakurugenzi wote kwa sababu umeshatoka

Waraka kutoka Ofisi ya Rai, TAMISEMI ukiwataka Wakurugenzi wahakikishe kwamba wale walimu ambao wamejifunza elimu maalum wanapelekwa kufundisha katika shule maalum kwa sababu wana ujuzi nao. Kwa hiyo, ndani ya Mkoa wa Iringa na maeneo jirani ni vizuri Wakurugenzi wakahakikisha *stock* inachukuliwa ili wale walimu wote ambao wana ujuzi maalum waweze kupelekwa kabla huo mkakati wa pili wa ajira haujatekelezwa kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na upungufu wa watumishi ambao siyo wa taaluma ya elimu, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanapatikana kwa mujibu wa ikama lakini pia itategemea bajeti itakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kumekuwa na shida ya walimu wa alama kwa ajili ya wanafunzi viziwi. Je, Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha tunapata walimu zaidi kuweza kuwasaidia watu wanaotumia alama katika kujifunza? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi hawa walimu ambao wanatumia alama nayo ni elimu maalum. Kwa hiyo, sisi tunalitazama kwa mapana yake yote na ndiyo maana nimesema kwamba katika hao walimu watakaoajiriwa, naamini na hao wanaotumia alama ni mionganini mwa hao wenye uhitaji maalum na

watachukuliwa ili kuweza kuhudumia wanafunzi wanaohitaji walimu wenye kutumia alama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nitoe pole kwa walimu wote wa Tanzania, familia ya Mwalimu Bilago na Chama chake cha CHADEMA. Baada ya pole hizo, naomba swali namba 323 sasa lipate majibu ya Serikali.

Na. 323

**Kituo cha Polisi Chanika Kupatiwa Gari la Patrol**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kukipatia kKituo cha Chanika gari la *patrol*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuzingatie Kanuni ya 154.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kabla sijajibu swali hili, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kuomboleza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, haya ndiyo nasema, Mheshimiwa Spika ameshatoa pole kwa niaba yetu wote.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kipolisi ya Ukonga ipo katika Mkoa wa Kipolisi llala na Kituo Kikuu ni Kituo cha Polisi Stakishari ambacho kinasaidiwa na vituo vingine vidogo kama vile Pugu, Chanika, Msongola, Gongolamboto, Mazizini, Karakata, Kinyerezi, Tembo Mgwaza na Kitunda. Vituo hivi vyote huhudumiwa kwa magari saba toka katika Kituo cha Stakishari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika Kituo cha Polisi cha Chanika lipo gari Na. PT 1889 *Toyota Land Cruiser Pickup*, ndilo hutumika kufanya doria katika eneo hilo likisaidiwa na magari mengine toka katika Kituo cha Stakishari, kwani kituo hiki ni kikubwa ukilinganisha na vituo vingine vilivyo tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi litaangalia uwezekano wa kuongeza gari katika Kituo cha Polisi Chanika na kuzingatia vigezo kama vile hali ya uhalifu, idadi ya watu, sababu za kiutawala na kijiografia kwa kulinganisha na maeneo mengine yenye mahitaji kama haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwashukuru sana Jeshi la Polisi la Zimamoto. Juzi walipata ajali ya moto katika Kata ya Zingiziwa na ukaunguza maduka zaidi ya 15 lakini kwa mara ya kwanza Zimamoto waliwahi mapema wakasaidia kuzima moto ule pamoja na kwamba mdhara yalikuwa makubwa lakini walisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kituo kimejengwa kwa nguvu za wananchi pamoja na wadau mbalimbali na Naibu

Waziri anafahamu kwamba hii sehemu ndiyo mpakani mwa Mkuranga, unaenda Mkuranga, Kisarawe, mapori ya Dondwe na kama alivyosema vingine vyote ni *Police Post*. Kwa hiyo, naomba hii hoja ya kutafuta gari, kabla ya kuleta hili swali hapa Bungeni nimewasiliana na mapolisi, wanapata shida na eneo ni kubwa, Ukonga sasa ina watu zaidi ya 900,000. Kwa hiyo, kwa kweli tunahitaji gari kwani hilo gari lilitopo linafanya kazi ya *OCS* na ikitokea dharura wanakuwa *stranded* wanakimbiza watu na pikipiki jambo ambalo ni hatari. Eneo hili Benki ya *CRDB* imefungwa kwa sababu ya kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba hii hoja ya kutafuta gari ipewe uzito, gari liende pale liwe *stagnant* kwamba kuna gari ambalo viongozi wanalitumia na gari la doria kwa maana ya *ku-control*/Ukonga yote. Kwa hiyo, ningeomba hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza...

**MWENYEKITI:** Aah, Mheshimiwa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Haya la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata ya Kivule tunalo eneo tayari la kituo cha polisi, kama ambavyo Chanika wamejenga wananchi tumechangia, ningeomba *commitment* ya Waziri au Jeshi la Polisi, ni lini tutaenda kufanya harambee eneo lile kwa sababu tayari wananchi wameweka msingi eneo hili. Bunge lilitopita Waziri aliahidi hajaja, kwa hiyo, leo naomba kauli yake.

**MWENYEKITI:** Amekuelewa, ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Lini twende Kivule, tuchangishe fedha tujenge kituo kingine ili tupunguze uhalifu katika eneo lile? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya ya Mheshimiwa Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimepokea pongezi zake kwa niaba ya Jeshi la Zimamoto kuhusiana na kazi nzuri ambayo inaendelea kufanya. Hii inathibitisha juu ya kuimariika kwa huduma za vyombo hivi vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi ikiwemo Jeshi la Zimamoto katika kutekeleza majukumu yake na kuwapatia huduma wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, kama ambavyo nimejibu katika swali langu la msingi kwamba tutaangalia uwezekano huo. Kama unavyofahamu kwamba tuna changamoto za magari maeneo mengi nchini, kwa hiyo, tutaangalia vile vigezo na kulingana na idadi ya magari ambayo tutapokea ndipo tutaamua eneo hili linapaswa lipelekewe gari sasa hivi ama baadaye. Hata hivyo, tunatambua umuhimu wa kupeleka gari katika eneo hilo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu lini tutafanya harambee. Kwanza nimpongeze Mbunge kwa jinsi ambavyo ameweza kuhamasisha kuhusiana na hili suala la harambee, mimi nimwambie tuko tayari hata sasa hivi. Kwa hiyo, baada tu ya Bunge hili Tukufu tukae tuweze kupanga ratiba ya kuweza kufanya hiyo kazi. Tunathamini sana jitihada za Wabunge na wadau mbalimbali katika kusaidia kukabiliana na changamoto za vituo vyaya polisi nchini na hili jambo tutaliunga mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe na Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa tatizo kwenye swali la msingi la 323 la usafiri wa *patrol* kwa vituo vyta polisi lipo karibu nchi nzima. Je, Serikali sasa inajipangaje kwenda kutatua tatizo hili la usafiri wa *patrol*/katika vituo vyta polisi hasa katika Jimbo langu la Kavuu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo nimesema mwanzo kwamba tuna mpango wa kuweza kuona jinsi gani tutapunguza changamoto ya vitendea kazi ikiwemo magari katika kutoa huduma za Jeshi la Polisi. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ndiyo maana sasa hivi tupo katika jitihada za kuweza kukamilisha na kurekebisha mapungufu ambayo yalijitokeza ili tuweze kusambaza magari hayo ambayo yanategemewa kusaidia kupunguza changamoto hiyo ikiwemo katika Jimbo lake, kulingana na vigezo ambavyo nimevieleza katika swali langu la msingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkao wa Arusha jiografia yake ni pana sana na mkoa huu upo mpakani, hivyo unahitaji uangalizi mkubwa kiusalamu, lakini magari mengi ya polisi ni mabovu. Je, ni lini Serikali inafikiria kutuletea magari ya polisi mapya ndani ya Mkao wa Arusha? (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Arusha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya magari iliyopo katika Mkoa wa Arusha nayo tunaitambua. Katika mkakati wetu siyo tu kupeleka magari mapya lakini tunajitahidi kuangalia uwezekano wa kuyafanya matengenezo yale magari ambayo yanaweza yakarekebishika. Kazi hiyo imewezwa kufanywa katika baadhi ya mikoa na Arusha tutaangalia uwezekano wa kuweza kukarabati magari hayo lakini wakati huohuo magari yatakapokuwa yamepatikana tutaweza kuyasambaza katika mikoa yote nchini ikiwemo Mkoa wa Arusha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum kwa Wizara hiyo hiyo.

Na. 324

#### **Uchakavu wa Miundombinu Kituo cha Polisi – Konde**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Vituo vingi vya Polisi havina miundombinu mizuri na vingine ni vibovu na vichakavu:-

Je, ni lini Serikali itakifanya maboresho Kituo cha Polisi Konde?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu tafadhali.

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa miundombinu ya Kituo cha Polisi Konde ni mibovu na imechakaa kama ilivyo katika maeneo mengine nchini. Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kufanya ukarabati wa vituo hivyo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa Kituo cha Polisi Konde, utafanyika mara fedha zitakapopatikana ili kuboresha mazingira ya kazi kwa askari wetu na kuwawezesha kutoa huduma bora kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kadika.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza bado sijaridhika na majibu aliyotoa kwa sababu hayo ni majibu ya kila siku. Baada ya hapo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kwa kuwa miundombinu ya Kituo cha Konde ni mibaya sana hasa wakati wa mvua mpaka askari avue viatu ndiyo aweze kuingia kwenye kituo kutokana na maji yanayopita mbele ya kituo. Je, hili nalo linahitaji fedha za bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langu la pili, Kituo hicho cha Konde pamoja na nyumba za askari ni mbovu kabisa hazikaliki. Waziri amenijibu kuwa anasubiri fedha ni mwaka gani huo, mwaka huu au miaka kumi ijayo? Nataka kupata jibu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arejee swalii kwanza.

**MWENYEKITI:** Eeeh.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii kwanza halijasikika vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kadika swalii lako la kwanza uliuliza nini.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii langi la kwanza nilisema, miundombinu ya Kituo cha Konde wakati wa mvua maji yanapita mbele ya Kituo. Je, hili nalo linahitaji fedha za bajeti wakati askari hawezi kufika kituoni mpaka avue viatu? (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu kwa pamoja maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgeni Kadika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hicho cha Konde ni kweli kinahitaji marekebisho na sisi tuna mpango wa kurekebisha pale ambapo tutakapopata fedha na azma hii ipo palepale. Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge pia ana nafasi kwa yale mambo ambayo yanaonekana kwamba ni ya dharura, ni mambo madogo madogo ambayo Mbunge hayamshindi kama mabati, anaweza akachangia jitihada hizo kurekebisha mambo hayo lakini sisi kwa upande wetu kama Serikali tuna mambo mengi tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala lake la pili kuhusiana na changamoto za nyumba za askari, nadhani Mkoa wa Kaskazini Pemba ni mionganini mwa mikoa ambayo

inafaidika na ujenzi wa nyumba za askari takribani nyumba 12 na Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingine 400 vilevile Mkoa wa Kaskazini Pemba tutajenga. Kwa hiyo, hiyo ni katika jitihada ambazo Serikali tunafanya na vilevile tunapokea msaada kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge au wadau wowote katika kusaidia jitihada za Serikali kupunguza changamoto hii kubwa ya vituo vya polisi pamoja na makazi ya askari hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Itakumbukwa kwamba kuna vituo vya polisi ambavyo walijenga wakoloni, mkarithi lakini mmeshindwa kuviendeleza. Hivi karibuni kuna vifaa ambavyo mmepeleka Kisiwani Pemba viko Wilaya ya Mkoani.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Swali, je, vifaa hivyo ndio vinaenda kujenga Kituo cha Kengeja ambapo ni muda wa miaka 16 unaahidi lakini hutekelezi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa ambavyo tumepeleka si kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi cha Kengeja bali ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari Polisi katika Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunitendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba Jimbo la Konde na Mji wa Konde ndiyo uliokuwa Makao Makuu ya Wilaya kabla ya mabadiliko yaliyofanyika na kupelekwa katika Jimbo la Micheweni lakini haikuondoa uhalisia kwamba Mji wa Konde ndiyo Mji Mkuu katika Wilaya ya Micheweni hilo analielewa. Pamoja na hilo, bado Mahakama ya Wilaya ya Micheweni...

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ipo katika Jimbo la Konde na miundombinu hii miaka yote, Mheshimiwa Waziri jibu lake ni hilli kwamba Serikali mpaka ipate pesa ndiyo ifanyie marekebisho. Serikali hii hii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hebu uliza swali.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini hasa Waziri atachukua juhudhi za kufanya marekebisho katika Kituo cha Polisi cha Konde ili askari wetu wapate uhakika wa maisha yao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khatib, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu linakuwa linafanafana lakini na mabadiliko yanaonekana, maana mwaka jana tulizungumza kwamba tukipata fedha na utaona kwamba mwaka huu tumeypata fedha za kurekebisha baadhi ya changamoto hizi za Askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na eneo hilo kama ambavyo nimemjibu Mheshimiwa Kadika kwamba dhamira ya Serikali ipo palepale na hatua ambazo tunapiga za kupunguza changamoto hizi nchi nzima, hatua kwa hatua na awamu kwa awamu tunazipokea jitihada za Wabunge ikiwemo hata Mheshimiwa Mbunge kama ataamua Mfuko wake Jimbo atoe kidogo fedha kwa ajili ya kukarabati hicho kituo tutamkaribisha sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Edwin Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wananchi wa Kondoa Mjini walikusanya nguvu sana wakajenga Kituo cha Polisi kidogo pale Mjini Stand. Kituo hiki sasa kina zaidi ya mwaka kimefungwa kutokana na upungufu na ukosefu wa askari. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea askari kituo kile kifunguliwe na kifanye kazi iliyokusudiwa? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Edwin Sannda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kweli sababu hasa ni askari peke yake tunataraja kuajiri askari 1,500 hivi karibuni, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia kibali cha kuajiri askari hao, tunaamini kwamba itasaidia kupunguza changamoto ya askari. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge, mimi na yeye tupange utaratibu hata *weekend* moja twende hapo tukaangalie ili kama changamoto tu ni hiyo na kwa sababu tunahamasisha wananchi washiriki ujenzi wa vituo haikubaliki hata siku moja kuona kituo kimekamilika halafu hakitumiki. Mimi nataka nimuahidi kwamba kama itakuwa ni changamoto tu ya askari mimi na yeye tutashirikiana kulikamilisha hilo na tutakizindua kituo hicho ili kiweze kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea bado tupo katika Wizara hiyo hiyo, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 325

**Tatizo la Wahamiaji Haramu Nchini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Tatizo la wahamiaji haramu hasa kutoka Ethiopia limeshamiri sana katika nchi yetu kwa sasa:-

(a) Je, ni wahamiaji haramu wangapi wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vy'a sheria?

(b) Kama wapo ambao wanaendelea na kifungo, je, ni hatua gani za kisheria ambazo zinachukuliwa baada ya kutolewa kifungoni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji imekamata jumla ya wahamiaji haramu 13,393 katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi 2018. Miongoni mwao wahamiaji haramu 2,815 walishktiwa, 117 walitozwa faini, 429 walifungwa, 6,316 waliondoshwa nchini, 1,353 waliachiwa huru baada ya kutoa nyaraka za uthibitisho wa ukaazi wao. Aidha, zipo kesi 2,363 zinazoendelea katika mahakama mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kisheria ambazo huchukuliwa baada ya wahamiaji haramu kumaliza vifungo vyao gerezani ni kurudishwa nchini kwao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fakharia Shomar.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yametoa mwangaza kwa Watanzania, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wahamiaji haramu wanapoingia nchini bila kutambuliwa kisheria baadhi yao huzaa watoto hapa nchini. Je, hawa watoto wanakuwa raia wa nchi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa wale Watanzania ambao wanawakaribisha wahamiaji haramu hapa nchi na wanajua kisheria siyo utaratibu, je, Serikali inachukua hatua gani kwa raia hao? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hao Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Shomar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa suala la watoto wa wahamiaji haramu na wenyewe pia itakuwa ukaazi wao nchini ni kinyume na sheria za nchi yetu. Kama ambavyo tunafahamu kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji mtu anaweza kuwa raia wa nchi ikiwa angalau mmoja wa wazazi wake wakati anazaliwa alikuwa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na suala la raia ambao wamekuwa wakihifadhi wahamiaji

haramu, kwanza tunataka kutoa wito kwa wananchi wenye tabia hizo kuacha mara moja kwani kufanya hivyo ni kinyumbe na sheria za nchi lakini vilevile adhabu yake ni kali sana. Moja katika jitihada ambazo tunazifanya kukomesha au kutokomeza kabisa hii biashara ya uhamiaji haramu ni kushughulika na mitandao ya wale ambaao wanajihuisha na biashara hii ikiwemo wanaosafirisha, wanao-*organize* pamoja na wanaohifadhi. Kwa hiyo, wote hawa tukiwakamata tutawachukulia hatua za kali kabisa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la wahamiaji haramu kutoka Ethiopia linaongezeka, je, Serikali haioni imefikia wakati wa kulzungumza suala hili kidiplomasia kati ya Tanzania na Ethiopia ili kuweka utaratibu maalum kuepuka kuwaweka magerezani ambapo huligharimu Taifa? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu sahihi aliyyoyatoa tangu mwanzo na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kulileta swali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ijumaa na Jumamosi tulikuwa na vikao vyta Jumuia ya Afrika Mashariki vinavyoshughulikia masuala ya kiusalama ya kisekta na kwenye maazimio tulyoyapitisha ni pamoja jambo hili kuwa jambo la mipaka yote ya Jumuia ya Afrika Mashariki tofauti na ilivyo sasa ambako nchi zingine zote za Jumuia ya Afrika Mashariki ikiwepo Kenya wanapopitia zaidi kwao wao hili jambo halikuwa kama tatizo walikuwa wanapita tu kama mtembeaji mwengine yejote aliyeo ndani ya nchi husika.

Kwa hiyo, kwa sasa tumesema hili ni jambo ambalo tutalioanisha na mambo mengine ambayo yanazuiwa katika Jumulya ya Afrika Mashariki ili hawa watu waweze kuanza kuzuiwa kwenye mipaka ya Kenya na Sudan Kusini tofauti na ilivyo sasa ambapo huwa wanapata kipingamizi wanapofika Tanzania na nchi zingine zote wanakuwa wameshapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunalipokea na hilo jambo ambalo amelisemea la kuongea nanchi husika ambao wahamiaji hawa wanatoka ambapo ni Ethiopia, Eritrea pamoja na Somalia. Hiyo tutaifanya kwa kuanzia na Balozi zao zilizopo hapa ili jambo hilo liweze kuongewa pia katika nchi zao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Tatizo la wahamiaji haramu ni kubwa sana katika magereza nyingi za nchi hii na wengine wako *under age*. Tatizo kubwa ni pale ambapo hawa wahamiaji haramu kwa mfano Waethiopia wanakuwa wamemaliza vifungo vyao mfano mzuri ni Gereza la Lwanda, Mbeya Waethiopia 41 wamemaliza vifungo vyao zaidi ya miezi mitano, Serikali haina pesa za *ku-process* kuwarudisha nyumbani kwao wanaendelea kula chakula chetu. Ni lini Serikali itafanya mchakato wa makusudi wa kuwarudisha? Shahidi mzuri ni Mheshimiwa Sugu ambaye alikuwa katika gereza hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya jitihada nyingi sana kuhakikisha kwamba wahamiaji hawa wanarudi

majumbani kwao baada ya kukamilisha kifungo chao. Si tu kwa kutumia rasilimali zetu chache tulizokuwa nazo, lakini pia kwa kutumia ushirikiano na uhusiano tulyokwanayano na Taasisi ya Uhamiaji ya Dunia (*IOM*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mchungaji Msigwa atambue kwamba jitihada hizo tuendelee nazo kwa kasi. Hatupendelei wafungwa hawa waendelee kuishi magerezani kwani kufanya hivyo ni kuitia hasara Serikali. Sisi tutaendelea jitihada hizo kadri uwezo unavyoruhusu. Nadhani matukio kama haya ni machache sana nchini wengi tumekuwa tukiwarudisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa Mbunge wa Karagwe, kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 326

### **Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Nyakahanga – Chamchuzi**

**MHE. INNOCENT L. BUSHUNGWA** aliuliza:-

Wananchi wa Bushagaro wamekuwa wakitengwa na maeneo mengine wakati wa vipindi vyaa mvua kwa sababu ya ubovu wa barabara ya Nyakahanga-Chamchuzi, na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wakati wa kampeni za uchaguzi za mwaka 2015 aliahidi ujenzi wa barabara hiyo kwa lami na kuweka kivuko eneo la Chamchuzi:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa na kuwekwa kivuko?

(b) Je, ni lini ahadi ya kujengwa kwa lami kilomita 5 ya kianzio kwa ajili ya kutengeneza eneo korofi la Kajuna Nketo itaanza kama Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alivyoahidi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nyakahanga – Chamchazi (km 97) inahusisha barabara ya Kajura – Nkeito (km 5) na barabara ya Nyakahanga – Nyabionza – Nyakakika (km 92), ambazo ni barabara za Wilaya zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara Vijjini (*TARURA*). Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitenga shilingi milioni 150 kuititia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ili kufanya matengenezo sehemu korofu na kujenga makaravati. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga shilingi milioni 150 ili kuendelea kuifanyia ukarabati barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutekeleza ahadi zake pamoja na ahadi za Viongozi Wakuu wa Taifa zilizotolewa katika nyakati mbalimbali. Utekelezaji wa ahadi hizo unazingatia sera na vipaumbele viliviyowekwa na Serikali ambavyo ni pamoja na kukamilisha kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa, kuunganisha Tanzania na nchi jirani kwa barabara za lami na ujenzi wa barabara nyingine muhimu, ikiwemo barabara ya Nyakahanga – Chamchazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwекaji wa kivuko eneo la Chamchazi, Serikali kuititia Wizara yangu itapeleka wataalam eneo la Chamchazi ili kutafiti katika eneo hilo kuona uwezekano wa kuweka kivuko. Utafiti huo pamoja na mambo mengine, utahusisha kutambua kina cha maji ya mto iwapo kinatosha kuweka kivuko ambacho kitaelea kipindi chote cha mwaka. Mahitaji ya miundombinu yote katika eneo hilo kama vile barabara unganishi na maegesho

ya kivuko (*ramps*) katika pande zote mbili za mto. Uamuzi wa kuweka kivuko katika eneo hilo utategemea matokeo ya utafiti huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Kwandikwa, ni mchapa kazi na msikivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, barabara hii ya Nyakahanga – Nyabionza – Chamchuzi kwenda Nyakakika imekuwa korofi miaka yote na ndiyo maana wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliona ipo haja ya kuweka lami kilometra 5 kipande cha Kajura - Nkeito. Mvua iliyonyesha imefanya mawasiliano ya hii barabara yawe magumu sana na maeneo mengine ya Karagwe, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambia nini wananchi wa Karagwe kuhusu kukatika kwa mawasiliano ya barabara hii na maeneo mengine ya Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, wananchi wanaoishi katika barabara za Bugene, Kasulo na Mgakorongo Mlongo wamesubiri kwa miaka mingi sana kupata fidia ili kuweza kujengwa lami barabara hizi. Je, ni lini wananchi hawa watalipwa fidia zao? Nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bashungwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pungezi nazipokea lakini kwa ruhusa yako nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Bashungwa kwa sababu anazifuatilia sana barabara hizi za Jimbo lake. Nimwambie tu eneo lake hili ni kati ya maeneo ambayo yanaunganika na nchi za jirani, ndio maana kuna vipaumbele vingi tunavifanya kuhakikisha kwamba tunatekeleza sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuungana na wenzetu, kwa maana ya *Intergration ya East Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, ninawaambia nini wananchi, upande wa Serikali tunao mkakati ule wa kuhakikisha kwamba barabara hizi zote zinapitika wakati wote. Kwa hiyo, kama ilivyo kawaida tumetenga fedha mwaka 2017/2018, lakini mwaka 2018/2019 pia tunazo fedha za kuhakikisha kwamba tunaboresha. Kwa sababu, tumekuwa na mvua nyngi kama tulivyoshuhudia, labda niweke msisitizo tu, tumeelekeza *TANROADSMikoa* yote na *TARURAKwenye* maeneo yote kuhakikisha wanayatambua maeneo ambayo yameharibiwa na mvua na kuleta gharama zake. Upo utaratibu wa kupata gharama za pamoja ili tuweze kurejesha hiyo miundombinu iliyoharibika. Kwa hiyo, niwatoe tu hofu wananchi wa Karagwe na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaenda kurejesha maeneo haya ambayo yameharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ya muda mrefu, niseme tu kwamba kama ilivyo utaratibu suala la fidia ni la kisheria, sisi Serikali tutaendelea kulipa fidia kulingana na taratibu na sheria zilizopo, kwa hiyo, wananchi hawa wa Karagwe watalipwa fidia. Hata hivyo, Mheshimiwa Bashungwa azingitie kwamba katika bajeti tuliyopitisha, barabara alioitaja ya Bugene – Kasulo – Mlongo tunategemea kuipandisha hadhi kwenda kwenye kiwango cha lami (*double surface dressing*), kwa maana hiyo, uko

umuhimu wa kuzingatia tunalipa fidia haraka ili wakati wa kuipandisha hadhi tuweze kwenda bila mkwamo wowote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa daraja la Sanjo katika Mto Simiyu na kilometra 4 za lami Mjini Mwanhuizi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi Wakuu zipo nydingi na kuna baadhi ya maeneo ambapo ahadi zinaendelea kutekelezwa na maeneo mengine tunaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunatekeleza. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano tutahakikisha sehemu kubwa ambazo viongozi wameahidi tunaendelea kutekeleza. Kikubwa tu ni kwamba kila wakati tunaendelea kufanya uratibu ili kuhakikisha hizi ahadi zinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira. Maeneo haya nina *interest* ya kuyatembelea, nitatembea pia niweze kuona hili daraja alilolitaja pamoja na mipango mizima ya kuhakikisha kwamba ahadi zinatekelezwa, lakini kikubwa tunaboresha miundombinu ya barabara maeneo yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa hizo ahadi napenda kusikia katika barabara ya kutoka Redio Habari...

**MWENYEKITI:** Unaonaje ukiuliza swali?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Redio Habari Maalum Arusha kwenda katika Hospitali ya Wilaya ya Oltrumet katika Halmashauri ya Arusha DC. Tungependa kusikia ni lini sasa mtatimiza ujenzi wa barabara hiyo kama ilivyokuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ni ahadi za Rais hizi, tuna miaka hii iliyobaki, utekelezaji ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Molle, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivytangulia kusema tunaendelea na uratibu wa kuona kwamba ahadi hizi zote zinatekelezwa, tumejipanga vizuri. Nimpongeze sana Mheshimiwa Amina Molle kwa *concern* yake ya kuboresha barabara hii inayokwenda katika Hospitali ya Arusha DC maana tumeizungumza mara nydingi. Nami kwa uzito aliouweka Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili nilikuwa nimepanga kwamba nitatembelea Arusha, nilipotembelea safari iliyopita niliangalia barabara zingine hii sikuiona, ili tuweze kushauriana na kuweka msukumo kuhakikisha watu wanaoenda kupata huduma katika hospitali hii wanapita bila usumbufu wowote, kwa hiyo, tutaifanya namna hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ajali Akbar.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya Karagwe yanafanana sana matatizo ya Halmashauri ya Wilaya ya Newala kuhusiana na barabara kutoka Newala kuititia Kitangali hadi Mtama. Je, ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga kilometra 5 - 10, kuanzia pale Kitangali ambapo wameanza kujenga kilometra 3, kama Serikali ilivyokuwa imeahidi hasa ukizingatia ni sehemu korofii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Akbar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa ujumla kwamba tunatambua mahitaji ya uboreshaji wa barabara hasa upande wa Kusini. Hii barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge niliipita wakati nikiangalia barabara ile ya Kutoka Mtwara kwenda Mnivata tunavyoendelea kujenga kwa kiwango cha lami. Nimeona barabara hii ya Newala – Mtama lakini pia hicho kipande kingine cha kutoka Tandahimba kwenda Mtama ni muhimu sana kwa vile maeneo haya kwa kweli yanazalisha sana korosho na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Newala kwa ujumla kwamba barabara hizi tunazitazama. Nami nimeziona barabara hizi na hata ile barabara ya ulinzi ina umuhimu wake. Kwa hiyo, nimwambie tu kwamba Serikali tunalitazama kwa macho mawili eneo hili ili tuweze kuendelea kuboresha. Tumeshaanza na hizi kilometra 3 lakini tutaendelea ili kuhakikisha barabara hii inapitika wakati wote na kuboresha zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kwa Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 327

### **Mawasiliano ya Simu Katika Jimbo la Kilolo**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Katika nchi yetu kuna kampuni za simu zenye ushindani mkubwa lakini katika Jimbo la Kilolo, hasa maeneo ya Kimala, Kidabaga, hayana mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini Serikali itazishawishi kampuni za simu kusimika minara yao kwenye maeneo ambayo hayana mtandao wa mawasiliano ya simu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilainisha Kata ya Kimala na Kidabaga kwa ajili ya kupelekewa huduma za mawasiliano kupitia Kampuni ya Mawasiliano ya *Halotel*. Tayari *Halotel*/imejenga mnara eneo la Kimala na mnara huo umeanza kutoa huduma tangu tarehe 17 Septemba, 2016. *Halotel* ni kampuni pekee

inayotoa huduma za mawasiliano katika eneo hilo la Kimala. Vilevile *Halotel* imejenga mnara katika eneo la Kidabaga ambao pia, umeanza kutoa huduma tangu tarehe 9 Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana wakati swalii hili linaletwa na Mheshimiwa Mbunge, labda siku hiyo kulikuwa hakuna mawasiliano eneo hilo, lakini kuna barua ambayo nimeletemwa na Mbunge wa Jimbo la Kilolo, Mheshimiwa Venance Mwamoto, ambayo inaeleza maeneo tofauti kabisa ambayo hayana mawasiliano tofauti na aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, Wizara itawatuma wataalam wake kwenda kuangalia maeneo hayo kama kuna changamoto yoyote ili tuangalie uwezekano wa kuongeza *coverage* katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nasikitika Waziri anavyojibu, anaingiza suala la Mbunge wa Jimbo wakati mimi niliuliza swalii langu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, majibu ya Waziri hayajaniridhisha kabisa. Kuna vijiji vya Kimala, Idete, Uluti, Nyamuhanga, Ibofwee na Itimb. na vingine ambavyo sijavitaja wanajihusisha sana na kilimo kwa ajili ya biashara pamoja na kuzalisha zao la mbao, ambayo yote haya yanahitaji mawasiliano kwa ajili ya kupata soko. Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa wananchi hawa wanapata mawasiliano ili waweze kuuza mazao yao na kupata masoko wanayoyahitaji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa Waziri amesema minara hiyo imejengwa na inatoa huduma kama kawaida, yuko tayari twende akaone hiyo minara anayosema inatoa huduma ili ahakikishe mwenyewe kwamba huduma hiyo haipatikani? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuondoe masikitiko kwa sababu hizi shughuli tunazifanya kwa kuwa tunazijua na tumeshatembelea na kufanya *surveyya* kutosha nchi nzima kujua maeneo gani yana shida ya mawasiliano *critical* na eneo gani ambalo lina shida ya mawasiliano ya kawaida ambayo yanahitaji kuongezewa *coverage* na ni maeneo gani ambayo yana shida za mawasiliano kwa vipindi tu vifupi kutokana na kufungiwa *solar* badala ya umeme wa kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kujibu maswali yake kuhusu eneo la Kimala, Kidete na vijiji vinavyohusiana, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafanya ziara baada ya Bunge hili la bajeti kwenye maeneo yote pamoja na maeneo ya Kata nzima ya Kising'a najua kuna changamoto za mawasiliano, lakini nitafanya ziara kwenye Kata ya Mahenge, maeneo ya Magana na llindi ambako kuna shida kabisa ya mawasiliano, vilevile nitafanya ziara kwenye Kata ya Ibumu kwenye Kijiji cha Ilambo kuangalia kuhusu changamoto ya mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitakuwa tayari kuongozana naye pamoja na Mbunge wa Jimbo kuangalia maeneo hayo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza uniruhusu niwape pole wananchi

wa Kata ya Mahenge ambao wameingiliwa na tembo ambao wanafanya fujo kwelikweli, naomba Serikali isikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amekiri kwamba yuko tayari kuongozana kwenda kuangalia sehemu ambazo zina shida ya mitandao hasa katika Kata ya Kising'a, Kata ya Ibumu, Ilambo pamoja na Mahenge, Ilindi na Mdaila, basi na mimi niungane naye, niombe watakapokuwa wamepanga basi wasiniache. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 328

**Ahadi ya Rais Kupandisha Hadhi  
Barabara – Jimbo la Mchinga**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI** aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Urais mwaka 2015 Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alifika Kijiji Nangaru katika Jimbo la Mchinga na kuahidi kupandisha hadhi Barabara ya Mtange – Chikonji – Nangaru kutoka hadhi ya Halmashauri kuwa barabara ya Mkoa:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itapandishwa hadhi?

(b) Je, ni kwa nini Serikali huchukua muda mrefu kutekeleza ahadi mbalimbali zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Uchaguzi Mkuu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mwasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kuwa, mwezi Julai, 2017, Serikali ilianzisha rasmi Wakala wa Barabara za Vijijiini na Mijini (*TARURA*) kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza mtandao wa barabara za Wilaya. *TARURA* imeanzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali (*The Executive Agency Act*), Sura 245 kupitia Gazeti la Serikali, *GN No. 211*, la tereha 12 Mei, 2017. Lengo la uanzishwaji wa wakala huu ni kuhakikisha kuwa barabara za Wilaya zinapata msukumo wa usimamizi wa kutosha kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imesitisha zoezi la upandishaji hadhi wa barabara za Wilaya kuwa za Mkoa kwa vile kuna Wakala wa Barabara za Vijijiini na Mijini (*TARURA*) ulioanzishwa mahsusini na kupewa jukumu la kusimamia na kuendeleza barabara za Wilaya nchini. Ni matumaini yangu kuwa mtaipa ushirikiano *TARURA*, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kukidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Viongozi Wakuu, ahadi hizi zinajulikana na zitaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Meneja wa *TARURA* wa *Lindi DC*, hii barabara sasa hivi iko kwenye matengenezo, kipande cha kutoka Nangalu kwenda mpaka Moka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inahusisha Halmashauri mbili, Manispaa ya Lindi kwa eneo la Mtange, Chikonji na maeneo ya Kineng'ene pamoja na *Lindi DC*. Sasa nilitaka kujua, ili barabara hii yote ikamilike ni Meneja gani wa *TARURA* anahusika kwa sababu barabara hii ni zaidi ya kilometra 50 na inahusisha Manispaa pamoja na *Lindi DC*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kama nilivyosema kwenye swalii msingi kwamba Mheshimiwa Rais alikwenda Nangalu wakati wa kampeni, akaahidi barabara hii ataipandisha hadhi na kuna vitu aliviangalia ndyo maana akaahidi hivi. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba mtufikishie salamu hizi kwamba ile ahadi ya Mheshimiwa Rais kuna haja ikatekelezwa kwa sababu ya umuhimu na urefu wa barabara hii. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Bobali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza zile pongezi ambazo amezielekeza *TARURA* nazipokea na tutazifikisha *TARURA*. Niseme tu ni azma ya Serikali kwa kweli kuja na *TARURA* ili kuhakikisha kwamba barabara zetu sasa tunazisimamia na tunazitengeneza kwa kufuata weledi (*Professionalism*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ni mwaka tu toka waanza na wameanza kwa kupokea bajeti iliyokuwa kwenye Halmashauri na wameanza vizuri na uratibu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wameratibu barabara zote, kwa maana kwamba sasa hata *allocation* ya mafungu itakwenda kwa kulingana na kuwiana na mahitaji ya barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la barabara hii aliyoitaja kuhusisha Lindi Manispaa na Lindi *DC*, uko utaratibu wa usimamizi wa barabara. Kama hii barabara aliyoitaja imetajwa kwa maana ya kwamba ina jina moja *project* namba fulani, kama itaunganisha barabara zote utaratibu wetu kama Serikali ni kwamba mafungu yanaweza kutengwa kupitia *TARURA* upande mmoja lakini upo utaratibu wa hawa Mameneja kuwasiliana kuhakikisha kwamba barabara inakwenda kwa *standard* zilezile. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi lengo ni kuhakikisha barabara aliyoitaja itapata huduma bila kujali Meneja yupi amesimamia. Cha msingi ni kupeana mrejesho kama kuna sehemu ambayo tunatakiwa kuitazama kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais kama alivyosema, hizo salamu kwa kweli Mheshimiwa Rais amezisikia, tunakushukuru sana kwa pongezi zako. Kwa kweli ni hulka nzuri kutoa kutoa shukrani pale ambapo jambo jema limetokea. Kwa hiyo, nasi tukupongeze sana Mheshimiwa Mbunge na tutaendelea kushirikiana, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swalii linalofuta linaulizwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma kwa Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto.

Na. 329

### **Hitaji la *CT SCAN* Hospitali ya Bugando**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. MHE. KITETO Z. KOSHUMA)** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Bugando inatoa huduma kwa Mkoa wa Mwanza na Mikoa jirani ikiwemo Simiyu na Mara lakini Hospitali hiyo haina *CT Scan*:-

Je, ni lini Serikali itapeleka *CT Scan* katika Hospitali hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua umuhimu wa kuimarisha huduma za uchunguzi katika hospitali za Kibingwa ngazi ya Kanda na Taifa ikiwemo hospitali ya Bugando. Hii ni pamoja na kuhakikisha hospitali hizi zinakuwa na vifaa nya kisasa nya uchunguzi vikiwemo kuwa na *CT Scan* na *MRI*. Wizara ipo katika hatua za utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa vifaa nya uchunguzi kupitia mradi wa *ORIO* ambapo Hospitali ya Bugando ilipangiwa kupata *MRI* na *CT Scan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wakati Wizara ikiendelea ukamilishaji wa mradi huu, Hospitali ya Bugando nayo ilinunua *CT Scan* kupitia mipango yake ya hospitali na tayari ilishasimikwa, kuzinduliwa na kuanza kazi tangu tarehe 26 Januari, 2018. Wizara inaipongeza Hospitali ya Bugando kwa juhudhi hiyo. Serikali kwa sasa itaendelea na mpango wa kuitafutia Hospitali ya Bugando mashine ya *MRI*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda tu sasa kufahamu na niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa kuwa vifaa hivi nya uchunguzi ni muhimu sana kwenye Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa na Kanda, Serikali imeonekana kuwa inachukua muda mrefu sana bila kutekeleza ahadi za

kupeleka vifaa hivi kwa wakati na izingatiwa kwamba suala la afya ni muhimu sana. Mheshimiwa Waziri atuambie kwa kuwa wanategemea mradi wa *ORIO* ambaao muda siyo mrefu watapata vifaa hivyo, ni lini Hospitali ya Bugando itapata kipata kifaa cha MRI kwa sababu ya wananchi wengi wa Kanda ya Ziwa kupata huduma? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, tunayo hospitali ya Mkoa ya *Sekou Toure*, vifaa hivi kama *CT Scan* kwenye hospitali ya Mkoa ni muhimu sana. Ni lini sasa Wizara kwa mpango ule watahakikisha walau kifaa kimoja, *CT Scan* kwenye Hospitali ya Rufaa ya *Sekou Toure* kinapatikana na kusaidia wananchi wengi zaidi? Nakushukuru. (*Makoffi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa ufuatiliaji wa karibu katika masuala ya afya katika Mkoa nzima wa Mwanza vilevile katika Jimbo lake la Nyamagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabula ameuliza ni lini mashine ya *MR*/itapatikana. Kama nilivyojibu katika jibu la msingi nilisema kwamba Serikali inaendelea na maandalizi na tuko katika majadiliano na Serikali ya Netherlands kuititia mradi wa *ORIO* na awamu ya kwanza ya mashine ya kwanza ya *X-Ray*, vilevile na upatikanaji wa *CT Scan* na *MR*/kwa baadhi ya hospitali ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Bugando tunatarajia kabla ya mwisho wa mwaka huu itaweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la pili ameuliza ni lini sasa tutapeleka mashine ya *CT Scan* ama *MR* katika Hospitali ya Rufaa ya *Sekou Toure*. Kulingana na mwongozo

wetu tulio nao sasa huduma ya *CT Scan* na *MRI*/zinapatikana kuanzia ngazi ya Rufaa ya Kanda, lakini tumeona kwamba mahitaji yamezidi kuongezeka, idadi ya watu imezidi kuongezeka na mfumo wa uendeshaji hospitali za rufaa umebadilika, kwa hiyo, sasa hivi Wizara inafanya mapitio ya miongozo yake ikiwa ni pamoja na kuangalia mahitaji ya huduma kama ya *CT Scan* katika ngazi ya Rufaa za Mikoa. Tutakapokamilisha taratibu hizo basi huduma hizi *CT Scan* tutazishusha katika ngazi ya Rufaa ya Mikoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tunaendelea, swali linalofuata linauzwa na Dkt. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega linaelekezwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Na. 330

### **Migogoro kati ya Hifadhi za Taifa na Wananchi-Busega**

**MHE. DKT. RAPHAEL M.CHEGENI** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwepo na migogoro mingi kati ya Hifadhi za Taifa na wananchi ambao ni wakulima na wafugaji hali inayosababisha uvunjifu wa amani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa tatizo hili linapata ufumbuzi endelevu hasa maeneo ya Lamadi, Makiloba, Kijereshi na Nyamikoma katika Wilaya ya Busega?

(b) Baadhi ya wanyama kama tembo wamekuwa wakifanya uharibifu wa mali na mazao ya wananchi wanaoishi maeneo hayo. Je, Serikali inatoa tamko gani la kuzuia tatizo hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hasunga.

## **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Lamadi, Mwakiloba, Nyamikoma na Kigereshi yanapakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori la Akiba la Kijereshi, hivyo kuna muingiliano kati ya wanyama pori na binadamu jambo linalosababisha migogoro. Aidha, maeneo yaliyohifadhiwa yanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uvamizi unaotokana na shughuli za kibinadamu kama kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, illi kumaliza tatizo la migogoro ya mipaka, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wananchi na wadau wengine, inayo nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba migogoro kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi inatatuliwa. Kazi hii inahusisha kuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi katika viji vyote vinavyozunguka hifadhi, kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi, kuimarisha miradi ya ujirani mwema na kupitia upya mipaka iliyopo katika maeneo yenye migogoro. Kazi ya kupitia mipaka na kuweka vizingi kwa sasa itaendelea kwa ushirikishwaji wa wadau wote muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyamapori hususan tembo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kunusuru maisha na mali za wananchi waishio kando ya Hifadhi ya Serengeti na Pori la Akiba la Kijereshi kama vile kuimarisha Timu ya Udhibiti wa Wanyamapor Hatari na Waharibifu ambaoinajumuisha watumishi kutoka Kikosi dhidi ya Ujangili Bunda, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Pori la Akiba Kigereshi na Halmashauri ya Wilaya, pia kwa kutumia ndege zisizo kuwa na rubani kwa ajili ya kufukuza tembo. Lengo ni kuhakikisha kwamba tukio

lolote la uvamizi wa tembo linashughulikiwa kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kusizitiza kuhusu umuhimu wa kuepuka kufanya shughuli za kibinadamu kwenye shoroba za wanyamapori na maeneo ya mipaka ya hifadhi ya vijiji. Aidha, Wizara imeandaa kanuni za kutenga na kuhifadhi shoroba na maeneo ya mtawanyiko ili kuruhusu mwingiliano wa kiikolojia kati ya wanyamapori utakaoimarisha utofauti wa vinasaba pamoja na kuboresha ustawi endelevu wa bioanuai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika majibu yake amekiri tatizo la tembo linazidi kuongezeka na wananchi wengi sana wanapata madhara makubwa na wanaathirika sana na tatizo hili. Wananchi wa vijiji husika wakiwemo vya Matongo, Mwauchumu, Longalombogo na maeneo mbalimbali hapa nchini wameathirika sana. Nataka tu kujua Serikali sasa inachukua hatua gani za kimkakati, tuache hizi hadithi za kwamba tutafanya, tuko mbioni, ni lini tatizo hizi sasa tutalipatia ufumbuzi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Kikosi dhidi ya Ujangili kimeshajenga kituo pale Lukungu na kituo hiki maana yake ni kusaidia kufukuza wanyama waharibifu wakiwemo viboko. Je, ni lini kituo hiki cha Lukungu kitaanza kufanya kazi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Chegeni, naona umenitajia na maeneo ambayo kwenye Jimbo langu yameathirika sana na hawa wanyama pamoja na Itilima. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mazuri na ya uhakika kwa maswali haya. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya

Mheshimiwa Dkt. Chegeni. Kwanza kabla sijajibu, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia na hii ni mara ya tatu kuliuliza hili swali, hii inaonesha kwamba hili swali ni muhimu sana katika eneo la Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye jibu la msingi kwamba katika maeneo yote haya ambayo kuna matatizo sasa hivi tutachukua hatua za dhati kuanzia tarehe 1 Julai, 2018 wakati bajeti mpya itakapoanza kutekelezwa. Tumejipanga sawasawa kuhakikisha kwamba haya yote tutayatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu hiki Kituo cha Kupambana na Ujangili (*KDU*) kwanza kama alivyosema mwenyewe tayari majengo yameshakamilika, tunachosubiri hivi sasa ni kuhakikisha kwamba rasilmali watu pamoja na vifaa vyta kutendeakazi vinakamilika ili kusudi kile kituo kianze kufanya kazi katika mwaka wa fedha unaokuja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu siyo rafiki. Maswali kwa siku ya leo ndiyo hayo yameisha lakini tumekula kidogo muda wetu. Naomba utulivu kidogo Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo ya wageni, ninaanza na waliokaa katika Jukwaa la Spika, tunao wageni wa Mheshimiwa William Lukvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Ndugu Doroth Mwanyika - Katibu Mkuu; Dkt. Moses M. Kusiluka - Naibu katibu Mkuu; Ndugu Alex Mangowi - Mshauri kutoka Shirika la Maendeleo la Uingereza (*USAID/DFID*); Ndugu Felix Maagi - Kaimu Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba (NHC); Ndugu Stephen Nindi - Mkurugenzi Mkuu *NLUPC*; Ndugu Suleiman Dabbas - Mtaalamu Mshauri *LTSP*; Ndugu Biseko Musiba - Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora; Dkt. Adam Nyaruhuma- Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro; Ndugu Dismas W. Minja - Mkurugenzi Mkuu *NHBRA* na Ndugu Mary G. Makondo - Kamishna wa Ardhi. (*Makofii*)

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wadau 13 wa maendeleo, Watendaji Wakuu kutoka sekta na makampuni binafsi wakiongozwa na Mwakilishi wa *Care International* Ndugu Mary Ndaro. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa William Lukuvi, ni kutoka mradi wa *Land Tenure Assistance* chini ya *USAID*, Ndugu Malaki Msingwa na Ndugu Tressan Sullivan. Pia wapo wadau wa sekta ya nyumba wanaoshiriki katika maonesho ya Nyumba Bora. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, ambaao ni wataalam wa sekta ya ardhi kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Illemela na Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kutoka Wilayani Pangani Mkoani Tanga, Ndugu Mohamed Rished Abdallah ambaye ni Mbunge Mstaifu wa Jimbo la Pangani. Karibu sana Mheshimiwa Mohamed. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ambaao ni viongozi wa CCM kutoka Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi wakiongozwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Amani, Ndugu Abbdullah Mwinyi Hassan. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Ridhard Mbogo ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Nsimbo Mkoani Mpanda. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni shemeji yake Ndugu Boniphace Ndengo kutoka Mkoani Mara. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni watano wa Mheshimiwa Martin Msuha ambaao ni viongozi wa Kampuni ya Mipango Miji ya

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

HUSEA kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Renny Chiwa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe ambao ni Makatibu wake wa Kavuu kutoka Mkoani Katavi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 60 wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambao ni *Muungano Jogging and Dodoma Fitness Club* wa Jijini Dodoma. Karibuni sana, naona mpo *fit* kweli kweli. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis ambao ni viongozi wa CCM, Wilaya ya Kinondoni kutoka Jijini Dar es Salaam. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Walimu Sita kutoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Dodoma Mwalimu Augustine Njamasi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyonayo kwa leo. Waheshimiwa Wabunge kwa ratiba yetu ya leo leo sitachukua mwongozo wowote. Katibu.

**NDG. PAMELA PALANGYO- KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**MWENYEKITI:** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi wasilisha hoja yako. (*Makofi*)

## **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA**

**MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Fungu Namba 03 kwa mwaka 2018/2019. Vilevile, pamoja na hotuba hii nimewasilisha taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi ikijumuisha miradi inayosimamiwa na Wizara pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa hii yapo maonesho machache nyuma ya Jengo la Utawala ambapo ningeomba Waheshimiwa Wabunge wote mpitie kuna nyaraka nyingi zaidi ambazo tumeshindwa kuzifikisha ziko ndani ya makabrasha. Wale wote ambaao walikuwa wanataka kununua viwanja katika maeneo mbalimbali ya Mijini wapite kule pamoja na Dodoma, Mwanza, Tanga na Dar es Salaam, lakini na wale ambaao wanataka kushiriki katika kupima maeneo yao ya mijini, yako makampuni binafsi ambapo mnaweza mkapatana nao wakawafanya hizo kazi kwenye Majimbo yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Aidha, kufuatia kifo cha Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama kilichotokea mwezi Novemba, 2017, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, wananchi wa Jimbo la Songea Mjini pamoja na wote walioguswa na msiba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majonzi na masikitiko makubwa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, wananchi wa Jimbo la Buyungu, pamoja wote walioguswa kufuatia kifo cha Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago kilichotokea tarehe 26 Mei 2018 katika Hospitali ya Muhimbili Jijini Dar es Salaam. Vilevile natoa pole kwa wananchi wote waliofiwa na walioathirika kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika maeneo mbalimbali. Nawatachia kila la kheri wenzetu wote watakaotuwakilisha kwenye msiba wa Mheshimiwa Bilago, safari njema na Mungu awatangulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia rasilimali za Taifa ikiwemo ardhi; kupambana na rushwa; kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Katika uongozi wake amezidi kuijengea heshima kubwa nchi yetu. Namshukuru kwa maelekezo na ushirikiano anaonipa, ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu aliyonikabidhi ya kusimamia sekta hii ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Kassim, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na viongozi wote wa Serikali kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Balozi Seif Ally Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wao huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza kwa kuongoza shughuli za Bunge lako Tukufu kwa ufanisi. Pia

nawapongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansansu, kwa utendaji mzuri katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti wote wa Bunge hili ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima muendelee kutimiza jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri aliyoafanya mwezi Oktoba, 2017. Vile vile nampongeza Dkt. Kilangi kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawatachia wote kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Janeth Masaburi, aliyyeteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa Mamasita, Mbunge wa Longido na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha kwa kuchaguliwa na wananchi wao kuwakilisha. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini na Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini nao kwa kuchaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni. Nawatachia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya utangulizi ya jumla ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa kazi za Serikali zitakazotekelwa katika mwaka wa fedha ujao. Wizara yangu imeanza kuyafanyia kazi yale yote yanayohusu sekta ya ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake jasiri Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kemirembe Lwota kwa ushauri wao ambao umewezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawashukuru sana, Waheshimiwa Wabunge hawa ni waungwana mno, kwa uchambuzi na ushauri wao makini wa ukweli walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Namba 48, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Namba 3 ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka 2018/2019. Pia nawashukuru kwa maoni na ushauri walioutoa kwa Wizara wakati Kamati ilipotembelea miradi ya taasisi zinazosimamiwa na Wizara na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuhakikishia kuwa ushauri wao utazingatiwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Narudia kuwashukuru sana wajumbe hawa wa Kamati, hii ni Kamati nzuri sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuunda Kamati hii ambayo imekuwa kwa mara ya kwanza imeanza kutushauri kwa upendo na ushauri wao tutauzingatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wangu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, kwa ushirikiano na ushauri anaonipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu. Pia nawashukuru Katibu Mkuu Bi. Dorothy Mwanyika, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Moses Kusiluka, Wakuu wa Idara, vitengo, taasisi, wakala zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi na wadau wote wengine wamekuja leo, wameshatoka ambao tunashirikiana kwenye sekta ya ardhi, wapima binafsi,

wapangaji binafsi, mabenki, taasisi mbalimbali, idara mbalimbali zinazojitegemea na walipa kodi wote wa sekta ya ardhi kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa namna ya kipekee, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Dkt. Yamungu Kayandabila, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa mchango wake mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nampongeza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania na kumtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ismani kwa kunivumilia. Kwa namna ya pekee, niwashukuru Wabunge wote wa Bunge hili kwa ushirikiano wanaonipa katika kazi hizi. Nawaahidi nitakuwa nanyi hadi kero za wananchi wenu kuhusu ardhi zitakavyomalizika. Aidha, napenda kumshukuru sana mke wangu Germina Lukuvi na watoto wangu wote kwa kunivumilia kwa muda mwingi huku Dodoma na kufanya kazi nyingi Mikano na Waheshimiwa Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa muhtasari wa utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara pamoja na Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2018/2019. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa miradi ambayo ni sehemu ya hotuba imeambatishwa na nyingine, kama nilivyosema mtazikuta kwenye mabegi kule nje. Pia majedwali mbalimbali yaliyomo katika hotuba yanafafanua kwa kina mafanikio katika utekelezaji wa bajeti. Takwimu za utekelezaji wa bajeti zilizopo katika hotuba hii zinaishia 15 Mei. Aidha, naomba hotuba yangu yote kama ilivyo kwenye kitabu inukuliwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya 2017/2018. Katika kutekeleza majukumu

ya Wizara yangu, tumeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya mwaka 2020/2025. Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano yaani 2016/2017 - 2020/2021, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, pamoja na sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya Fungu Na. 48, ambalo ni la Wizara, ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka huu wa fedha unaoishia Juni, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 112.5 kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, Wizara imekusanya shilingi bilioni 78.9 sawa na asilimia 70 ya lengo Ni matarajio yangu kwamba hadi Juni 2018 lengo la kukusanya shilingi bilioni 112.5 litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waloliipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati, lakini natoa onyo kwa wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi, Serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani na kutaifisha mali zao ili kufidia kiwango cha kodi wanazodaiwa au kuwafutia miliki. Kwa hiyo, natoa wito kwa wote ambao wanamiliki ardhi kisheria wakumbuke kulipa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha huu, Serikali illahidi kupunguza tozo ya mbele (*premium*) ambayo hutozwa mara moja tu wakati wa umilikishaji ardhi, kutoka asilimia 7.5 hadi asilimia 2.5 ya thamani ya ardhi. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ahadi hiyo imetekelezwa. Hata hivyo, pamoja na punguzo hilo, tathmini iliyofanywa na Wizara yangu imebaini kwamba bado kuna mwitikio mdogo wa wananchi kukubali kumilikishwa ardhi, hususan katika maeneo ya urasimishaji wa makazi mijini, yale yaliyokuwa *squatter*. Imebainika kwamba changamoto hii kwa kiwango kikubwa inachangiwa na gharama kubwa za

umilikishaji zinazochangiwa na tozo ya mbele. Hivyo, Serikali inaangalia uwezekano katika mwaka ujao wa fedha kushusha tena kiwango cha tozo ya mbele ili kuwavutia wananchi wengi wenyewe maeneo ya ardhi, wakiwemo wananchi wanyonge kujitokeza kwa wingi zaidi kupimiwa na kumilikishwa ardhi yao. Mkakati huu unalenga kuwamilikisha wananchi ardhi waliyo nayo ili wawewe kuitumia kikamilifu kwa shughuli za maendeleo ikiwemo kuondoa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi na pia ardhi kutumika kama dhamana ya kupata mikopo katika taasisi za fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu inatarajia kukusanya shilingi bilioni 120 kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- (i) Kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi ya pango la ardhi kwa kurasimisha makazi mijini.
- (ii) Kutoza kodi la pango ya ardhi katika maeneo yote ya mijini ambayo hayajapimwa na kumilikishwa lakini yanamilikiwa na watu.
- (iii) Kuhuishwa miundo ya kiutumishi ya wataalamu wa sekta ya ardhi katika halmashauri ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali ardhi, ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.
- (iv) Kupunguza tozo ya mbele yaani *premium* kwa wananchi wote waliojenga nyumba katika maeneo ambayo hayajapangwa ili kuwawezesha kulipa kodi ya pango la ardhi.
- (v) Kuimarisha mifumo iliyopo ya utunzaji wa kumbukumbu na kuhuishwa taarifa za ardhi.

(vi) Kuhimiza wamiliki wote wa ardhi nchini kulipa kodi ya ardhi, kwa mujibu wa sheria na kuwachukulia hatua wadaiwa sugu ikiwemo kuwafikisha Mahakamani.

(vii) Kuendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji pamoja na sekta binafsi katika upangaji na upimaji wa ardhi ili kuongeza idadi ya viwanja na hivyo kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

(viii) Kuendelea kuboresha mifumo ya kumbukumbu za ardhi ili kurahisha ulipaji wa kodi ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imefanya tathmini kuhusu mwenendo wa ulipaji wa kodi ya pango la ardhi unaofanywa na taasisi za umma ikiwemo shule, vyuo, wakala, ofisi za Serikali na kubaini baadhihaziendeze ardhi kibashara lakini zinadaiwa malimbikizo mengi ya kodi ya pango la ardhi. Ili kuondoa kero na gharama za kufuatilia ulipaji wa madeni hayo, Serikali inakusudia kutoa msamaha wa kodi ya pango la ardhi kwa taasisi na mashirika ya umma ambayo yamejikita kutoa huduma na si kutumia ardhi kibashara. Hili litaambatana na upimaji wa lazima wa maeneo yote ili yasivamiwe. Maeneo kama ya shule na hospitali za Serikali yatapimwa na kupewa hati ili wasilipe kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 68.65 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 43.26 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 25.4 ni bajeti ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 38.34 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 55.8 ya bajeti. Mchanganuo wa matumizi umeonyeshwa katika jedwali namba 2, ukurasa wa 75 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na.3, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Tume ilipokea shilingi bilioni 1.41 sawa na asilimia 67 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara ili kuwezesha kutekeleza shughuli za Tume katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ardhi na miliki. Wizara yangu ina jukumu la kutoa huduma mbalimbali za ardhi kwa wananchi zinazolenga kuimarisha usalama wa miliki na kuifanya ardhi kuwa moja ya nguzo kuu za uchumi katika uzalishaji mali. Kwa kuzingatia uamuzi wa Serikali wa kuhuisha muundo wa utumishi wa wataalamu wa sekta ya ardhi, waliopo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wataalam hawa watasi mamiwa moja kwa moja na Wizara yangu. Lengo la uamuzi huu ni kuimarisha utoaji huduma wa sekta za ardhi, kudhibiti zaidi migogoro baina ya watumiaji wa ardhi na pia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kwa jamii hususani kwa wananchi wanyonge, ili wasije kudhulumiwa au kuingizwa katika migogoro kuhusu ardhi wanayoimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Wizara yangu inatambua umuhimu wa sekta ya ardhi katika kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kufikia uchumi wa kat iifikapo 2025 kwa kuongeza uwekezaji katika viwanda. Ili kuendana na azma hii, Wizara yangu imehakikisha kuwa katika uandaaji wa mipango kabambe, maeneo ya kutosha yanatengwa kwa ajili ya wawekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, mipango kabambe ya miji 18 ilioandaliwa imetenga jumla ya ekari 127,942.96 katika maeneo na Wilaya mbalimbali 18 za nchi hii kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Mchanganuo wa maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya viwanda yanapatikana katika jedwali Na. 3 ukurasa wa 76. Aidha, Wizara yangu

imetoa mwongozo kwa mamlaka zote za upangaji kuhakikisha zinatenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda wakati wa uundaji wa mipango kabambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imebatilisha miliki za mashamba yenye ukubwa wa ekari 9,639.19 katika Wilaya za Lushoto, Busega, Bukoba, Arumeru, Kilosa na maeneo mengine nchini. Nimetoa maelekezo kwa mamlaka za upangaji, yaani Wilaya na Mikoa inayohusika kuzingatia utengaji wa maeneo kwa ajili ya viwanda, kilimo na ardhi ya akiba bila kusahau ardhi kwa ajili ya mahitaji ya wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mikubwa ya Kitaifa. Wizara yangu imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mikubwa ua ujenzi wa mlundombinu ya kitaifa hususan bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Mkoani Tanga; reli ya kisasa (*Standard Gauge Railway*) na ufuaji wa umeme katika Mto Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*). Katika mradi wa bomba la mafuta, Wizara imeshiriki katika uandaaji mikataba ya uendeshaji wa miradi, uandaaji wa ramani za msingi katika njia ya bomba la mafuta, utaratibu wa utoaji wa ardhi na uthamini wa ardhi na mali kwa ajili ya fidia na upimaji wa njia ya bomba la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya ufuaji wa umeme, Wizara inashiriki katika upimaji wa eneo la mradi na kuandaa ramani za msingi kwa ajili ya kuandaa michoro ya kihandisi. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na mamlaka husika katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara itaanza kuandaa kwa awamu mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya zote 24 na vijiji 134 ambavyo bomba la mafuta linapita, na katika maeneo ambayo reli ya kisasa inajengwa, ili maeneo hayo yapangwe vizuri kwa maendeleo ya viwanda na biashara kwa lengo la kuongeza tija za miradi hiyo

mikubwa hasa katika maeneo yote ambayo reli na bomba la mafuta litapita. Miji yote kandokando itapangwa na maeneo ya viwanda na biashara yatapangwa kandokando ya maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi. Azma ya Wizara ni kuhanikiha kwamba kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa. Lengo la kufanya hivyo ni kuwa na miliki salama na hivyo kuondoa na kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi, kutumia ardhi kama mtaji hai, kuchochea uwekezaji, kupanua wigo wa mapato ya Serikali, kuongeza mchango wa sekta ya ardhi katika uchumi, kuhanikiha kuwa ardhi inatumika kwa tija na kuwa na makazi bora na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo ni takribani asilimia 15 tu ya ardhi ya jumla ndiyo iliyopangwa na kupimwa. Hali hii inafanya ardhi isiwe na mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa na kuikosesa Serikali mapato. Katika kukabiliana na hali hii, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini. Ni matumaini yangu kwamba programu hii ikitekelezwa ardhi itatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Ardhi za Kanda. Wizara imeimarisha kanda zote kwa kipeleka vitendea kazi vya kisasa na wataalam. Dhamira ya Wizara ni kuendelea kuimarisha huduma zake, katika ngazi za mikoa na halmashauri zote nchini. Natoa rai kwa wananchi wote kutumia Ofisi za Ardhi za Kanda kupata huduma za ardhi badala ya kufuata huduma hizo Makao Makuu ya Wizara kama ilivyokuwa hapo awali, kwa sababu ndani ya kanda sasa kuna wataalamu wote wenye maamuzi ya mwisho yanayohusiana na masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki wa mashamba na viwanja. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu iliendelea kuhakiki mashamba na viwanja nchini ili kubaini uzingatiaji wa masharti ya umiliki. Kati ya mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018 jumla ya mashamba 32 yalibatilishwa. Katika mwaka wa fedha huu tunaoenda nao, mashamba manne (4) yaliyopo katika Wilaya ya Lushoto, Busega, Bukoba na Arumeru ambayo wamiliki wake wamekiuka masharti yalibatishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha kamili ya mashamba yote yaliyobatilishwa mpaka sasa iko katika Jedwali Na.7, ukurasa wa 110. Mashamba haya yamerudishwa Mikoa ili Wakuu wa Mikoa kwa kushirikiana na halmashauri zinazohusika waainishe mahitaji ya wananchi wa maeneo hayo ili wapimiwe wapewe lakini na pia kuzingatia mahitaji viwanda na maeneo mengine ya uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi na udhibiti wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Kamati ya Kisikta iliyoundwa kubaini aina, vyanzo na kupendekeza namna bora ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ilikamilisha kazi yake. Kamati hii kama mnavyojua iliundwa na Wizara tano. Kamati ilichambua migogoro 1,392 iliyowasilishwa hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge waliandika kila mtu katika maeneo yake na migogoro yake mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya tathimini ya hali halisi Kamati ilibaini kuwepo jumla ya migogoro 1,750 ambapo migogoro 564 ilihusu uvamizi wa maeneo ya hifadhi, 218 mwingiliano ya mipaka ya kiutawala, 369 uanzishwaji wa vijiji ndani ya maeneo ya hifadhi, migogoro 204 ni ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, migogoro 206 wananchi na wawekezaji kwenye maeneo ya ranchi, mashamba na migodi na migogoro 115 ilitokana na madai ya fidia. Vilevile kulikuwa na migogoro 77 ambayo ilikuwa na vyanzo vingine vidogo ambavyo utatuzi wake hauhitaji taasisi zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Wizara inayohusika imeandaa mkakati wa kutekeleza mapendekezo ya Kamati. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI zimeanza kupitia na kujiridhisha na kuchukua hatua juu ya migogoro mbalimbali inayohusu mipaka ya vijiji kwa vijiji, wilaya kwa wilaya, mipaka ya hifadhi za misitu na vijiji, mipaka ya hifadhi ya wanyama na wananchi, ranchi mbalimbali za mifugo na mashamba makubwa yanayomilikiwa na Serikali. Kila Wizara itachukua hatua kutatua migogoro inayohusu sekta zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ujumla imeshaelekeza Wakuu wa Mikoa kutatua migogoro yote inayohusu mipaka ya vijiji katika mikoa yao. Naamini kazi hii inaendelea, kila mkoa utasimamia kuhakikisha kwamba migogoro ya mwingilliano kati ya vijiji na vijiji inakamilika kwa mujibu ya *GN* zilizotangaza vijiji husika. Maliasili wameshaanza kuchukua hatua ya kumaliza kabisa migogoro inayohusu hifadhi na vijiji, hifadhi mbalimbali za wanyama, misitu na nyingine. Wizara ya Mifugo na Kilimo nao wameanza uhakiki wa maeneo yao na kutoa *notice* kwa watu ambao hawaendelezi mashamba yao ya mifugo na kilimo ili waweze kupewa wananchi wengine. Wizara yangu itaendelea kutoa utaalami ili kufanikisha utatuzi huu wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchambuzi uliofanywa na Kamati ya Kisekta, Wizara yangu kupitia kauli mbiu ya 'Funguka kwa Waziri wa Ardhi' nilifanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini ili kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi. Aidha, kupitia kauli mbiu hiyo, Wizara yangu ilisambaza dodoso katika Halmashauri zote nchini ambapo wananchi walibainisha kero zao na changamoto zinazowakabili kuhusiana na sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kauli mbiu hiyo hadi tarehe 15 Mei, jumla ya malalamiko 3,599 yalipokelewa. Wizara yangu kwa kushirkiana na halmashauri na mamlaka nyingine ya Serikali inaendelea kuyachambua na kuyapatia

ufumbuzi malalamiko hayo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu itaendelea kwa kasi kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu na kuendelea kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia majibu kadiri zinavyopolewa. Aidha, tutaongeza kasi ya kuja mikoani na kwenye majimbo ili kutatua kero kwa haraka. Ni ushahidi na dhahiri kwamba kero zimepungua sana sasa na kero tunazoshughulika na kuzisikia ni za siku nydingi sana. Wote ni mashahidi kwamba sasa hivi kumekuwa na uadilifu kutoka na nidhamu ya utendaji mikoani na hivyo kero zinazotengenezwa sasa zimekuwa chache kidogo kulinganisha na zile za zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuwezesha Umilikaji wa Ardhi. Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Umilikaji wa Ardhi (*Land Tenure Support Programme*) inayotekelizwa katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi Mkoani Morogoro. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara ilipanga kuhakiki vipande vya ardhi 80,000; kujenga ofisi za ardhi mbili katika Wilaya ya Malinyi na Ulanga; ukarabati wa ofisi katika Wilaya Kilombero na kuandaa vyeti vya ardhi katika vijiji 15. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi tarehe 15 Mei, jumla ya vipande vya ardhi 96,257 vilipimwa, kati ya vijiji 41 ambapo jumla ya hati miliki za kimila zilizotolewa ni 20,583; mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 36 imeandaliwa, wakandarasi wa ujenzi wa ofisi za ardhi za wilaya wamepatikana na taratibu za kuandaa vyeti vya ardhi 75 zilivyopimwa zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jumla ya vijiji 20 vimeandaliwa mipango kina ya makazi ambapo jumla ya viwanja 18,224 vimepimwa kwa ajili ya kuandaliwa hati ya hati miliki za kimila. Vilevile Benki za NMB na CRDB zimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.4 kwa wananchi ambao tayari wameshapata hati miliki za kimila katika maeneo hayo yaliyotekeliza programu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itapima vipande vya ardhi kwa ajili ya kuandaa

hati miliki za kimila 120,000; kuandaa mipango kina ya vijiji; kupima viwanja 20,000; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi vijiji 30 na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kisera, kisheria na kitaasisi juu matumizi ya ardhi. Kazi nyingine ni kuzijengea uwezo taasisi zinazohusika na utatuvi wa migogoro ya ardhi katika ngazi ya vijiji, kata na wilaya; kufanya tafiti tatu za masuala ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuboresha utawala wa ardhi na kukamilisha ujenzi wa ofisi za ardhi katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi. Maelezo ya kina yanapatikana katika taarifa na vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuvunjwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu. Baada ya kuvunjwa kwa iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*), Wizara yangu ilipewa jukumu la kumilikisha upya ardhi kwa kutoa hati miliki kwa miaka 99 badala ya ile 33 iliyokuwepo zamani kwa wamiliki wote waliokuwa na hati za pango la ardhi yaani *ground lease*. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi tarehe 15 Mei, 2018, wananchi wote 21,124 waliokuwa wanamiliki hati za pango la ardhi zilizopo katika masjala ya Wizara zimebadilishiwa kutoka *ground lease* ya miaka 33 na kuwa hati miliki ya miaka 99. Wananchi wote wamebadilishiwa hati zao zote bila malipo na gharama yoyote wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge waliokuwa na *ground lease* sasa wamepewa *title dead* bila malipo yoyote. Aidha, wananchi wote walionunua viwanja viliyopimwa na Manispaa yaani Jiji sasa watapewa hati za miaka 99. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Dodoma kwa kasi ya upimaji wa viwanja. Kama mlivyoomba Waheshimiwa Wabunge humu ndani Serikali inasikia maneno yenu. Tumeongeza muda wa ulipaji kutoka mwezi mmoja mpaka miezi 3 kwa wananchi wote ambao wanununua viwanja hapa Dodoma. Kwa hiyo, wale wote ambao walifikiri wanatakiwa kulipa viwanja hivi vinavyonunuliwa kwa mwezi mmoja, hapana, sasa mmepeewa hadi miezi 3 ili wananchi mjikusanye taratibu. Vilevile viko viwanja vingine vinaunauzwa katika mikoa mbalimbali lakini wao kule

wanatoa miezi 6, hata hivyo sisi tuliopo hapa Dodoma tutaendelea kuangalia *trend* inavyokwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo ya kielektroniki na huduma za ardhi. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali iliahidi kuanza kutoa Hati za Kielektroniki katika Manispaa za Kinondoni na Ubungo kwa kutumia Mfumo Uganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Intergrated Land Management Information System*). Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia Julai, 2018 hati za kielektroniki zitaanza kutolewa kwa wamiliki wa ardhi katika Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni na Ubungo. Nimewaambiwa waoneshe picha ya hati moja ambayo itakuwa inatolewa sasa ambayo ni ya karatasi moja ile pale badala ya faili lenye kurasa 10. Kwa wale wananchi wa Wilaya ya Kinondoni na Ubungo tumeshaanza ku-scan hati zao zote za zamani zitabdalishwa watapewa zile zinazoonekana hapo kwenye screen na kuanzia mwezi wa saba hati mpya zitakuwa za karatasi moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliahidi kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Kodi ya Pango la Ardhi (*Land Rent Management System*) katika halmashauri mbalimbali nchini. Ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi, umilikaji wa ardhi na usajili wa hati, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imeboresha mfumo huo ambao wananchi wanaweza kupata taarifa za hatua za umilikishaji na usajili wa hati zao kwa njia ya elektroniki katika ofisi za halmashauri. Maboresho haya yatawapunguzia wananchi usumbufu, muda na gharama katika kufuatilia huduma hizo Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mfumo huo umeunganishwa na mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Mafunzo ya kutumia mfumo huo yanetolewa kwa kanda zote nane za ardhi, halmashauri 185 na Mabaraza ya Ardhi yote 53. Vilevile kwa sasa wamiliki wa ardhi wanaweza kutumia mfumo huo kulipia kodi ya pango

la ardhi kwa kutumia simu za mikononi kwa kufuata maelekezo kama yalivoonekana katika kiambatanisho Na.4 ukurasa wa 72. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mifumo ya kielektroniki niliyoelezea hapa juu, Wizara yangu kupitia wataalam wake wa ndani imetengeneza mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa udhibiti wa taarifa za mashamba yote nchini. Mfumo huu utaainisha ukubwa, umiliki, matumizi na hali ya maendelezo kupitia picha za *satellite* na taarifa zake zitapatikana kwa kutumia kompyuta au simu za kiganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo utaraphisisha utambuzi wa mashamba yasiyoendelezwa kwa ajili ya miliki zake kubatilishwa au kupangiwa matumizi mengine. Hadi mwezi Mei, taarifa za mashamba yaliyopo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Lindi, Iringa, Manyara, Arusha zitakuwa zimeingizwa kwenye mfumo huu. Mfumo huu ukikamilika Waheshimiwa Wabunge haitatulazimu sisi kufika mikoani kukagua mashamba yenu. Pale pale ofisini tutakuwa tunajua watu ambao hawajaendeleza mashamba na kuchukua hatua ya kuyafuta na kuwapa wananchi wengine wayaendeleze kutoptana na mfumo huu. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itaendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki ili utoaji wa huduma za ardhi uwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa mali na fidia. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara iliahidi kuandaa na kuidhinisha taarifa 35,000 za uthamini kwa ajili ya fidia na uthamini wa kawaida kwa matumizi mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini 23,831 ambapo taarifa 13,316 ni uthamini wa fidia na 10,515 ni uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, Wizara ilikamilisha uundaji wa Bodii ya Usajili wa Wathamini ambayo imeanzhishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na.7 ya mwaka 2016. Bodii

hii pamoja na mambo mengine inasimamia usajili wa taaluma na maadili katika utendaji kazi wa wathamini. Bodi imepewa mamlaka ya kuwachukulia hatua za kinidhamu ikiwemo kuwafutia usajili wathamini wote waliokiuka maadili ya taaluma zao. Natoa rai kwa wananchi na wadau wote wa tasnia wa uthamini kutoa taarifa kwa bodi juu ya wathamini wote wanaokiuka maadili ya taaluma zao au watu wanaofanya kazi za uthamini kinyume cha sheria ili waweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya ardhi hubadilika kutokana na mabadiliko ya hali ya soko. Kutokana na hali hiyo, Wizara hahuisha viwango vya thamani ya ardhi mara kwa mara. Uhuishaji huu huwezesha kuwa na viwango sahihi vya ulipaji fidia, utozaji wa kodi na ada mbalimbali zitokanazo na miamala ya ardhi. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itahuisha viwango vya bei ya soko la ardhi kwa nchi nzima. Pia wizara inakusudia kuandaa na kuidhinisha taarifa za uthamini 35,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mfuko wa Fidia imezinduliwa na tayari imeanza kazi. Kwa kuwa sasa kuna Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016, Bodi inafanya mapitio ya Kanuni za Ardhi za Usimamizi wa Mfuko wa Fidia za mwaka 2001 ili ziweze kukidhi mazingira ya sasa ya ulipaji wa fidia na kuondoa mgongano wa kisheria wa sheria hiyo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Mfuko wa Fidia itakamilisha utungaji wa kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa ramani. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu iliahidi kuhuisha ramani za msingi za uwiano wa 1:50,000 katika miji 50. Ramani hizi ni muhimu katika uandaaji wa ramani za matumizi mbalimbali ya ardhi na ramani zinazoonesha mipaka ya viwanja na mashamba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ramani za misingi 20 za uwiano wa 1:50,000 za miji midogo 68 katika Wilaya za Geita, Mbogwe, Nyangw'ale na Chato zimehuishwa kwa kutumia picha za *satellite*. Katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu

itaendelea kuhuisha ramani za msingi katika miji 100 katika wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya ndani ya nchi. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu iliahidi kuendelea kuainisha mipaka ya ushoroba wenyewe ukubwa wa kilomita 2,500 katika Pori Tengefu la Loliondo, Wilayani Ngorongoro. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ushoroba wa Pori Tengefu wa Loliondo wenyewe ukubwa wa kilomita 1,500 umeainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi na uhakiki wa mpaka kati ya Wilaya ya Kilindi na Kiteto umefanyika. Vile vile uhakiki wa mikapa ya vijiji sita vinavyopakana na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro umefanyika kwa lengo la kuondoa mgongano. Katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu itahakiki mipaka sita ya Wilaya ya Babati na Monduli, Manyoni na Sikonge, Gairo na Kilosa, Kisarawe na Kibaha, Njombe na Mufindi na Mbarali na Mufindi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya kimataifa. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa ramani za msingi pamoja na kupima kipande cha kuanzia Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron chenye urefu wa kilomita 240. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hii inaendelea na imeshaanza ambapo hadi tarehe 15 Mei, kipande cha mpaka cha kilomita 50 kutoka Ziwa Victoria hadi Sirari kimekamailika. Katika kipande hicho jumla ya alama 480 za kati ya mpaka zimesimikwa, alama kuu saba zimebomolewa zimejengwa upya na alama 18 zimekarabatiwa. Aidha, uchukuaaji wa taarifa za kijiografia katika vijiji 32 vilivyo katiaka eneo la mpaka huo zimekamilika kwa ajili ya kuandaan ramani za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara yangu iliahidi kuimarisha mpaka baina ya Tanzania na Uganda katika eneo

la nchi kavu. Kazi hii inaendelea kwa uwekaji wa alama za mpaka, uandaaji wa ramani za msingi pamoja na uandishi wa andiko la mkataba wa mpaka. Katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu itakamilisha uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Uganda, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi pamoja na kuendelea na uimarishaji wa mpaka baina ya Tanzania na Kenya. Vilevile Wizara itaimarisha mipaka yetu ndani ya Ziwa Tanganyika na nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Burundi na Zambia. Uimarishaji wa mipaka yetu na nchi jirani ni kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi pamoja na utekelezaji wa Azimio la Umoja wa Afrika linalozitaka nchi wanachama kuimarisha mipaka yao ifikapo mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa viwanja na mashamba. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja 200,000 na mashamba 400. Hadi tarehe 15 Mei, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja 144,780 na mashamba 257 zimeidhinishwa nchini kote. Katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu imepanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja 200,000, mashamba 400 pamoja na kufufua mipaka ya viwanja vya mashamba 500 yenye migogoro ya matumizi ya ardhi katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara yangu iliahidi kusimika na kupima alama za msingi yaani kuweka *control points* 200 katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi tarehe 15 Mei, Wizara yangu imesimika na kupima alama za msingi 250 katika Wilaya za Rufiji, Kilombero, Malinyi na Tarime. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu itasimika na kupima alama nyingine 500 za msingi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga uwezo wa kupima ardhi nchini. Ili kuongeza kasi na kupunguza gharama za upimaji wa ardhi nchini ni muhimu kuwa na vifaa vya kisasa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu iliahidi kununua vifaa vya kisasa vyenye ufanisi mkubwa katika upimaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taratibu za ununuzi wa

vifaa hivyo zimekamilika na mzabuni ataviwasilisha vifaa hivyo vyote nchini kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Vifaa hivyo vitasambazwa katika kanda zote nane na vitatumiwa na halmashauri zote nchini bila gharama yoyote. Vilevile Wizara yangu itaandaa mafunzo yatakayofanyika mwezi Juni kwa ajili ya kuwapa elimu wapima wote waliopo kwenye halmashauri, Kanda na Wizara ili waweze kuvitumia vizuri vifaa hivyo. Lengo ni kwamba halmashauri ziweze kupima maeneo yote katika wilaya zao na kupunguza gharama za wananchi wanaotaka kupimiwa viwanja na mashamba kwa sababu vifaa hivi sasa vitakuwa ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji miji na vijiji. Upangaji wa miji na vijiji unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira, kuzuia matumizi kinzani na kuwa na uhakika wa uwekezaji katika ardhi. Majukumu haya yanatekelezwa kuititia mipango kabambe, mipango kina mijini na vijini, uramishaji, makazi yanayoendelezwa kiholela na udhibiti wa usimamizi wa uendelezaji miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango kabambe ya uendelezaji miji. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, huu tunaoenda nao, Wizara iliahidi kushirikiana na halmashauri husika kukamilisha mipango kabambe ya majiji ya Dar es Salaam na Tanga, Manispaa za Iringa, Singida pamoja na Miji ya Ifakara, Mahenge, Malinyi, Bariadi, Kibaha na Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, jumla ya mipango kabambe ya miji 8 imekamilika. Mipango ya miji (*master plan*) zillizokamilika ni ya Miji ya Musoma, Mtwara, Iringa, Kibaha, Singida, Korogwe, Arusha na Mwanza. Mipango mingine ya miji 20 iko katika hatua mbalimbali za uandaaji nayo ni mipango ya Miji ya Bariadi, Babati, Geita, Njombe, Ifakara, Ulanga, Malinyi na Tunduma. Manispaa za Moshi, Bukoba, Lindi, Sumbawanga, Morogoro, Shinyanga, Kigoma Ujiji, Tabora, Mpanda na Songea, Jiji la Tanga na Dar es Salaam nayo iko katika orodha ya kukamilisha mipango yao. Orodha ya mipango hiyo inapatikana katika Jedwali Na.10 ukurasa 121.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara yangu itashirikiana na Mamlaka za Upangaji za Kigoma Ujiji, Songea, Morogoro, Tabora, Lindi, Tunduma, Babati, Geita na Njombe kukamilisha mipango kabambe ya miji hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu na uendelezaji wa miji. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro 2,000 kutoka Mamlaka za Upangaji yaani Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 jumla ya michoro ya mipango miji 1,947 ilipokelewa na 1,870 iliidhinishwa. Michoro hii iliyoidhinishwa ina jumla ya viwanja 418,607. Kati ya hivyo, viwanja 5,932 ni kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara inatarajia kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro ya mipango miji 2,500 kutoka Mamlaka za Upangaji nchini yaani Halmashauri za Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urasimishaji wa makazi holela mijini. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Upangaji, Halmashauri zote nchini, pamoja na wadau mbalimbali kama MKURABITA na sekta binafsi iliendelea kurasimisha makazi katika Halmashauri 27 nchini. Hadi Mei, 2018 jumla ya viwanja 142,992 vilipimwa katika Halmashauri mbalimbali. Orodha ya maeneo yaliyofanyiwa urasimishaji yanapatikana katika Jedwali Na. 11 ukurasa wa 126.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kurasimisha makazi katika Halmashauri za Songea, Njombe, Dodoma, Lindi, Mtwara Mikindani, Musoma, Mwanza, Illemela, Kigoma Ujiji, Tabora, Nzega, Singida, Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga, Mbogwe, Busega, Kibaha, Ubungo na Kinondoni. Aidha, Wizara yangu itaendelea kujenga uwezo wa watumishi wa Mamlaka ya Upangaji katika kutekeleza miradi ya urasimishaji makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara yangu itaendelea kutekeleza Programu ya Kurasimisha na Kuzuia Ujenzi wa

Makazi Holela ya mwaka 2013 - 2023. Zoezi hili la urasimishaji halina mipaka. Wilaya yoyote nchini ambayo iko tayari na ina maeneo haya inaweza kuendelea bila kujali hii orodha ya Wilaya ambazo nimezitaja. Wilaya yoyote nchini ambayo ina makazi holela inaweza kupanga mikakati ya kuanza urasimishaji mahali popote pale wanapoamua kufanya katika Wilaya zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya matumizi ya ardhi. Uhuishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi mwaka 2013-2023. Katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu kwa kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliahidi kufanya mapitio ya programu za mpango huo ili kuhuisha na kujumuisha masuala ya maendeleo ya viwanda nchini. Wizara yangu imeupitia mpango na kuainisha maeneo ambayo yatahuishwa kwa kuzingatia mahitaji ya viwanda na mabadiliko ya tabianchi. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara yangu itakamilisha uhuishaji wa mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (*TANAPA*)itawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya vijiji 392 vinavyopakana na hifadhi za Taifa kote nchini katika Wilaya za Babati, Kondo, Simanjiro, Monduli, Kigoma, Muleba, Chato, Geita, Kilombero, Kilosa, Mpanda, Arusha na Arumeru. Wilaya nyingine ni Busega, Itilima, Meatu, Iringa, Mbarali, Chunya na Chamwino. Aildha, Wilaya za Bagamoyo, Rungwe, Makete, Wanging'ombe, Mikumi, Hai, Rombo, Moshi, Karatu na Ngorongoro nazo zitanufaika na mpango huu wa uwekaji wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji 392 vinavyopakana na mbuga na hifadhi mbalimbali chini ya *TANAPA* kwa gharama za *TANAPA* lakini kwa utendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya sekta ya nyumba. Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uendelezaji sekta ya nyumba nchini. Sekta hii huchangia kukuza uchumi, kuongeza ufanisi, fursa za ajira na kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia hayo, Serikali imeendelea kuweka mazingira

wezeshi ili kuwavutia uwekezaji katika sekta hii na kuwawezesha wananchi kumudu gharama za nyumba zilizo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu iliahidi kuendelea kukusanya taarifa za waendelezaji miliki na kuziingiza katika kanzidata. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taarifa mbalimbali za nyumba zimeendelea kuingizwa na nyingine kuboreshwa ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu bei za nyumba katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, taarifa ya Vyama vya Ushirika na nyumba 34 zimeingizwa kwenye kanzidata hiyo. Kati yake vyama 16 vimejenga jumla ya nyumba 1,000. Aidha, taarifa za waendelezaji miliki 130 ambazo wamejenga nyumba 24,870 zimeingizwa katika kanzidata (*database*). Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara yangu itaendelea kukusanya na kuboresha taarifa za nyumba katika kanzidata ya nyumba nchini na kuanzisha Kituo cha Taarifa ya Kumbukumbu ya Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa. Wizara yangu inasimamia Shirika la Nyumba la Taifa kwa ajili ya kujenga nyumba, kuuza na kupangisha, ikijumuisha nyumba za gharama nafuu. Kwa kuzingatia majukumu ya shirika na malengo yaliyojipangia, hadi Mei 15, Shirika limekamilisha ujenzi wa nyumba 151 katika eneo la Iyumbu, kati ya nyumba 300 ambazo shirika litajenga katika mradhi huo. Vilevile Shirika limekamilisha miradi 39 yenye jumla ya nyumba 2,280 maeneo mbalimbali nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi unapatikana katika aya za 94 – 97 ya kitabu cha hotuba. Aidha, kwenye kitabu kingine cha majedwali kuna taarifa mbalimbali nyingine za maendeleo ya nyumba. Aidha, katika mwaka wa fedha ujao, Shirika litaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 149 zilizobaki katika eneo la Iyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kisheria na sera. Katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu iliahidi kukamilisha rasimu ya Miswada ya Sheria ukiwemo ule wa

kutunga Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Sekta ya Miliki. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba rasimu ya Muswada wa Sheria hizo umeandaliwa. Hatua za kukamilisha Miswada hii zinaendelea kwa kuchambua maoni ya wadau ili yaweze kuzingatiwa katika rasimu ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yangu itaendelea na taratibu za kukamilisha Rasimu za Miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Miliki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidia na Sheria ya Mawakala wa Ardhi. Tunatunga Sheria ya Mawakala wa Ardhi ili kuondoa makanjanja sokoni, kuwafanya walipe kodi na waache kudhulamu wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya sera. Wizara inaendelea na taratibu za kukamilisha marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha usalama wa miliki, kuboresha mazingira ya uwekezaji, kudhibiti migogoro baina ya watumiaji wa ardhi, kuimarisha haki na usawa katika upatikanaji na utumiaji wa ardhi kwa makundi mbalimbali ya watumiaji pamoja na kuhakikisha ardhi kama moja ya nguzo kuu ya uchumi inatumika ipasavyo katika kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, Wizara iliahidi kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na kuandaa Sera ya Taifa ya Nyumba. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mtaalamu Mwelekezi amekamilisha kuandaa rasimu ya sera hizo na hivi sasa wadau ikijumuishwa Wizara na Taasisi za Serikali na wadau wengine wanaendelea kuchambua na kutoa maoni kwa ajili ya kuziboresha zaidi rasimu hizo. Sera zote zitakamilishwa katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala na rasilimali watu. Mwaka huu wa fedha, Wizara yangu iliahidi kuwapatia mafunzo watumishi 70 na kuajiri watumishi 291. Pia Wizara iliahidi kuendeleza na kupanua na kuboresha ofisi zake ili kuwezesha watumishi wote kuhamia Dodoma. Napenda

kuliarifu Bunge lako Tukufu, hadi tarehe 15 Mei, Wizara imeajiri watumishi 61 na kuwapangia mafunzo. Aidha, Wizara imeimarisha ofisi zake na kuwezesha watumishi kuhamia Jijini Dodoma. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itawapatia mafunzo watumishi wengine 70 na kuajiri watumishi wengine kadri vibali vitakavyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri. Kwa kuzingatia uamuvi wa Serikali wa kuwataka wataalamu wote wa Sekta ya Ardhi walipo katika Halmashauri kuwajibika katika Wizara moja, yaani Wizara ya Ardhi, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inaandaa utaratibu bora wa utekelezaji wa maamuzi hayo ili kuwezesha kusimamia kwa ufanisi rasilimali ardhi. Wizara itahakikisha inawapanga upya watumishi ili kuwa na uwiano mzuri ukillinganisha na ilivyo sasa. Wilaya nyingine hazina watumishi lakini nyingine ina watumishi waliopindukia. Kwa hiyo, watumishi wa sekta hii watapangwa upya katika kila Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kukabiliana na changamoto. Katika hotuba yangu nimeainisha mikakati mbalimbali inayotekelwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 na hivyo kukabiliana na changamoto mbalimbali. Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali ya uhaba wa wataalamu na vitendea kazi katika ngazi za Halmashauri, Wizara yangu inaendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi za Kanda kwa kupeleka wataalamu wote na wengi zaidi ili kuwezesha kutoa usimamizi wa karibu na ushauri wa kitaalamu katika Halmashauri. Aidha, itaendelea kupeleka vifaa vya upimaji katika Ofisi zote za Kanda na Wilaya za Halmashauri ili kuwezesha kazi za upangaji na upimaji ardhi katika Halmashauri kufanyika kwa kasi. Pia itaendelea kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watu na mifugo, ikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa ni mojawapo ya chanzo cha migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Katika kukabiliana na changamoto

hii, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri inatekeleza programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi. Programu hii inatekelezwa katika Halmashauri za majaribio za Malinyi, Kilombero na Ulanga Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji inayozingatia mahitaji ya makundi mbalimbali ya watumiaji. Pia kwa kutumia uzoefu huo wa Wilaya tatu unaopatikana kutoka kwenye miradi ya majaribio ya Wilaya ya Kilombero na Malinyi, Wizara itatumia uzoefu huo kwa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo mengine nchini. Kadhalika Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa uendelezaji wa sekta ya miliki nchini kumesababisha Sekta hii ya Miliki (*Real Estate*) kukosa usimamizi madhubuti na kuifanya kushindwa kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa. Wizara yangu imeandaa rasimu ya mapendekezo ya Muswada ambao utakuja Bungeni mwaka ujao wa fedha (*The Real Estate Bill*) ambao unakusudia kuunda chombo cha kusimamia uendelezaji wa Sekta Miliki ambao utaambatana na Miswada midogo mingine ya kudhibiti hawa madalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na kero ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia unaofanywa na taasisi na wadau wanaotwaa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, Wizara yangu imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa ajili ya kuratibu shughuli za ulipaji wa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Kwa niaba ya Wizara yangu, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji. Vilevile napenda kuishukuru Benki ya Dunia na nchi wahisani zikiwemo Uingereza, Denmark,

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Sweden, Japan, China, India, Korea ya Kusini na Marekani.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawashukuru wadau wengine walioshiriki katika utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila ambao ni pamoja na MKURABITA, *Care International*, *Ujamaa Community Resource Team*, *OXFAM International*, *African Widelife Foundation*, *Tanzania Natural Resources Forum*, *SNV*, *Haki Ardhi*, *PELUM*, *Eco Village Adaptation*, *Climate Change in Central Tanganyika* na *Belgium Technical Cooperation* na wadau wote ambao wanashiriki katika kuondoa kero na kufanikisha shughuli za ardhi katika maeneo mbalimbali nchini kote. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau wote wa sekta za ardhi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Bila kusahau mabenki yote yanayotoa mikopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi maskini kukopa nyumba kwa bei nafuu pamoja na Benki Kuu ya Tanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula kwa kunisiaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda tena kumshukuru sana Katibu Mkuu Bi. Dorothy Mwanyika na Naibu wake Dkt. Moses Kusiluka kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi katika ngazi zote za Halmashauri ya Wilaya, Mikoa mpaka kwenye Kanda. Nawashukuru sana kwa utumishi wao uliobadilika. Hivi sasa wanafanya kazi angalau kwa maadili mazuri na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, siyo kama ilivyokuwa zamani. Naomba waendelee hivyo ili angalau kupunguza au kuondoa kero kabisa kwa wananchi wa Tanzania kuhusu masuala ya ardhi. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Katika mwaka wa fedha ujao, Wizara itaendelea kushirkiana na Halmashauri,

wadau, washirika wa maendeleo ya wananchi kwa ujumla, kutayarisha na kutekeleza mipango ya kuendeleza miji na vijiji, kusimamia upangaji, upimaji, urasimishaji, umilikishaji na usajili wa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa wa miliki. Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali pamoja na wadau wote wa sekta ya ardhi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kama nguzo kuu ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari, naomba nisisitize yafuatayo:-

(i) Kwa kuangalia uwezo wa wananchi waliopo katika maeneo yasiyo rasmi kwenye *squatter* ili kufanikisha zoezi la urasimishaji, katika mwaka wa fedha ujao Serikali itapunguza tena tozo ya mbele (*premium*) kwa wananchi wanaorasimisha makazi yao hasa maskini waliojenga mijini illi nao waweze kurasisimisha makazi yao na kupewa hatimiliki. Kwa hiyo, wale wote ambao wanaendelea na zoezi hili waendelee kwa kasi kwa sababu zoezi hili lina muda wake. Tutatoa fursa ya mwisho, tutapunguza kodi ile ambayo ni kikwazo kikubwa cha urasimishaji ili ipungue zaidi. Tunapenda wananchi wote wanaomiliki maeneo yasiyo rasmi mijini wapate hati ili ziweze kuwasaidia kiuchumi, waweze kufika kwenye mabenki na kukopa kulingana na rasilimali walizoziedeleza. Kwa hiyo, jambo hili tatalifanya katika mwaka ujao wa fedha. (*Makofii*)

(ii) Vifaa vipyta vyta kisasa ambavyo ndiyo imekuwa kikwazo cha upangaji na upimaji na kasi yake katika Wilaya vitaanza kutumika nchini kote kuanzia Julai ili kuongeza ufanisi, kuondoa kero ya upimaji na kupunguza gharama za upimaji ardhi nchini. Sambamba na hili, tutayachukulia hatua kali makampuni binafsi ikiwemo kuyafutia usajili makampuni ambayo yanachelewesha kazi za wananchi, kutoza fedha nyingi sana katika upimaji na upangaji bila utaratibu, kufanya utapeli, kuchukua fedha za wananchi bila kufanya kazi na kuvunja sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamejitokeza baadhi ya makampuni ambayo tumeyapa fursa ya kupanga na kupima,

sasa wanadanganya wananchi hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Wao wanachukua fedha wakati fedha zinatakiwa zisimamiwe na vikundi vyta wananchi warasimishaji katika mtaa. Wao wataendelea kulipwa kulingana na kazi waliyoifanya katika mtaa lakini wasipewe fedha. Fedha zisimamiwe na Kamati ya Wananchi katika mitaa ambayo inarasimishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naagiza kabisa, asitokee mtu mwenye kampuni akasema kila mwananchi amlipe Sh.300,000 ni marufuku. Fedha hizo zichangishwe na Wanakamati, ziwekwe kwenye akaunti ya Wanakamati, watunze wao, wamlipe *contractor* kwa kazi alizofanya. Iwe ni marufuku kwa wakandarasi kwenda kwenye mitaa bila Wilaya kujua. Kuna watu wanatisha kwamba tusiporasimisha sasa, Mheshimiwa Waziri atavunja nyumba zenu. Hakuna Waziri wa Ardhi wa nchi hili anayekuja kuvunja nyumba zenu, hatuvunji makazi rasmi. Nataka ma-*contractor* binafsi wasitumie mwanya huu vibaya, wafanye kazi kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

(iii) Kufuatia watu wengi kuhamia Dodoma, Manispaa imepima viwanja 10,000. Nawapongeza sana Watendaji wa Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi, Bwana Kunambi kwa kufanya kwa kasi kazi ya upimaji wa viwanja. Wale wote watakaomilikishwa viwanja hivi tutawapa hati ya miaka 99 na ninyi mmeputa uzoefu sasa, tunatoa hati hapa siyo zaidi ya mwezi mmoja tangu umewasilisha hati yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote ambao walikuwa wameshaanza kulipia mwezi mmoja kama nilivyosema, Serikali yenu ina masikio, imesikia kilio cha Wabunge. Najua mlikuwa hamjisemei ninyi Wabunge mlikuwa mnasemea na wananchi wengine. Kwa hiyo, ninyi Waheshimiwa Wabunge ambao mnanunua viwanja na tunawashawishi mnunue viwanja na wananchi wote ambao wanataka kununua viwanja Dodoma vile vilivyopimwa na Manispaa, sasa watatakiwa kulipa kidogo kidogo angalau kwa miezi mitatu, siyo kwa mwezi mmoja. Tunajua wananchi

wa kawaida hawana uwezo wa kulipa hizi milioni kwa mwezi mmoja. Kwa hiyo, kilio chenu wananchi kimefikishwa na Waheshimiwa Wabunge humu ndani. Kwa hiyo, wote kwa pamoja mmenufaika na ongezeko hili. (*Makofii*)

(iv) Wizara ya Maliasili, TAMISEMI, Mifugo na Kilimo zimeanza kutekeleza mikakati ya kuondoa kero na migogoro iliyopo ndani ya Wizara zao kufuatia kukamilika kwa taarifa ya timu za wataalamu wa Wizara tano za kisekta. Naamini Waheshimiwa Wabunge sasa maswali yenu ya mgogoro kati ya mpaka na hifadhi mtayaelekeza Maliasili zaidi kwa sababu najua yeye ndiyo mwenye *instrumentya* kutatua huu mgogoro na taarifa hizi ziko mezani kwake. Mgogoro kati ya Jeshi na vijiji mtayaelekeza kwa Waziri wa Ulinzi, mimi ni msimamizi wa jumla, nitawasaidia katika kufuatilia.

(v) Hati mpya za kielecktroniki ambazo tuliahidi tutaanza kuzitoa mwezi Julai, katika Wilaya za Ubungo na Kinondoni. Baada ya hapo tunatengeneza mradi ambao *uta-roll-over* Wilaya zote. Siyo nia ya Serikali kutekeleza mradi huu katika wilaya mbili, hizi ni za mfano, lakini baada ya hapa sasa tutaunganisha Wilaya zote Tanzania. Huu ndiyo mradi utakaofanywa kuanzia mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, zoezi hili tumelianza na tutawaalika Wawakilishi wa Waheshimiwa Wabunge katika uzinduzi wa mradi huu mwishoni mwa mwezi Julai.

(vi) Viongozi wa Wizara, mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri tutaendelea kutembelea Wilaya zenu, kukusanya maoni, kutatua migogoro na kero mbalimbali moja kwa moja huko huko. Nawashukuru viongozi wa Mikoa na Wilaya pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mnaotupa. Kero nyingi zilizobaki ni za siku nyingi sana, kwa kweli mpya wote tunakiri kwamba sasa hazizalishwi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema wale wataalam wangu zamani walikuwa wanakula bila kunawa, siku hizi wananaawa mara tatu. Kama wanakula, wanakula kiustaaraku, ndiyo maana kero hazizalishwi sana. Pia

kutokana na nidhamu ya utendaji iliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Tano, Watendaji wangu kidogo wamebadilika, yale wallyokuwa wanafanya zamani sasa hawawezi kufanya hata mkiwapa pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa onyo kwa Watendaji wote wa Sekta ya Ardhi ambao bado wanaendekeza utendaji unaochochaea kero, migogoro na rushwa, sasa dawa yao imepatikana kwa sababu wote watakuwa chini ya usimamizi wa Wizara moja, hawatakuwa na kichaka cha kujificha. Wanaharibu Sheria za Ardhi halafu wanajificha kule TAMISEMI kwa sababu kule walikuwa na uwezo, wakiwa-settle wale Madiwani kidogo, basi wanawakingia kifua, sasa sisi Wizarani hatuna Madiwani, sauti ni moja. (*Makofi*)

(vii) Nawaomba wananchi wote tujenge tabia ya kulipa kodi ya ardhi kwa wakati kila mwaka bila kusubiri kusukumwa.

(viii) Nawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote kwenye maonesho kama nilivyo sema ili muweze kujifunza mambo mbalimbali machache ambayo tumewaletea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2018/2019. Mapato. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 120 kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Na.3 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

- (i) Mapato ya Serikali Sh.120,000,000,000.
- (ii) Matumizi ya mishahara Sh.17,689,383,000  
Matumizi mengineyo Sh.17,762,362,638  
Jumla ndogo ni Sh.35,451,745,638.
- (iii) Fedha ya maendeleo.  
Fedha ya ndani Sh.20,000,000,000  
Fedha ya nje Sh.10,537,602,000.  
Jumla ndogo Sh.30,537,602,000  
Jumla kubwa Matumizi ya Kawaida na  
Maendeleo ni Sh.65,989,347,638/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na.3 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora.

- (i) Matumizi ya mishahara Sh.1,102,104,000
- (ii) Matumizi mengineyo Sh.979,822,000
- (iii) Matumizi ya maendeleo Sh.5,000,000,000  
Jumla Sh.7,081,926,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa kwa Wizara Fungu 48 na Fungu Na. 3 ni Sh.73,071,273,638.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tena, narudia kutoa shukrani za dhati kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote na Kamati yangu ya Ardhi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa namna moja au nyingine mmeendelea kutupa ushirikiano mkubwa katika sekta ya ardhi. Naomba mwendelee kutupa ushirikiano kipindi hiki cha Bunge. Leteni wageni mbalimbali wenyе migogoro mikubwa iliyokubuhu ili wakutane na sisi hapa Wizarani. Tupo tayari kuwasikiliza na kuwasaidia. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kutoa hoja. (*Makofij*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NAMAENDELEO  
YA MAKAZI, MHESHIMIWAWILLIAM V. LUKUVI (MB.),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA  
2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana nataarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasalikubali kupokea na kujadili taarifa yautekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhikwa mwaka wa fedha 2017/18.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili nakupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu **48** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu **03** kwa mwakawa fedha 2018/19. Vilevile, pamoja na hotubahii nimewasilisha taarifa ya utekelezaji waprogramu na miradi ikijumuisha miradiinayosimamiwa na Wizara pamoja na taasisi zake.

2. **Mheshimiwa Spika**, namshukuruMwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa 11wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha,kufuatia kifo chaMhe. Leonidas Tutubert Gama kilichotokea mwezi Novembra, 2017, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangukutoa pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu,familia ya marehemu, ndugu, wananchi wa Jimbo la Songea Mjini pamoja na wote walioguswa na msiba huo. Vilevile, natoa polekwa wananchi wote waliofiwa na walioathirika kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokeakatika maeneo mbalimbali nchini.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna yakipekee, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wakemahiri katika kusimamia rasilimali za Taifa, kupambana na rushwa, kuimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Zaidi ya hayo, ameendelea kuzipatia majibu kero za wananchi pamoja na kusimamia azma ya Serikali ya awamu ya Tano ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hakika uongozi wake umezidi kuijengea heshima kubwa nchi yetu.

Namshukuru kwa maelekezo na ushirikiano anaonipa ambaao unaniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta ya ardhi. Vilevile, nawapongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja naviongozi wote wa Serikali kwa mafanikiomakubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, nawapongeza Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyezekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Balozi Seif Ali Idd (Mb.), Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana chiniya uongozi wao. Vilevile, nawapongeza Wabunge naviongozi wote wa Chama cha Mapinduzi kwa usimamizi mzuri na utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama chetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuongoza shughuli za Bunge lako Tukufu kwa ufanisi. Pia, nampongeza Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika wa Bungeletu Tukufu kwa utendaji mzuri katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Vilevile, niwapongeze Wenyevitit wote wa Bunge ambaao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongozashughuli za Bunge kwa ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima ili muendelee kutimiza jukumu hili.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda piakutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri naNaibu Mawaziri walioteuliwa na MheshimiwaRais katika mabadiliko ya Baraza la Mawazirialiyofanya mwezi Oktoba, 2017. Vilevile, nampongeza Mhe. Dkt. Adelardus Kilangi kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nawatachia wote kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda nitumiefursa hii kumpongeza Mhe. Janeth MauriceMasaburi aliyeteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu. Aidha, nawapongeza Mhe. Maulid Said Abdallah Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa Mamasita, Mbunge wa Longido Mhe. Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha, Mhe. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini na Mhe. Justine Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini kwa kuchaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika hivi karibuni. Ninawatachia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao.

7. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumiafursa hii kumpongeza Mhe. Kassim MajaliwaMajaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri yaMuungano wa Tanzania kwa hotuba yakeambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/18 namwelekeo wa kazi za Serikali zitakazotekelawa katika mwaka wa fedha 2018/19. Wizara yanguimeanza kuyafanya kazi yale yote yanayoihususekta ya ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanafikiwa.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna yakipekee natoa shukrani zangu za dhati kwawajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge yaArdhi, Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota (Mb.), kwa ushauri wao ambao unaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa uchambuzi na ushauri makini walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango nabajeti ya mwaka

wa fedha 2017/18 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu **48**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2018/19. Pia, ninawashukuru kwa maoni naushauri waliotoa kwa Wizara wakati Kamatiilipotembelea miradi na taasisi zinazosimamiwa na Wizara na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Napenda kukuhakikishia kuwa, ushauri wao utazingatiwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

**9. Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani zadhati kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula (Mb.) kwa ushirikianona ushauri anaonipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, ninawashukuru Katibu Mkuu Bibi Dorothy Mwanyika; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Moses Kusiluka; Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote wasekta ya ardhi katika ngazi zote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi naufanisi.

**10. Mheshimiwa Spika**, kwa namna yapekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru Dkt. Yamungu Kayandabila aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa mchango wakemkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nampongeza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania na kumtakiakila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake.

**11. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezohayo ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa muhtasari utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2017/18 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/19. Takwimu za utekelezaji wa bajeti zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2018.

B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YAMWAKA WA FEDHA 2017/18 NAMALENGO YA MWAKA WA FEDHA2018/19

12. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu, tumeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); Ilani yaUchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka2015; Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka2000 pamoja na sheria na miongozo mbalimbaliinayotolewa na Serikali.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48 (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi)**

**Ukusanyaji wa Mapato**

13. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **112.05** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali zaardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2018, Wizara imekusanya shilingi bilioni **78.9** sawa na asilimia **70.4** ya lengo (**Jedwali Na. 1**). Ni matarajio yangu kwamba hadi Juni, 2018, lengola kukusanya shilingi bilioni **112.05** litafikiwakwa kutekeleza mikakati mbalimbali. Mikakatihiyo ni pamoja na kutumia vyombo vya habarikuhamasisha wamiliki wa ardhi kulipa kodi yapango la ardhi, kuwafikisha mahakamani nakunadi mali za wale wote ambao hawatalipakodi hiyo kwa wakati. **Natumia fursa hiikuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipakodi ya pango la ardhi kwa wakati. Natoaonyo kwa wadaiwa sugu wa kodi ya pango laardhi kwamba Serikali itaendeleakuwachukulia hatua kali za kisheria ikiwa nipamoja na kuwafikisha mahakamani,kutaifisha mali zao ili kufidia kiwango chakodi wanazodaiwa na kuwafutia miliki.**

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18 Wizara iliahidi kuhuishakiwango cha kodi ya pango la ardhi cha shilingi **400/=** kwa ekari kwa mwaka kwa mashamba ya

biasara yaliyopimwa na kumilikishwa nje yamiji chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufukwamba ili kuendana na thamani halisi yaardhi kwa sasa, Serikali ilihuisha kiwango hichona kuwa shilingi **1,000/** = kwa ekari.

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Serikali iliahidi kupunguza tozo ya mbele (*premium*) ambayo hutozwa mara moja tu wakati wa umilikishaji ardhi kutoka asilimia **7.5** hadi asilimia **2.5** ya thamani ya ardhi. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwambaa hadi hiyo imetekelzeza.

Hata hivyo, pamoja na punguzo hilo tathmini iliyofanywa na Wizara yangu imebaini kwamba bado kuna mwitikio mdogo wa wananchi kukubali kumilikishwa ardhi hususan katika maeneo ya urasimishaji makazi mijini. Imebainika kwamba changamoto hii kwa kiwango kikubwa inachangiwa na gharama kubwa za umilikishaji zinazochangiwa na tozo ya mbele. Hivyo, Serikali inaangalia uwezekano wa kushusha zaidi kiwango cha tozo ya mbele ili kuwavutia wananchi wenye maeneo ya ardhi kujitokeza kwa wingi zaidi kupimiwa na kumilikishwa ardhi yao.

16. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2018/19, Wizara yangu inatarajiakukusanya shilingi bilioni **120** kutokana nakodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi. Lengo hililitafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i) Kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi ya pango la ardhi kwa kurasimishamakazi mijini;

ii) Kutoza kodi ya pango la ardhi katikamaeneo yote ya mijini ambayohayajapimwa na kumilikishwa rasmi;

iii) Kuhuisha muundo wa kiutumishi wawataalam wa sekta ya ardhi katika 10 Halmashauri ili kuongeza ufanisi

katika usimamizi wa rasilimali ardhi ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;

iv) Kupunguza tozo ya mbele kwa wananchiwote waliojenga nyumba katika maeneoambayo hayajapangwa ili kuwawezeshakulipa kodi ya pango la ardhi;

v) Kuimarisha mifumo iliyopo ya utunzaji wakumbukumbu na kuhuisha taarifa zaardhi;

vi) Kuhimiza wamiliki wote wa ardhi nchini kulipa kodi ya ardhi kwa mujibu washeria na kuwachukulia hatua wadaiwasugu ikiwemo kuwafikisha Mahakamani;

vii) Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi katika upangaji na upimaji wa ardhi ili kuongeza idadi ya viwanja na hivyo, kuongeza wigo wa mapato ya Serikali; na

viii) Kuendelea kuboresha mifumo ya kumbukumbu za ardhi ili kurahisisha ulipaji wa kodi ya pango la ardhi.

### **Matumizi**

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara ilidhinishiwa jumla yashilingi bilioni **68.65** kwa ajili ya matumizi yakawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **18.48** ni kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni **24.77** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **25.4** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi tarehe 15 Mei, 2018, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni **38.34** kwa ajili ya matumizi yakawaida na miradi ya maendeleo, sawa naasilimia **55.8** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **12.89** ni kwa ajili ya mishaharanaya shilingi bilioni **12.63** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni **12.82** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **50.5** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **5.83** ni fedha za ndani na shilingi bilioni **6.99** ni fedha za nje (**Jedwali Na. 2**).

## **Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03(Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi)Ukusanyaji wa Mapato**

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume ilitarajia kupo keashilingi milioni **700** kutoka kwa wadau wamaendeleo, makusanyo ya kodi ya pango la nyumba za Tabora na mauzo ya nyaraka zazabuni. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2018, Tume ilipokea shilingi milioni **459.5** sawa na asilimia **65.7** ya lengo kutokana na vyanzo hivyo kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa.

### **Matumizi**

19. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni **2.1** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **1.13** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi millioni **979.8** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2018, Tume ilipokea shilingi bilioni **1.41** sawa na asilimia **67.1** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati yafedha hizo, shilingi milioni **741.66** ni kwa ajili ya matumizi

20. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kutoa huduma mbalimbali za ardhi kwa wananchi zinazolenga kuimarisha usalamawa milki na kuifanya ardhi kuwa moja yangozu kuu za uchumi. Katika kutoa huduma, Wizara yangu inaongozwa na sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa misingi ya haki na usawa.

21. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia uamuzi wa Serikali wa kuhuisha muundo wa utumishi wa wataalam wa sekta ya ardhi waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, wataalam hawa watasimamiwa moja kwa moja na Wizara yangu. Lengo la uamuzi huu nikuimarisha utoaji huduma za sekta ya ardhi chini.

22. **Mheshimiwa Spika**, huduma zinazotolewa na Wizara yangu ni pamoa na kuratibu na kusimamia upangaji ambao unalenga kuwa na miji na makazi bora

yaliyopangwa, kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake na kuwa na uhakikawa uwekezaji katika ardhi. Pia, Wizara inatoa huduma za utayarishaji ramani za msingi ambazo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya maendeleo kwa sekta mbalimbali. Huduma nyingine ni upimaji wa ardhi, utoajiwa hatimiliki za ardhi; hati za hakimiliki za kimila; uthamini; usajili wa hati, nyaraka na miamala ya ardhi; usimamizi wa sekta ya milki, uwekaji wa mifumo ya upatikanaji wa makazi bora na kwa gharama nafuu na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi.

23. **Mheshimiwa Spika**, dhamira yaWizara ni kuifanya ardhi kuwa kichocheo cha maendeleo na nyenzo muhimu katika kupambana na umaskini. Ili kufikia azma hii, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusiana na sekta ya ardhi ili wananchi waweze kuitumia ardhi kwa tija.

#### **Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara naUwekezaji**

24. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatiaumuhimu wa ardhi katika uchumi, Wizara yangu imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Ili kutekeleza azma hiyo, Wizara yangu imeendelea kuimarisha Kitengo cha Uwekezaji katika ardhi kwa kukiongezea rasilimali watu na vitendea kazi. Dhamira ya Wizara ni kuwa na wataalam wa Kitengo hiki katika kila kanda ili kusogezahuduma hii karibu na wawekezaji. Aidha, kwakushirikiana na mamlaka za upangaji, Wizara imeendelea kubainisha ardhi ya uwekezaji na ardhi ya akiba na kutoa miongozo ya kusimamia matumizi ya ardhi hiyo.

Vilevile, Wizara imeboresha huduma zake kwa kupunguza muda wa kuandaa na kusajili hati ambapo kwa sasa mwekezaji anaweza kupatahati ndani ya muda wa siku 30 endapo amekidhi vigezo na masharti ya umilikishaji. Aidha, mifumo ya kutoa huduma za ardhi kwa njia za kielektroniki imeimarishwa ambapo muda wa upatikanaji wa taarifa za

hati nanyaraka nyingine zilizosajili wa umepungua kutoka siku saba (7) hadi tatu (3). Kadhalika, Wizara imeunda Bodimbalimbali za kitaalumaili kuhakikisha wataalam wa sekta ya ardhi niwale wenye sifa, weledi na uadilifu.

### **Ardhi kwa Ajili ya Matumizi ya Viwanda**

25. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yanguinatambua umuhimu wa sekta ya ardhi katikakufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025 kwa kuongeza uwekezaji katika viwanda. Ilikuendana na azma hiyo, Wizara yangu imehakikisha kuwa katika uandaaji wampango kabambe, maeneo ya kutosha yanatengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 mipango kabambe ya miji **18** inayoandaliwa imetenga jumla ya ekari **127,942.96** kwa ajili ya matumizi ya viwanda (**Jedwali Na. 3**). Wizara yangu imetoa Mwongozo kwa Mamlaka zote za upangajikuuhakikisha zinatenga maeneo ya uwekezaji waviwanda wakati wa uandaaji wa mipangokabambe.

26. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, katikamwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuongeza hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi hicho, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Upangaji ya Halmashauri ya Wilaya Kibaha, imepanga eneo lenye jumla ya hekta **1,563** kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vikubwa **124** na viwanda vidogo **23**. Aidha, Wizara imetengaeneo la ardhi ya akiba lenye ukubwa wa hekta **89.9**, maeneo ya biashara hekta **40.6** na ardhi ya kilimo cha biashara yenye ukubwa wa hekta **334**. Maeneo hayo yote yamepangwa kutokanana hekta **2,383** za ardhi ambayo milki yake imebatilishwa kwa kukiuka masharti ya uendelezaji (**Kiambatisho Na. 1**). Aidha, Wizara yangu imebatilisha milki za mashamba yenye ukubwa wa ekari **9,636.19** katika Wilayaza Lushoto, Busega, Bukoba na Arumeru naimetoa maelekezo kwa Mamlaka za Upangaji kuzingatia utengaji wa maeneo kwa ajili ya viwanda, kilimo na ardhi ya akiba. Pia, katika kutekeleza azma hii Wizara kwa kushirikianana Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni inaendelea kuandaa mpango wa kuendeleza ardhi katika

eneo la Mbwamaji lenye ukubwawa ekari **711** kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya uwekezaji. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa jumla ya ekari**184.5** zimetengwa kwa ajili ya ardhi ya akiba, ekari **452** kwa ajili yaviwanda na ekari **1,680** kwa ajili ya kilimo chabiashara.

### **Miradi Mikubwa ya Kitaifa**

27. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yanguimeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombini ya kitaifa hususan Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga, Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway*) na ufuaji wa umeme katika mto Rufiji (*Rufiji Hydropower Project*). Katika mradi wa Bomba la Mafuta, Wizara imeshiriki katika uandaaji mikataba ya uendeshaji wa mradi, uandaaji waramani za msingi katika njia ya bomba la mafuta, uratibu wa utwaaji wa ardhi nauthamini wa ardhi na mali kwa ajili ya fidia na upimaji wa njia ya bomba la mafuta.

28. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa ufuaji umeme, Wizara inashiriki katika upimaji wa eneo la mradi na kuandaa ramani za msingi kwa ajili kuandaa michoro yakihandisi. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu itaendelea kushirikana namamlaka husika katika utekelezaji wa miradihiyo. Vilevile, Wizara itaanza kuandaa kwa awamu mpango wa matumizi ya ardhi katika wilaya **24** na vijiji **134** ambavyo bomba lamafuta linapita na katika maeneo ambayo reli ya kisasa inajengwa (**Kiambatisho Na. 2**).

### **Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

29. **Mheshimiwa Spika**, azma ya Wizara nikuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa. Lengo la kufanya hivyo ni kuwa na miliki salama na hivyo kuondoa na kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi, kutumia ardhikama mtaji hai, kuchochea uwekezaji, kupanua 18 wigo wa mapato ya Serikali, kuongeza mchangowa sekta ya ardhi katika uchumi,

kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kwa tija na kuwa na makazi bora na endelevu.

30. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo ni takriban asilimia **15** tu ya ardhi ya jumla nchini ndio imepangwa na kupimwa. Hali hii inafanya ardhi isiwe na mchanggo mkubwa katika uchumi wa Taifa na kuikosesa Serikali mapato. Katika kukabiliana na hali hii, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya Programu yaKupanga, Kupima na Kumilikisha kila Kipandechaa Ardhi nchini. Ni matumaini yangu kwamba Programu hii ikitekelezwa ardhi itatoa mchangomkubwa katika maendeleo ya kiuchumi nakijamii.

### **Ofisi za Ardhi za Kanda**

31. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yanguimeendelea kuboresha na kusogeza huduma zasekta ya ardhi karibu na wananchi kwa lengola kuwapunguzia gharama na usumbufu wakufuata huduma hizo Wizarani. Maboresho hayo ni pamoja na kupeleka wataalam wakada za ardhi katika fani za upangaji, upimaji,uthamini, usimamizi ardhi na usajili wa hati. Vilevile, Wizara imeimarisha kanda zake kwakupeleka vitendea kazi vya kisasa. Dhamira yaWizara ni kuendelea kuimarisha huduma zake katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zotenchini. **Natoa rai kwa wananchi kutumia ofisi za ardhi za kanda kupata huduma za ardhi badala ya kufuata huduma hizo makao makuu ya Wizara kama ilivyokuwa hapo awali. Utoaji Milki za Ardhi**

32. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza sera na sheria za ardhi, Wizara inaratibu utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, hati za hakimiliki za kimila na hatimiliki za ardhi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuandaa hatimiliki za ardhi **400,000**, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **1,000** nakutoa hati za hakimiliki za kimila **57,000**. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 Wizara imeandaa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **375**, imetoa hati za hakimiliki za kimila **70,299** na hatimiliki za viwanja na mashamba **41,179** (**Jedwali Na. 4**). Wizara yangu inaendelea kutambua na kuthamini michango ya wadau

katika kuwezesha utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na hati za Hakimiliki za Kimila kuititia miradi mbalimbali ya urasimishaji ardhi.

33. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi imeendelea kuhakikisha kuwa kilakipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 miradi ya upimaji wa viwanja katika miji mbalimbali nchini imekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kupanga na kupima ardhi ili kuongeza kasi ya utoaji wa milki za ardhi nchini. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushiriki wasekta binafsi utaendelea kuongeza kasi ya upangaji na upimaji wa ardhi, na hivyo kutoa fursa za ajira na kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na kodi ya pango la ardhi.

34. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri nchini itaandaa Hatimiliki **400,000**, kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **1,000** na Hati za Hakimiliki za Kimila **170,000** zikiwemo **120,000** za Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa hati ili wananchi waweze kuwa na milki salama.**

#### **Kamati za Ugawaji Ardhi**

35. **Mheshimiwa Spika**, Kamati za Ugawaji Ardhini muhimu katika kusimamia ugawaji wa ardhi nchini kwa mujibu wa sheria. Kamati hizi zina jukumu la kuhakikisha haki na usawa katika ugawaji ardhi vinakuwepo pamoja na kuepusha migogoro baina ya watumiaji. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati hizo huidhinishwa na Wizara yangu baada ya kupokea mapendekezo kutoka katika Halmashauri husika. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu imeidhinisha uteuzi wa Kamati za Kugawa Ardhi katika Halmashauri **10** za Majiji ya Tanga na Dodoma; Manispaa za Kinondoni, Ilala, Temeke na Wilaya za Kiteto, Msalala, Kyela, Singida na

Makete. Uteuzi huu umefanya jumla ya Halmashauri **152** kati ya Halmashauri **184** kuwa na kamati hizo. (**Jedwali Na. 5**). Natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazina Kamati za Ugawaji wa Ardhi kuwasilisha mapendekezo ya wajumbe kwa ajili ya kuidhinisha uteuzi wao.

36. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kuidhinisha maombi ya umilikishaji ardhi yanayohusiana na uwekezaji, maeneo ya fukwe, pamoja na maeneo yote yakimkakati ya uwekezaji yenye manufaa kwa Taifa. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Kamati hii ilipitia na kuidhinisha jumla ya maombi **158** ya umilikishaji ardhi yaliyowasilishwa kutoka katika halmashauri mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 6**).

### **Uhakiki wa Mashamba na Viwanja**

37. **Mheshimiwa Spika**, katika mwakawa fedha 2017/18, Wizara yangu iliendelea kuhakiki mashamba na viwanja nchini ilikubaini uzingatiaji wa masharti ya umiliki. Katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2017/18, jumla ya mashamba **32** yalibatilishwa (**Jedwali Na. 7**). Baada ya mashamba hayo kubatilishwa, Wizara yangu ilisambaza Mwongozo wa namna ya kupangana kutumia ardhi ya mashamba yaliyobatilishwa ikiwemo; utengaji wa ardhi kwa ajili ya viwanda, akiba ya ardhi, mahitaji ya wananchi wa eneo husika na matumizi mengine ya jamii. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji za Kibaha, Kigambonina Kinondoni imeandaa mipango ya matumizi ya mashamba yaliyobatilishwa na kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda, biashara, akiba ya ardhi, kilimo cha biasharana matumizi mengine.

### **Utatuzi na Udhhibit wa Migogoro ya Matumiziya Ardhi**

38. **Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kisektailiyoundwa kubaini aina, vyanzo nakupendekeza namna bora ya utatuzi wamigogoro ya matumizi ya

ardhi ilikamilisha kazi yake. Kamati ilichambua migogoro **1,392** iliyowasilishwa Bungeni katika mwaka wafedha 2016/17 pamoja na kufanya tathmini ya hali halisi uwandani na kubaini kuwepo jumla ya migogoro **1,750** ambapo migogoro **564** ilihusu uvamizi wa maeneo ya hifadhi; **218** mwingiliano wa mipaka ya kiutawala; **366** uanzishwaji wa vijiji ndani ya maeneo yahifadhi; **204** migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji; **206** wananchi na wawekezaji kwenye maeneo ya ranchi, mashamba na migodi na migogoro **115** ilitokana na madai ya fidia. Vilevile, kulikuwa na migogoro **77** ambayo ilitokana na vyanzo vingine vidogo ambavyo utatuzi wake hauhitaji taasisi zaidi ya moja. Ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ya matumizi ya ardhi, Serikali inaandaa mkakati mahsuswi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati.

39. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Wizara yangu imeingia makubaliano maalum na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) ili kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji **392** vinavyozunguka Hifadhi za Taifa kote nchini ili kutatua migogoro baina ya vijiji na hifadhi.

40. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi uliofanywa na Kamati ya Kisектa, Wizara yangu kupitia **Kauli Mbiu ya Funguka kwa Waziri wa Ardhi** nilifanya ziara katika maeneo mbalimbali nchini ili kusikiliza kero zawananchi na kuzipatia ufumbuzi. Aidha, kupitia kauli mbiu hiyo, Wizara yangu ilisambaza dodoso katika Halmashauri zote nchini ambapo wananchi walibainisha kero zao na changamoto zinazowakabili kuhusiana na sekta ya ardhi.

41. **Mheshimiwa Spika**, kupitia kauli mbiu hiyo, hadi tarehe 15 Mei 2018 jumla ya malalamiko **3,599** yalipokelewa. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri na mamlaka nydingine za Serikali inaendelea kuyachambua na kuyapatia ufumbuzi malalamiko hayo. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu itaendelea kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu na kuendelea kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia majibu kadri zitakavyopokelewa.

## Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi

42. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (*Land Tenure Support Programme*) inayotekelozwa katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara ilipanga kuhakiki vipande vya ardhi **80,000**. Vilevile, Wizara ilipanga kujenga ofisi za ardhi mbili (**02**) katika Wilaya ya Malinyi na Ulanga, kukarabati ofisi ya ardhi katika Wilaya ya Kilombero na kuandaa vyeti vya ardhi ya kijiji katika vijiji **15**.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi tarehe 15 Mei, 2018 jumla ya vipande vya ardhi **96,257** vilipimwa katika vijiji **41** ambapo jumla ya Hatiza Hakimiliki za Kimila **20,583** zimeandaliwa, mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji **36** imeandaliwa, wakandarasi wa ujenzi wa ofisi za ardhi za wilaya wamepatikana na taratibu za kuandaa vyeti vya ardhi ya vijiji **75** viliviyopimwa zinaendelea. Aidha, jumla ya vijiji **20** vimeandaliwa mipango ya makazi ambapo jumla ya viwanja **18,224** vimepimwa kwa ajili ya kuandali wa Hati ya Hakimiliki ya Kimila. Vilevile, benki ya NMB na CRDB zimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **1.4** kwa wananchi kwa kutumia Hati ya Hakimiliki ya Kimila kama dhamana kwa ajili yakuanzisha miradi ya kiuchumi katika Wilayazinazotekeleza Programu.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2018/19, Wizara itapima vipande vya ardhi kwa ajili ya kuandaa hati za hakimiliki za kimila **120,000**; kuandaa mipango kina ya vijiji na kupima viwanja **20,000**; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **30** na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kisera, kisheria na kitaasisi juu ya utawala na matumizi ya ardhi. Kazi zingine ni kuzijengea uwezo taasisi zinazohusika na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika ngazi za vijiji, kata na wilaya; kufanya tafiti tatu (**03**) za masuala ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuboreshautawala wa ardhi na kukamilisha ujenzi wa ofisi za ardhi katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi.

## **Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka**

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu ilipanga kusajili Hatimiliki na nyaraka nyingine za kisheria **453,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2018 Hatimiliki pamoja na Nyaraka za Kisheria **79,456** zimesajiliwa. Kati ya hizo Hatimiliki ni **30,143** na nyaraka nyingine ni **49,313**. Nyaraka **31,779** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334) na Hati za Umilikiwa Sehemu ya Jengo **923** zimesajiliwa chini yasheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo (Sura 416) (**Jedwali 8A**). Aidha, Nyaraka za Kisheria zipatazo **16,290** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura 117) (**Jedwali 8B**) na Nyaraka **1,244** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura 210) (**Jedwali 8C**). Wananchi wanahamasishwa kupima maeneo yao na kupata hatimiliki ambazo zinahakikisha usalama wa maeneo wanayomiliki. Hati hizo pia zinaweza kutumika kama dhamana za mikopo kutoka katika taasisi za fedha. Katikamwaka wa fedha 2018/19, Wizara imepanga kusajili Hatimiliki na nyaraka za kisheria **453,000**.

## **Ubadilishaji wa Hati Zilizotolewa naliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu**

45. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuvunjwakwa iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA), Wizara yangu ilipewa jukumu la kumilikisha upya ardhi kwa kutoa hatimiliki za miaka 99 kwa wamiliki wotewaliokuwa na hati za pango la ardhi (*groundlease*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufukwamba hadi terehe 15 Mei, 2018, hati zote **21,124** za pango la ardhi zilizopo katika masjala ya Wizara zimebadilishwa kutoka *Ground Lease* ya miaka 33 na kuwa Hati miliki za miaka 99. **Natoa wito kwa wananchi ambao bado hawajabadili hati zilizotolewa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu kuwasilisha hati hizo katika Ofisi ya Msajiliwa Hati Kanda ya Kati ili kuzibadilisha.**

## Mifumo ya Kielektroniki ya Huduma za Ardhi

46. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Serikali iliahidi kuanza kutoahati za kielektroniki katika Manispaa za Kinondoni na Ubungo kwa kutumia Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System*). Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufukwamba kuanzia mwezi Juni 2018, hati za kielektroniki zitaanza kutolewa kwa wamiliki wa ardhi katika Halmashauri za Manispaa za Kinondoni na Ubungo. Muonekano wa hati hii upo katika **Kiambatisho Na. 3.**

47. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, katikamwaka wa fedha 2017/18 Wizara iliahidikuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Kodi yaPango la Ardhi (*Land Rent Management System-LRMS*) katika Halmashauri mbalimbali nchini ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi, umilikishaji ardhi na usajiliwa hati. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imeboresha mfumo huo ambapo wananchi wanaweza kupata taarifa za hatua za umilikishaji na usajili wa hati zao kwa njia ya kielektroniki katika ofisi za Halmashauri. Maboresho haya yatawapunguzia wananchi usumbufu, muda na gharama katika kufuatilia huduma hizo Wizarani. Aidha, mfumo huo umeunganishwa na Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali (*Government Electronic PaymentGateway System - GePG*). Mafunzo ya kutumiamfumo huo yametolewa katika Kanda za Ardhi nane (08), Halmashauri 185 na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 53. Vilevile, kwasasa wamiliki wa ardhi wanaweza kutumiamfumo huo kulipia kodi ya pango la ardhi kwakutumia simu za mkononi kwa kufuatamaelekezo maalum (**Kiambatisho Na.4**).

48. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mifumo ya kielektroniki niliyioielezea hapo juu, Wizara yangu kupitia wataalam wake wa ndani imetengeneza mfumo wa kielektroniki wa usimamizi na udhibiti wa taarifa za mashamba yote nchini. Mfumo huu utaainisha ukubwa, umiliki, matumizi na hali ya maendelezokupitia picha za satelaiti na taarifa zake zitapatikana kwa kutumia kompyuta

au simu ya kiganjani. Mfumo utarahisisha utambuzi wa mashamba yasiyoendelezwa kwa ajili ya milki zake kubatilishwa na kupangiwa matumizi mengine. Hadi tarehe 15 Mei, 2018, taarifa za mashamba yaliyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Lindi, Iringa, Manyara na Arusha zilikuwa zimeingizwa kwenye mfumo.

49. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara itaendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa huduma za ardhi.

#### **Uthamini wa Mali na Fidia**

50. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara iliahidi kuandaa na kuidhinisha taarifa **35,000** za uthamini kwa ajili ya fidia na uthamini wa kawalda kwa matumizi mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini **23,831** ambapo taarifa **13,316** ni uthamini wa fidia na **10,515** ni uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali. Aidha, Wizara ilifanya uthamini kwa ajili ya mizania ya hesabu na utawala kwa baadhi ya taasisi za Serikali. Vilevile, Wizara imekamilisha uandaaji wa Jedwali la Viwangovya Thamani ya Mazao kwa nchi nzima.

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18 Wizara ilikamilisha uundai wa Bodi ya Usajili wa Wathamini ambayo imeanzhishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016. Bodi hii pamoja na mambo mengine, inasimamia usajili, taaluma na maadili katika utendaji kazi wa wathamini. Bodi imepewa mamlaka ya kuwachukuliahataua za kinidhamu ikiwemo kuwafutia usajiliwa thamini wote wanaokiuka maadili ya taaluma zao.

**Natoa rai kwa wananchi nawadau wote wa tasnia ya uthamini kutoataarifa kwa Bodi juu ya wathamini wote wanaokiuka maadili ya taaluma zao au watuwanaofanya kazi za uthamini kinyume chasheria.**

52. **Mheshimiwa Spika**, thamani ya ardhi hubadilika kutokana na mabadiliko ya hali ya soko. Kutokana na hali hiyo, Wizara huhuisha viwango vya thamani ya ardhi mara kwa mara. Uhuishaji huu huwezesha kuwa na viwango sahihi vya ulipaji fidia, utozaji wa kodi na ada mbalimbali zitokanazo na miamala ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara itahuisha viwango vya bei ya soko la ardhi kwanchi nzima. Pia, Wizara inakusudia kuandaana kuidhinisha taarifa za uthamini **35,000**.

53. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mfuko waFidia imezinduliwa na tayari imeanza kazi. Kwakuwa sasa kuna Sheria ya Uthamini na Usajiliwa Wathamini ya mwaka 2016, Bodi inafanya mapitio ya Kanuni za Ardhi za Usimamizi wa Mfuko wa Fidia za mwaka, 2001 ili ziweze kukidhi mazingira ya sasa ya ulipaji fidia na kuondoa mgongano na Sheria hiyo. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Mfuko wa Fidia itakamilisha utungaji wa kanuni hizo.

### **Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia na kuhudumia Mabaraza **53** yanayofanya kazi nchi nzima. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **23,299** yaliyokuwepo na ambayo yatafunguliwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 jumla ya mashauri **41,920** yalishughulikiwa ambapo kati ya hayo mashauri **17,320** yalitolewa maamuzi. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara itaendelea kushughulikia mashauri **24,600** yaliyobaki na yatakayofunguliwa.

55. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia mradi wa maboresho ya sekta ya ardhi,iliyapatia samani za ofisi Mabaraza ya Ardhi yaWilaya **12**. Aidha, Wizara iliahidi kuanzisha Mabaraza mapya katika Wilaya tatu (**03**) ambazo ni Kongwa, Mpwapwa na Urambo. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa taratibu za ajira zitakapokamilika, Mabaraza hayo na Mabaraza katika wilaya nyingine yataanzishwa.

Ili kufikia azma ya Serikali ya kuwa na Baraza katika kila Wilaya, natoa wito kwa Halmashauri kutoa nafasi za Ofisi kwa ajili ya shughuli za Mabaraza bila kuhitaji gharama kubwa za ujenzi au ukarabati.

#### **UPIMAJI NA RAMANI**

#### **Huduma za Ramani**

56. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuhuisha ramani za msingi za uwiano wa 1:50,000 katikamiji **50**. Ramani hizi ni muhimu katika uandaaji wa ramani za matumizi mbalimbali za ardhi kama vile ramani za matumizi ya ardhina ramani zinazoonesha mipaka ya viwanja na mashamba.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ramani za msingi **20** za uwiano wa 1:50,000 za miji **68** katika wilaya za Geita, Mbogwe, Nyang'hwale na Chato zimehuishwa kwa kutumia picha za satelaiti. Katika mwaka wa fedha, 2018/19 Wizara yangu itaendelea kuhuisha ramani za msingi katika miji 100 katika Wilaya mbalimbali.

#### **Mipaka ya Ndani ya Nchi**

57. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu iliahidi kuendelea kuainisha mipaka ya ushoroba wenyewe ukubwa wa kilomita za mraba **2,500** katika pori tengefu la Loliondo wilayani Ngorongoro. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvina Hifadhi ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ushoroba wa pori tengefu la Loliondo wenyewe ukubwa wa kilometa za mraba **1,500** umeainishwa. Utambuzi na uhakiki wa mpaka kati ya Wilaya ya Kilindi na Kitetoumefanyika.

Vilevile, uhakiki wa mipaka yavijiji sita **(6)** vinavyopakana na uwanja wandege wa Kimataifa wa Kilimanjaro umefanyika kwa lengo la kuondoa mgogoro.

Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu itahakiki mipaka sita (**06**) ya Wilaya za Babati na Monduli; Manyoni na Sikonge; Gairo na Kilosa; Kisarawe na Kibaha; Njombe na Mufindi; na Mbarali na Mufindi.

### **Mipaka ya Kimataifa**

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa ramani za msingi pamoja na kupima kipande cha mpaka kuanzia Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron chenye urefu wa kilomita **240**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi hii inaendelea. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 kipandecha mpaka cha kilometra **50** kutokea Ziwa Victoria hadi Sirari kimekamilika. Katika kipande hicho jumla ya alama **480** za kati yampaka zimesimikwa, alama kuu sabazilizobomolewa zimejengwa upya na alama **18** zimekarabatiwa. Aidha, uchukuaji wa taarifa zakijigrafia katika Vijiji **32** vilivyoko katika eneola mpaka huo zimekamilika kwa ajili yakuandaa ramani za msingi (**Jedwali Na. 9**).

59. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara yangu iliahidi kuimarishe mpaka baina ya Tanzania na Uganda katika eneo la nchi kavu. Kazi hii inaendelea kwa uwekaji wa alama zampaka, uandaaji wa ramani za msingi pamojana uandishi wa andiko la mkataba wa mpaka unaendelea. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu itakamilisha uimarishaji wampaka wa Tanzania na Uganda, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi pamoja na kuendelea na uimarishaji wa mpaka baina ya Tanzania na Kenya. Vilevile, Wizara itaimarisha mipaka yetu ndani ya Ziwa Tanganyika na nchiza Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Burundina Zambia. Uimarishaji wa mipaka yetu na nchi jirani ni kwa ajili ya kuimarishe ulinzi na usalama wa nchi pamoja na utekelezaji wa Azimio la Umoja wa Afrika linalozitaka nchi wanachama kuimarishe mipaka yao ifikapo mwaka 2022.

## **Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **200,000** na mashamba **400**. Hadi tarehe 15 Mei, 2018, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **144,780** na mashamba **257** zimeidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu imepanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja **200,000**, mashamba **400** pamoja na kufufua mipaka yaviwanja na mashamba **500** yenye migogoro yamatumizi ya ardhi.

61. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara yangu iliahidi kusimika na kupima alama zamsingi za upimaji (*control points*) **200**. Haditarehe 15 Mei, 2018, Wizara yangu imesimikana kupima alama za msingi **250** katika Wilaya za Rufiji, Kilombero, Malinyi na Tarime. Katikamwaka wa fedha 2018/19 Wizara yanguitasimika na kupima alama za msingi **500**.

## **Upimaji wa Ardhi chini ya Maji**

62. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la India, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na mamlaka ya Bandari imekamilisha upimaji wa chini ya maji katika bandari za Pemba na Wete. Upimaji ndani ya maji nimuhimu kwa ajili ya kutambua na kuainisha kupima njia za meli kwa ajili ya kuingilia ndani ya bandari hizo. Njia hizi ni muhimu kwa ajili ya kuzisaidia meli zinazoingia zisikwame katika mafungu ya mchanga au maeneo yenye kinakidogo cha maji. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu itakamilisha uandaajiwu ramani elekezi (*Navigation charts*) za upimaji uliofanyika katika bandari za Wete na Pemba. Vilevile, itapima maeneo ya chini ya maji katika eneo la bandari ya Mtwara.

## Kujenga Uwezo wa Kupima Ardhi Nchini

63. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza kasina kupunguza gharama za upimaji wa ardhi nchini ni muhimu kuwa na vifaa nya kisasa. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu iliahidi kununua vifaa nya kisasa vyenyeufanisi mkubwa katika upimaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taratibu za ununuzi wa vifaa hivyo zimekamilika na mzabuni ataviwasilisha vifaa hivyo nchini kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha. Vifaa hivyo vitasambazwa katika kanda kwa ajili yakutumiwa na Halmashauri. Vilevile, Wizara yangu itaandaa mafunzo yatakayofanyika mwezi Juni, 2018 kwa ajili ya kuwapa elimu wapima juu ya matumizi bora ya vifaa hivyo.

## Utayarishaji wa Ramani Picha

64. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18 Wizara yangu iliahidi kuhuisharamani za msingi, ili zitumike katika kubuni na kuandaa mipango mbalimbali ya maendeleo katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchora na kuhuisha ramani ya Jiji la Dar es Salaam. Aidha, ramani picha hizo zitatumiwa na mamlaka mbalimbali katika uandaaji wa njia za reli mpya ya kisasa, upangaji wa njia zaumeme na kuandaa mradi wa uboreshaji miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (*Dares Salaam Metropolitan Development Project*). Vilevile, ramani picha hizo zimetumika katika kuandaa rasimu ya mwisho ya mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam.

## UPANGAJI MIJI NA VIJIJI

65. **Mheshimiwa Spika**, upangaji wa mijina makazi vijijini unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira, kuzuia matumizi kinzani na kuwa na uhakika wa uwekezaji katika ardhi. Majukumu haya yanatekelezwa kuititia mipango kabambe, mipango kina ya mijini na vijijini, urasimishajimakazi yaliyoendelezwa kiholela na udhibiti nausimamizi wa uendelezaji miji.

## Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji

66. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri husika kukamilisha mipango kabambe ya majji ya Dar es Salaam na Tanga, Manispaa za Iringa na Singida pamoja na miji ya Ifakara, Mahenge, Malinyi, Bariadi, Kibahana Korogwe. Napenda kuliarifu Bunge Iako Tukufu k uwa hadi tarehe 15 Mei, 2018 Mipango Kabambe ya Manispaa za Iringa na Singida ilikuwa imeidhinishwa na kuzinduliwa. Mipango Kabambe ya miji ya Kibaha na Korogwe imekamilika na kuidhinishwa. Rasimu za Mipango Kabambe ya miji ya Bariadi na Tunduma zimekamilika na utaratibu wa mawasilisho kwenye mikutano ya hadhara (*public hearing*) unaendelea kufanyika katika maeneo ya Mpango ili kupata maoni na mapendekezo kutoka kwa wananchi na wadauwa miji hiyo. Rasimu ya Mpango Kabambe wa Jiji la Tanga imekamilika na kuwasilishwa katika Mamlaka ya Upangaji.

Aidha, rasimu ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam imekamilika na itawasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Uandaaji wa Mipango Kabambe ya miji ya Ifakara, Mahenge na Malinyi unaendelea. Hadi 15 Mei, 2018 jumla ya mipango kabambe ya miji nane (08) imekamilika na mipango mingine **20** ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji (**Jedwali Na.10**)

67. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2018/19, Wizara yangu itashirikiana na Mamlaka za Upangaji za Kigoma/Ujiji, Songea, Morogoro, Tabora, Lindi, Tunduma, Babati, Geita na Njombe kukamilisha mipango kabambe ya miji hiyo. Wizara kwa kutumia wataalam wake itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji katika uandaaji wa mipango kabambe. Aidha, itaendelea kupo keana kuidhinisha mipango kabambe ya miji kadri itakavyowasilishwa kutoka katika Mamlaka za Upangaji. **Naendelea kutoa wito kwa mamlaka zote za upangaji nchini kulipatia kipaumbele suala la uandaaji wa mipango**

kabambe kwa kutenga fedha ili kuwezesha uandaaji wa mipango hiyo.

### **Usanifu na Uendelezaji wa Miji**

68. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Wizara iliahidi kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro **2,000** kutoka Mamlaka za Upangaji. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 jumla ya michoro ya mipango miji **1,947** ilipokelewa na **1,870** iliyodhinishwa. Michoro iliyodhinishwa ina jumla ya viwanja **418,607** kati ya hivyo, viwanja **5,932** ni kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara inatarajia kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro ya mipango miji **2,500** kutoka Mamlaka za Upangaji nchini.

### **Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji Miji**

69. **Mheshimiwa Spika**, moja ya majukumu ya Wizara yangu katika usimamizi wa uendelezaji miji ni kuhakikisha kwamba ardhi inatumika kwa mujibu wa matumizi yaliyopangwa. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara hupokea maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi na mgawanyo wa viwanja na mashamba kutoka Mamlaka za Upangaji. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 jumla ya maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi na mgawanyo wa mashamba **171** yalipokelewa na **157** yaliidhinishwa. Aidha, maombi **14** yalirejeshwa katika Mamlaka za Upangaji kwa ajili yamarekebisheso.

### **Urasimishaji wa Makazi Holela Mijini**

70. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji, MKURABITA na Sekta Binafsi iliendelea kurasimisha makazi katika Halmashauri **27** nchini. Hadi 15 Mei, 2018 jumla ya viwanja **142,992** vilipimwa katika halmashauri mbalimbali (**Jedwali Na. 11**).

71. **Mheshimiwa Spika**, elimu juu ya utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Urasimishaji na Kuzuia Ujenzi Holela mijini

imeendelea kutolewa kwa wadau mbalimbali zikiwemo kampuni binafsi zinazojishughulisha na urasimishaji makazi. Nakala za Programu pamoja na Mwongozo wa Urasimishaji Makazi zimesambazwa katika Mamlaka zote za Upangaji nchini.

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara itaendelea kushirikianana Mamlaka za Upangaji kurasimisha makazi katika Halmashauri za Songea, Njombe, Dodoma, Lindi, Mtwara/Mikindani, Musoma, Mwanza, Ilemela, Kigoma/Ujiji, Tabora, Nzega, Singida, Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga, Mbogwe, Busega, Kibaha, Ubungo na Kinondoni. Aidha, Wizara yangu itaendelea kujenga uwezo wa watumishi wa Mamlaka za Upangaji katika kutekeleza miradi ya urasimishaji makazi. Pia Wizara yangu itaendelea kutekeleza Programu ya Kurasimisha na Kuzuia Ujenzi wa Makazi Holela (2013-2023).

### **Upangaji wa Makazi ya Vijiji**

73. **Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya jukumu la Wizara yangu ni kuratibu na kusimamia upangaji wa makazi ya vijiji kama ambavyo imeainishwa katika Sheria ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara iliahidi kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Malinyi, Ulanga, Mbeya na Iringa ili ziweze kupanga makazi ya vijiji. Katika malengo hayo, Wizara imeweza kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga kuhusu uandaaji wa mipango kina ya makazi ya vijiji ambapo mipango kina ya makazi ya vijiji **20** imeandaliwa.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Wizara yangu itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka mbalimbali za Upangaji ili ziweze kuandaa mipangokina yamakazi ya vijiji pamoja na vitovu vyatia vya biashara.

## **Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji**

75. **Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa laBodi ya Wataalam wa Mipangomiji ni kusajiliwataalam na makampuni. Vilevile, Bodi hii ina jukumu la kusimamia weledi na kutoa adhabustahiki kwa wataalam na makampuni yanayokiuka taratibu na sheria zinazosimamia upangaji miji na vijiji. Majukumu haya yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajiliwa Wataalam wa Mipangomiji Na. 7 ya mwaka 2007. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuendelea kusajili wataalam na makampuni yatakayokidhi vigezo na kuchukua hatua stahiki kwa wataalam wasio waadilifu na makampuni yasiyofuata taratibu kwa mujibu wa sheria. Hadi tarehe 15 Mei 2018, Bodimesajili kampuni **48** za upangaji na Wataalam wa Mipangomiji **310**.

## **MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI**

76. **Mheshimiwa Spika**, jukumu la uratibu, usimamizi wa uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi linatekelezwa naWizara yangu kupitia Tume ya Taifa yaMipango ya Matumizi ya Ardhi. Ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali ardhi na kuondoa migogoro baina ya watumiaji waardhi, Tume imepewa jukumu la kuratibu na kuzisimamia Mamlaka za Upangaji ambazo ni Halmashauri za Wilaya na Vijiji.

## **Uhuishaji wa Mpango wa Taifa wa Matumiziya Ardhi (2013 – 2033)**

77. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kufanyamapitio ya Programu za Mpango wa Taifa waMatumizi ya Ardhi (2013 – 2033) ili kuhuishana kujumuisha masuala ya maendeleo yaviwanda nchini. Wizara yangu imeupitiampango na kuainisha maeneo ambayo yatahuishwa kwa kuzingatia mahitaji ya viwanda na mabadiliko ya tabianchi. Katikamwaka wa fedha 2018/19 Wizara yanguitakamilisha uhuishaji wa mpango huo.

## **Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhiya Wilaya na Vijiji**

78. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara iliahidi kuendeleakushirikiana na wadau mbalimbali ili kuongezakasi ya kupanga matumizi ya ardhi nchini na kufikia lengo la vijiji **1,500** na wilaya tano (**05**) kwa mwaka. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya za Muheza na Morogoro imekamilika na uandaaji wa mpango wa Wilaya ya Serengeti unaendelea. Aidha, katika kipindi hicho mipango ya vijiji **66** imeandalika katika Wilaya **13** za Malinyi (**15**), Kilombero (**12**), Nsimbo (**01**), Uvinza (**03**), Kilwa(**03**), Serengeti (**01**), Mpanda (**01**), Kalambo(**02**), Muheza (**04**), Ulanga (**20**), Kilolo (**01**), Tanganyika (**01**) na Morogoro (**02**). Hadi sasa, jumla ya Wilaya **110** zimeunda Timu za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi na kuzipatia mafunzo. Ni matarajio yangu kwamba kasi ya uandaaji wa mipango ya vijiji itaongezeka.

79. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2018/19, Tume itafanya tathmini ya hali ya uharibifu wa mazingira katika wilaya tatu (**3**) za Mlele, Ulyankulu na Tanganyika zilizokuwa na makambi ya wakimbizi katika ukanda wa magharibi mwa nchi; itatoa mafunzo kwa Timu za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi katika wilaya sita (**06**); na pia itawezesha upangaji wa matumizi ya ardhi katika wilaya sita (**06**) za Geita, Nyang'hwale, Misenyi, Ulyankulu, Tanganyika na Mlele navijiji **250** katika ukanda wa njia ya Bomba la Mafuta kwa upande wa Tanzania, Wilaya zilizopo mipakani na nchi jirani pamoja na Wilaya zilizokuwa na makambi ya wakimbizi katika ukanda wa magharibi mwa nchi.

80. **Mheshimiwa Spika**, vilevile katikamwaka wa fedha 2018/19, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwakushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa(TANAPA) itawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **392** vinavyopakana na Hifadhi za Taifa kote nchini.

81. **Mheshimiwa Spika**, kwa sasa Tume inafanya majadiliano na Taasisi zingine kama vile Mamlaka ya Huduma

za Misitu (TFS) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor (TAWA) ili kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji vyote vinavyozunguka na vilivyopo katika maeneo yote yanayosimamiwa na Mamlaka hizo. Zaidi ya vijiji **250** vinatarajiwu kupangiwa matumizi ya ardhi kuitia ushirikiano utakaoundwa baina ya Tume na Mamlaka hizi mbili. Naendelea kutoa rai kwa wadau wote kushirikiana na Tume ili kuongeza kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya Vijiji, Wilaya na kanda ili kuongeza tija katika uzalishaji, uhifadhi wa mazingira na kuondoa migogoro ya ardhi.

#### **MAENDELEO YA SEKTA YA NYUMBA**

82. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uendelezaji sekta ya nyumba nchini. Sekta hii huchangia kukuza uchumi, kuongeza fursa za ajira na kupunguzau maskini. Kwa kuzingatia hayo, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ilikuvutia uwekezaji katika sekta hii na kuwawezesha wananchi kumudu gharama za nyumba zilizo bora.

83. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuendelea kukusanya taarifa za waendelezaji milki na kuziingiza katika kanzidata. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taarifa mbalimbali za nyumba zimeendelea kuingizwa na nyingine kuboreshwa ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu bei za nyumba katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 taarifa za Vyama vya Ushirika wa Nyumba **34** zimeingizwa kwenye kanzidata hiyo na kat iaye vyama **16** vimejenga jumla ya nyumba **1,000**. Aidha, taarifa za waendelezaji milki na mawakala wa milki **130** ambao wamejenga jumla ya nyumba **24,870** zimeingizwa katika kanzidata. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu itaendelea kukusanya na kuboresha taarifa za nyumba katika kanzidata ya nyumba nchini na kuanzisha Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu za Nyumba.

84. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Mikopo ya Nyumba na upatikanaji wa mitaji vimeweza kuongezeka kwa Mabenki nataasisi za fedha zinazotoa mikopo ya

nyumba. Kwa sasa yapo Mabenki na taasisi za fedha **31** nchini zinazotoa mikopo hiyo ambayo imenufaisha wananchi **4,174**. Kiasi ambacho kimetolewa ni jumla ya shilingi bilioni **344.87**. Aidha, kupitia Mfuko wa Mikopo Midogo Midogo ya Nyumba (*Housing Microfinance Fund*) jumla ya shilingi bilioni **13.87** zimekopeshwa kwa wananchi **1,381** wa kipato cha chini kupitia taasisi tano za fedha. Taasisi hizo ni *DCB Commercial Bank*, *Yetu Microfinance Bank*, *EFC Tanzania Microfinance*, *MUCOBA Bank* na *Mkombozi Commercial Bank*. Natoa wito kwa wananchi hususan wa kipato cha chini kutumia fursa ya kukopa kutoka kwenye taasisi hizi ili waweze kujenga au kuboresha makazi yao.

85. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2018/19, Wizara yangu itaandaa miongozo na viwango vyatayiwa na nyumba 48 za gharama nafuu na kuanzisha Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu za Nyumba. Aidha, itaendelea kuratibu mahusiano na ushirikiano miongoni mwa wadau wa maendeleo ya sekta ya nyumba na makazi. **Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishiwa Serikali**.

86. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuendelea kupokea na kushughulikia maombi mapya na kukusanya marejesho kulingana na taratibu za Mfuko. Hadi tarehe 15 Mei, 2018, Wizara yangu ilipokea na kuchambua maombi **92** yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni **1.5**. Aidha, watumishi **20** wamekopeshwa kiasi cha shilingi milioni **260** na marejesho yaliyokusanywa yamefikia kiasi cha shilingi milioni **576.7**. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Serikali itaendelea kutoa huduma ya mikopo kwa watumishi wengi zaidi ili kuwawezesha kuwa na nyumba bora.

#### **Ushirikiano na Taasisi za Makazi za Kimataifa**

87. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuratibu ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya nyumba na makazi. Katika mwaka wa fedha

2017/18 Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya nyumba na makazi nchini iliadhimisha Siku ya Makazi Duniani tarehe 2 Oktoba, 2017. Katika maadhimisho hayo, Wizara ilitumia fursa hiyo kuwaelimisha wananchi juu ya masuala mbalimbali ya kisera na kisheria yahusuyonyumba na makazi na fursa mbalimbali zilizopokama vile upatikanaji wa mikopo ya nyumba, nyumba za gharama nafuu pamoja na mbinu za kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kumiliki nyumba kwa kupitia ushirika. Wizara pia iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano Mkuu wa Makazi Duniani (*World Urban Forum*) uliofanyika Jijini Kuala Lumpur Malaysia tarehe 7 – 13 Februari, 2018.

## **UTAFITI WA NYUMBA NA VIFAA VYA UJENZI**

88. **Mheshimiwa Spika**, majukumu yakutafiti, kukuza, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu nchini yanatekelezwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaavya Ujenzi (NHBRA).

89. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara kupitia Wakala iliahidi kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za nyumbabora na vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu na kusambaza matokeo yake kwa wananchi. Wakala umekamilisha utafiti wa kutengeneza fremu za milango kwa kutumia zege, matofali yanayofungamana ya kuchoma na ujenzi wadari la gharama nafuu. Pia Wakala umekamilisha utafiti wa mashine rahisi zakuzalisha vifaa vya ujenzi na nyingine kubwa inayotumia injini katika kutengeneza matofali mawili kwa wakati mmoja. Wakala ulitoa mafunzo ya utumiaji wa teknolojia hii kwa vikundi mbalimbali vya watu katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa na Morogoro ambapo zaidi ya wananchi **130** walipatiwa mafunzo. Aidha, Wakala unaendelea na utafiti wa kujenga nyumba kwa gharama nafuu kwa kutumia malighafi zilizoboreshwu kitaalam na zinazopatikana karibu na maeneo ya wananchi.

90. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wakala ulijitangaza katika maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) yaliyofanyika mkoani Lindi na Siku ya Makazi Duniani. Pia ilitangaza huduma zake kuititia vyombo vya habari.

91. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wakala utaendelea kufanya tafiti mbalimbali za kuendeleza teknolojia rahisiza ujenzi wa gharama nafuu, matumizi ya udongo mtupu katika ujenzi wa nyumba bora na matumizi ya chokaa kuimarisha udongo badala ya saruji. Pia Wakala unakusudia kufanya utafiti wa aina nyingine ya matofali ili kupunguza gharama za ujenzi. Aidha, matumizi ya mabaki ya mimea yatatafifiwa zaidi ili kuona namna ambavyo yanaweza kutumika na hivyo kupunguza gharama za ujenzi.

92. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wakala utaendelea kujitangaza ili kusambaza huduma kwa wananchi kwa kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa pamoja na kuititia vyombo vya habari. Aidha, Wakala utaendelea kufanya shughuli za kujiongezea kipato kwa kazi za ushauri wa ujenzi, ukandarasi pamoja na kutoa huduma za upimaji wa vifaambalimbali vya ujenzi katika maabara.

### **SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFAMiradi ya Ujenzi wa Nyumba**

93. **Mheshimiwa Spika**, jukumu la msingila Shirika la Nyumba la Taifa ni ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha ikijumuisha nyumba za gharama nafuu. Shirika linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 1990 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005.

94. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara iliahidi kuwa Shirikalitaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba katika eneo la Iyumbu na kukamilisha taratibu za kupata ardhi ya kujenga nyumba Jijini Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Shirika limekamilisha ujenziwa nyumba **151** katika eneo la Iyumbu, kati ya nyumba **300** ambazo Shirika litajenga katika

mradi huo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/19, Shirika litaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba **149** zilizobaki katika eneohilo na kukamilisha upimaji wa eneo lenyeukubwa wa ekari **188**. Shirika linaendelea nataratibu za kupata ardhi zaidi kwa ajili yaujenzi wa nyumba za makazi na maeneo yabiashara Jijini Dodoma.

95. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara iliahidi kuendelea ukamilishaji wa miradi iliyopo katika mikoa mbalimbali pamoja na kuendelea kujenga nyumba za gharama nafuu. Kati ya miradi **57**, ujenzi wa miradi **39** umekamilika. Miradi hiyo ni ya nyumba za gharama nafuu, gharama ya kati na juu, majengo ya biashara na majengo ya matumizi mchanganyiko na ina jumla ya nyumba **2,280**. Kati ya miradi hiyo iliyokamilika miradi **21** ni ya nyumba za gharama nafuu yenyenye jumla yanyumba **736**. Miradi **12** ya nyumba za makazi ya bei ya kati na ya juu na ina nyumba **1,106**. Miradi mitano (**5**) ni ya nyumba za biashara namradi mmoja (**1**) wa nyumba za matumizi mchanganyiko. Aidha, miradi **18** ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

96. **Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Mei 2018, nyumba zilizouzwa ni **498** nanyumba **749** zinaendelea kuuzwa ama kupangishwa. Walengwa katika ujenzi huu ni wananchi pamoja na Halmashauri za Wilaya. Katika baadhi ya maeneo, Shirika lilikamilisha ujenzi wa nyumba kutokana na Halmashauri hizo kuahidi kununua nyumba hizo hapo awali, lakini Halmashauri nyingi kwa sasa hazioneishi nia ya kununua nyumba hizo kwa sababu zakutokuwa na fedha. Pia, Shirika limeanzisha utaratibu wa kuuza nyumba hizo kwa mfumo wa "**Mpangaji Mnunuzi**" (Tenant Purchase Scheme - TP) ili kuwawezesha wananchi wengi kuweza kumiliki nyumba hizo kwa njia iliyorahisi na baadhi ya Nyumba zimepangishwa.

97. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika liliendelea kutekeleza miradi ya Vitovu vya Miji (*Satellite Cities*) kama Mwendelezaji Mkuu katika maeneo ambayo yanamilikiwa na Shirika. Ili kutimiza azma

hii, Shirika limefanikiwa kuandaa Mipango Kabambe katika miradi ya lyumbu (Dodoma), Kawe (Dar es Salaam), USA River (Arusha), Safari City (Arusha), Salama Creek (Dar es Salaam), Luguruni (Dar es Salaam) na Kunduchi Rifle Range (Dar es Salaam). Kwa sasa, Shirika lina miji ya pembezoni tisa (09) iliyopo katika hatua mbalimbali za uendelezaji. Mipango Kabambe ya lyumbu, Safari City, USARiver na Salama Creek imekamilika nakuidhinishwa na Mamlaka zote husika. Mipango Kabambe ya Kawe, Luguruni na Kunduchi Rifle Range inaendelea na iko katikahatua za mwisho. Katika mwaka wa fedha 2018/19, Shirika litaanza kuandaa Mipango Kabambe ya Songwe, Ruvu, Mafuru (Morogoro), Pemba mnazi, Chato na Kibondo.

### **Mauzo na Makusanyo ya Kodi ya Nyumba**

98. **Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Mei, 2018, Shirika lilikuwa limekusanya jumla ya shilingi bilioni **25.6** kutokana na mauzo yanyumba na shilingi **bilioni 4.825** kutokana namauzo ya viwanja. Kadhalika Shirika lili pangakukusanya shilingi bilioni **95.1** kutokana nakodi ya pango la nyumba. Hadi tarehe 15 Mei, 2018 jumla ya shilingi bilioni **83.8** zimekusanyaawa sawa na asilimia **88** ya lengo. Aidha, Shirika limefanya ukarabati wa majengo ya makazi na biashara **4,125** kwa gharama ya shilingi bilioni **5.64**. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Shirika linatarajia kukusanya kodi yapango kiasi cha shilingi bilioni **93.1**.

### **MAPITIO YA SHERIA NA SERA**

#### **Mapitio ya Sheria**

99. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kukamilisha rasimu za miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidia, Sheria ya Mawakalawa Ardhi na Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini. Napenda kuliarifu Bungelako Tukufu kwamba Rasimu za Miswada ya Sheria hizo zimeandaliwa. Hatua za kukamilisha miswada hii

zinaendelea kwa kuchambua maoni ya wadau ili yaweze kuzingatiwa katika rasimu ya mwisho.

100. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, katika kipindi hiki Wizara yangu ilizifanya marekebisho jumla ya sheria tano (5) za sekta ya ardhi kupitia Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*Miscellaneous Amendments*). Sheria hizo ni Sheria ya Ardhi, Sura 113, Sheria ya Mipangomiji, Sura 355, Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216, Sheria ya Upimaji Ardhi, Sura 324 na Sheria ya Usajiliwa Maafisa Mipangomiji, Sura 426.

101. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Ardhi, Sura 113 ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 yamwaka 2018 kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya muda mrefu. Ilibainika kwamba, wawekezaji katika ardhi hususan katika mashamba makubwa walikuwa wanatumia ardhi kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi lakini mikopo hiyo haikuinufaisha nchi. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba, pamoja na Hati kuwa na masharti ya kuendeleza ardhi, bado Sheria ya Ardhi haikuweka mfumo imara wa kudhibiti matumizi ya fedha hizo ili ziweze kutumika katika uendelezaji wa ardhi au uwekezaji mwingine nchini.

102. **Mheshimiwa Spika**, marekebishohayo yameweke sharti la lazima kwa mtu ye yeyote anayetumia ardhi kama dhamana yakupata mkopo kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ajili ya kuendeleza ardhihusika au kwa ajili ya uwekezaji hapa nchini. Ili kusimamia utekelezaji wa masharti yasheria, mmiliki wa ardhi inayotumika kama dhamana ya kupata mkopo husika anapaswakutoa taarifa kwa Kamishna wa Ardhi kuhusu matumizi ya mkopo huo ndani ya miezi sita baada ya ardhi husika kutumika kama dhamana ya mkopo.

103. **Mheshimiwa Spika**, pia marekebisho ya Sheria ya Ardhi yalifanyika ili kutekeleza matakwa ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania na sheria zinazotoa wajibu wa kulinda rasilimali za nchi. Hivyo, marekebisho hayo yanalenga kudhibiti utoroshaji wa mitaji inayotokana na rasilimaliardhi na badala yake mitaji hiyo itumike kwa maslahi ya nchi.

104. **Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefunchi yetu imekabiliwa na changamoto ya uwepo 57wa ramani zinazopotosha mipaka sahihi ya utawala wa nchi. Upotoshaji huo umechangia kuzuka kwa migogoro ya mipaka na hivyo kusababisha machafuko na hata mauaji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu imeifanyia marekebisho Sheria ya Upimaji wa Ardhi Sura 324 kwa kutoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani haki ya kipekee ya kuandaa, kutengeneza na kusambaza ramani zote zinazoonesha mipaka ya mikoa na nchi. Aidha, Sheria imeweka adhabu kali kwa wotewanaokiuka masharti ya sheria hili.

105. **Mheshimiwa Spika**, vilevile Wizaraimeifanyia marekebisho Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji Sura 426 ili kudhibitiwatu na makampuni yanayofanya kazi zamipangomiji bila kusajiliwa na Bodi ya Usajiliwa Maafisa Mipangomiji.

106. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihadaza kuimarisha Ofisi zetu za Kanda na kusogeza huduma karibu na wananchi, Wizara yangu imezifanyia marekebisho Sheria ya Mipangomiji Sura 355 na Sheria ya Upimaji Ardhi Sura 324. Kupitia marekebisho hayo wapo Maafisa Mipangomiji na Wapima Ardhi katika Kandaa mbao wamekasimiwa mamlaka kamili ya kufanya kazi zote za Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani.

107. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na marekebisho ya sheria za sekta ya ardhi, ili kuweka utaratibu madhubuti wa kusimamia na kutekeleza sheria, Wizara yangu imetunga Kanuni za Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipango miji za mwaka 2018 ambazo zimetangazwa katika Tangazo la Serikali Na.174 la tarehe 4 Mei, 2018. Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini za mwaka 2018 ambazo zimetangazwa

katika Tangazo la Serikali Na. 136 la tarehe 23 Machi, 2018 na Kanuni za Sheria ya Mipango miji za mwaka 2018 ambazo zimetangazwa katika Matangazo ya Serikali Na.79-93 ya tarehe 9 Machi, 2018.

108. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu itaendelea na taratibu za kukamilisha rasimu za miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidia, na Sheria ya Mawakala wa Ardhi.

### **Mapitio ya Sera**

109. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendeleana taratibu za kukamilisha marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarishe usalama wamilki, kuboresha mazingira ya uwekezaji, kudhibiti migogoro baina ya watumiaji wa ardhi, kuimarishe haki na usawa katika upatikanaji na utumiaji wa ardhi kwa makundi mbalimbali ya watumiaji pamoja na kuhakikisha ardhi kama moja ya nguzo kuu yauchumi inatumika ipasavyo katika kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

110. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara iliahidi kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na kuandaa Sera ya Taifa ya Nyumba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mtaalam Mwelekezi amekamilisha kuandaa Rasimu za sera hizo na hatua inayofuata ni kupata maoni ya wadaumbalimbali kwa ajili ya kuziboresha zaidirasimu hizo.

### **Habari na Elimu kwa Umma**

111. **Mheshimiwa Spika**, katika mwakawa fedha 2017/18 Wizara yangu iliahidikuendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliandaa nyaraka mbalimbali **30** kuhusu shughuli za Wizara zilizotolewa katika magazeti, redio, mitando ya kijamii na katika mikutano.

Aidha, ilichapisha na kusambaza nakala **5,000** za kipeperushi kuhusu ulipajikodi ya pango la ardhi, nakala **50,000** za kipeperushi kuhusu utaratibu mpya wa kulipakodi ya ardhi, nakala **2,500** za jarida lenye taarifa za shughuli za Wizara. Vilevile, vipindi maalum **37** vya televisheni na redio vinavyohusu shughuli za Wizara viliandaliwa na kurushwa hewani. Aidha, Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma kimewezechwa kwa kununuliwa vitendea kazi vya kisasa.

Wizara imenunua vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni **224.8** kwa lengo la kuimarisha Kitengo hiki. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara itaendelea na utaratibu wa upashanaji habari na elimu kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi.

## **UTAWALA NA RASILIMALI DATU**

112. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu iliahidi kuwapatia mafunzo watumishi **70** na kuajiri watumishi **291**. Pia, Wizara iliahidi kuendelea kupanua na kuboresha ofisi zake ili kuwezesha watumishi wote kuhamia Dodoma na katika ofisi za kanda. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi tarehe 15 Mei, 2018, Wizara imeajiri watumishi **61** na kuwapatia mafunzo, imeimarisha ofisi za kanda na Makao Makuu ya Wizara Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara itawapatia mafunzo watumishi **70** na kuajiri watumishi wengine kadri vibali vitakavyotolewa.

## **Wataalam wa Sekta ya Ardhi Katika Halmashauri**

113. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatiauamuzi wa Serikali wa kuwataka wataalamwote wa sekta ya ardhi walioko katika halmashauri kuwajibika Wizarani, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaainaaandaa utaratibu bora wa utekelezaji wamaamuzi hayo ili kuwezesha kusimamia kwaufanisi rasilimali ardhi.

## VYUO VYA ARDHI TABORA NA MOROGORO

114. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ina vyuo vivilili vya ardhi vilivyopo Tabora na Morogoro. Vyuo hivi vinatoa mafunzo ya cheti na stashahada katika fani za upimaji ardhi, umiliki, urasimu ramani, ubunifu na uchapishaji ramani, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili. Wizara imeendelea kuviimarisha vyuo hivi ili viweze kudahili wanafunzi wengi zaidi na kutoa ujuzi unaokidhi viwango vya taaluma zao. Idadi ya wahitimu imeongezeka kutoka **559** mwaka 2016/17 hadi **787** mwaka 2017/18. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara yangu itaendelea kuboresha miundombinu ya vyuo hivi ili kuongeza udahili wa wanafunzi.

## C: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YAKUKABILIANA NAZO

115. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudini zinazoendelea kufanyika katikakusimamia sekta ya ardhi nchini, Wizarainakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- a) Uhaba wa wataalam na vitendea kazikatika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikusimamia na kuendeleza sekta ya ardhikwa ufanisi na tija;
- b) Kasi ya ongezeko la watu na mifugoikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi liiyopangwa na kupimwa;
- c) Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi nauendelezaji wa sekta ya milki nchini;
- d) Ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia stahikikwa ardhi inayotwaliwa kwa ajili yashughuli za maendeleo; na
- e) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo yausimamizi wa sekta ya ardhi.

116. **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu nimeainisha mikakati mbalimbali itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/19 na hivyo, kukabiliana na changamoto hizmo. Katika kukabiliana na changamoto yauhaba wa wataalam na vitendea kazi katika ngazi ya Halmashauri, Wizara yangu inaendelea kuimarisha ofisi za ardhi za kanda kwa kupeleka wataalam wengi zaidi

ili waweze kusimamia kwa karibu sekta ya ardhi na kutoa ushauri wakitalaam kwa halmashauri. Aidha, itaendeleakupeleka vifaa vya upimaji katika ofisi zote zakanda za Wizara ili kuwezesha kazi ya upangaji na upimaji ardhi katika halmashauri kufanyika kwa kasi. Pia, itaendelea kuishirikisha sektabinafsi katika utekelezaji wa majukumu yake.

117. **Mheshimiwa Spika**, ongezeko la watu na mifugo ikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa ni mojawapo ya chanzo cha migogoro baina ya watumiaji wa ardhi. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara kwa kushirikiana na halmashauri inatekeleza Programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi. Programu hii inatekelezwa katika Halmashauri zamajaribio za Malinyi, Kilombero na Ulanga mkoani Morogoro. Wizara kwa kushirikiana na halmashauri itaendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji inayozingatia mahitaji ya makundi mbalimbali ya watumiaji. Pia, kwa kutumia uzoefu uliopatikana kutoka kwenye miradi ya majoribio katika wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga, Wizara itatumia uzoefu huo kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo mengine nchini. Kadhalika, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia sekta ya ardhi.

118. **Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa sekta ya milki nchini kumesababisha sekta ya milkikukosa usimamizi madhubuti na kuifanya kushindwa kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa. Wizara yangu imeandardaa rasimu ya mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Milki (*The Real Estate Bill*) ambao unakusudia kuunda chombo cha kusimamia uendelezaji wasekta ya milki.

119. **Mheshimiwa Spika**, ili kuondokana na kero ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia unaofanywa na taasisi na wadau wanaotwaa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, Wizara yangu imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa ajili ya kuratibu shughuli za ulipaji wa fidia.

D: SHUKRANI

120. **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wizara yangu, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali za Vijiiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa naMajiji. Vilevile napenda kuishukuru Benki ya Dunia na nchi wahisani zikiwemo Uingereza, Denmark, Sweden, Japan, China, India, Korea ya Kusini na Marekani. Vilevile, nawashukuru wadau wengine walioshiriki katika utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila ambao ni pamoja na MKURABITA, Care International, Ujamaa Community Resource Team, OXFAM International, African Wildlife Foundation, Tanzania Natural Resource Forum, SNV Netherlands Development Organisation, HakiArdhi, PELUM, Eco Village Adaptation to Climate Change in Central Tanzania na Belgium Technical Cooperation. Wizara yanguinatambua na kuthamini michango inayotolewana wadau wote wa sekta ya ardhi katikautekelezaji wa majukumu ya Wizara.

121. **Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Bibi Dorothy Mwanyika na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Moses Kusiluka kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamojana watumishi wote wa sekta ya ardhi katikangazi zote kwa kunisaidia kutimiza majukumu yangu.

E: HITIMISHO

122. **Mheshimiwa Spika**, katika mwakawa fedha 2018/19, Wizara itaendeleakushirikiana na Halmashauri, wadau, washirika wa maendeleo na wananchi kwa ujumla kutayarisha na kutekeleza mipango ya kuendeleza miji na vijiiji, kusimamia upangaji, upimaji, urasimishaji, umilikishaji na usajili wahati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wamilki.

Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali pamoja na wadau wote wasekta ya ardhi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kama nguzo kuu ya uchumi.

**F: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZIKWA MWAKA 2018/19**

**Makadirio ya Mapato**

123. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wafedha 2018/19, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 120** kutokana nakodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana nashughuli za sekta ya ardhi kwa kutekelezamikakati ambayo imeainishwa katika hotuba yangu.

**Makadirio ya Matumizi**

124. **Mheshimiwa Spika**, ili Wizara yangui weze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu **48**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**: Tume ya Taifa ya Mombando ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavvo:-

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Aina	Mapato/Matumizi	Kiasi (Shilingi)
A	Mapato ya Serikali	120,000,000,000
B	Matumizi ya Kawaida:	
	Matumizi ya Mishahara	17,689,383,000
	Matumizi Mengineyo	17,762,362,638
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>35,451,745,638</b>
C	Matumizi ya Maendeleo	
	Fedha za Ndani	20,000,000,000
	Fedha za Nje	10,537,602,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>30,537,602,000</b>
	<b>JUMLA KUU (B+C)</b>	<b>65,989,347,638</b>

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo **Shilingi 65,989,347,638/=**.

**Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Aina	Matumizi	Kiasi (Shilingi)
A.	Matumizi ya Mishahara	1,102,104,000
B.	Matumizi Mengineyo	979,822,000
C.	Matumizi ya Maendeleo	5,000,000,000
	<b>Jumla</b>	<b>7,081,926,000</b>

Jumla ya matumizi ya kawaida ni **Shilingi 7,081,926,000/=**.

125. **Mheshimiwa Spika**, jumla kuu yafedha zote zinazoombwa kwa Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ni **Shilingi 73,071,273,638/=**.

126. **Mheshimiwa Spika**, mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara [www.lands.go.tz](http://www.lands.go.tz).

127. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii au mwakilishi wake, nina tangazo hapa. Katibu wa Bunge anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa nje ya Ukumbi wa Bunge kuna *Coaster* kwa ajili ya Wabunge walio tayari kwenda kuupokea mwili wa Marehemu Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, Wilayani

Kakonko unaotarajiwa kuwasili hapa Dodoma kwa ndege. Kwa hiyo, mnaoweza kwenda, gari lipo hapo nje, lakini ndege imeshaondoka Dar es Salaam inaelekea hapa Dodoma. Hilo ndiyo tangazo.

Kulikuwepo na majina ya wageni ambayo hayakuwa yameorodheshwa huku, bado nasubiri kama yatakuwa yameletwa kabla sijafika hatua ya mwisho kwa leo nitayatangaza.

Mwakilishi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima Bulembo, una nusu saa yako. (*Makofii*)

**MHE. HALIMA A. BULEMBO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba kuwasilisha Mezani taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii ya Kamati iingie kama ilivyo kwenye *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu - 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu - 3 kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2019 inabainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za

kisekta ikiwemo Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa ni:-

- (a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia (ikiwemo Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi);
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- (c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- (d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1), (2) na Nyongeza ya Nane iliyo chini ya Kanuni ya 118, fasili ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 zimeweka sharti la Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha uliotangulia sambamba na kufanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa tarehe 17 hadi 20 Machi, 2018, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kati ya tarehe 22 hadi 26 Machi, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yaani Fungu 3 – Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi

ya Ardhi na Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inafafanua mambo makubwa matatu yafuatayo:-

- (a) Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- (b) Mpango na Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na
- (c) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio huu unakusudia kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja ili Bunge liweze kuamua kuhusu maombi ya fedha ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge mnamo Aprili, 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufika Machi, 2018 katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia mwezi Machi, 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa mpango wa bajeti ya mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kujuu hali halisi iliyopo Serikalini katika kutekeleza bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile ilijielekeza katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanya hadi kufikia Machi, 2018 ikililinganishwa na lengo la ukusanyaji liliowekwa wakati wa kupitisha bajeti Aprili, 2017. Lengo la kufanya ulinganisho wa namna hii ni kuiwezesha Kamati kupima juhudzi za Serikali na umakini wa mipango yake katika kukusanya maduhuli ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizotumiwa na Kamati zilitokana na vyanzo mbalimbali hususan Taarifa zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi, 2018. Pia mahojiano na majadiliano na wadau mbalimbali yalifanyika. Kwa pamoja yalichangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 112 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyohusiana na shughuli za sekta ya ardhi. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya shilingi bilioni 61.0 zilikusanya. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 54.5 ya maoteo kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa Fungu 3 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilikadiria kukusanya jumla ya shillingi milioni 700 kutoka katika kodi ya pango la nyumba Tabora, mauzo ya vitabu vya mipango ya matumizi ya ardhi na wadau wa maendeleo ya ardhi (*strategic Partners*). Hadi kufikia Februari 2018, Tume ilikusanya kiasi cha shillingi milioni 406.1. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 58 ya lengo liliokusudiwa. Mchanganuo wa mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali vya Sekta ya Ardhi pamoja na wadau wa kimkakati unaonekana katika Jedwali Na.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua taarifa ya makusanyo kwa kulinganisha makadirio yaliyokusudiwa na makusanyo halisi yaliyofikiwa hadi Machi, 2018 na kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Fungu 48 na Fungu 3 ni wa kuridhisha. Kamati inaipongeza Wizara kwa kukusanya

zaidi ya asilimia 50 ya lengo liliokusudiwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara isimamie mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ili kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka ifikapo Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za kutoka Hazina kwa Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara iliiidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 68.6 na kupewa ongezeko la shilingi milioni 117 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa na kupelekea bajeti ya Wizara kuwa shilingi bilioni 68.7. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 43.4 ni za matumizi kawaida na shilingi bilioni 25.4 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufika Februari, 2018 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 34.4 sawa na asilimia 50.1 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Mchanganuo ni kama ifuatavyo: Shilingi bilioni 12.2 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi bilioni 9.3 ni mishahara, shilingi bilioni 5.8 ni fedha za ndani za mandeleo na shilingi bilioni 6.9 ni fedha za nje za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Fungu 3, Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.1 ziliidhinishwa kwa ajili ya mshahara na shilingi milioni 979.8 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hata hivyo, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Tume haikupata tengeo la fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufika Februari 28, Tume ilipokea jumla ya shilingi milioni 933.1 sawa na asilimia 44.1 ya fedha iliyoidhinishwa. Hadi kufikia 28 Februari, 2018, Tume imeshatumia kiasi cha shilingi milioni 904.3 ambayo ni sawa na asilimia 96.9 ya fedha iliyopokelewa. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 480.7 ni matumizi mengineyo na shilingi milioni 423.5 ni fedha za mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa bajeti unaonesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni wa kuridhisha kwa mafungu yote mawili isipokuwa kwa shilingi billioni 10 zilizozuiliwa (*protected items*) kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kusimamia sekta ya ardhi ambazo hazikupokelewa kabisa. Kutopeleka fedha hizo kumezifanya Halmashauri kushindwa kusimamia sekta ya ardhi ipasavyo hivyo kuchangia ongezeko la migogoro ya ardhi nchini. Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha hizo katika Halmashauri kama zinavyoidhinishwa na Bunge ili kuziwezesha Halmashauri kusimamia sekta ya ardhi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo. Kamati ilifanya ziara kukagua miradi ya maendeleo ilio chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea mpaka wa Tanzania na Uganda na mpaka wa Tanzania na Rwanda iliyowekwa tangu enzi za ukoloni mwaka 1890. Mipaka hiyo iko katika hatua za kuboreshwa na kuimarishwa kutohana na ongezeko la watu, mwingiliano wa shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Uganda, Kamati ilitembelea alama ya mpaka ijulikanayo kama *BP* 27 uliopo Kakunyu pembezoni mwa Mto Kagera, *BP* 41 iliyopo katika kijiji cha Kashenyi pembezoni mwa Ziwa Victoria, na *BP* 30 iliyopo eneo la Bugango. Kamati ilielezwa kwamba fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha mipaka zimekwishatolewa ila ilikuwa bado haijatumika kwa vile mpango kazi wa kuimarisha mipaka ulikuwa unakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini tatizo kubwa la kutokuwepo barabara za kufikia alama za mipaka ambapo katika maeneo mengine Kamati illazimika kuvuka mpaka na kuingia upande wa Uganda ambako kulikuwa na barabara ya kuweza kufikia alama za mipaka. Ukosefu wa barabara unafanya hata kazi ya kukagua alama za mipaka kuwa ngumu sambamba na ulinzi wa mipaka

yenyewe. Kamati inashauri zijengwe barabara za kuwezesha kukagua alama za mipaka kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania na Rwanda, Kamati ilielezwa kuwa mpaka uliasisiwa na Uingereza kwa kushirikiana na Ubeligiji mwaka 1924. Mpaka huo uko katika eneo la kina kirefu ndani ya Mto Kagera. Hadi kufikia Machi, 2018 hakuna chochote kilichofanyika kuhusiana na zoezi la uimarishaji mpaka baina ya Tanzania na Rwanda. Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe mpaka huu wa majini unaimarishwa kwa kuweka alama madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwendelezo wa ziara hiyo ya maeneo ya mpakani, Kamati ilipata fursa ya kuoneshwa mradi wa ujenzi wa jengo la biashara la Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) uliopo Mtukula katika eneo la mpaka wa Uganda na Tanzania na kujionea ujenzi unaoendelea. Kamati ilielezwa jinsi mradi wa ujenzi wa kitega uchumi hicho ulivyosuasua kutokana na mkandarasi kutokamilisha kazi yake kwa wakati na hivyo kusitishiwa mkataba wake. Aidha, Kamati ilishuhudia mandhari isiyoridhisha, nyumba, maduka na majengo mengine yamejengwa bila kufuata taratibu halisi za mipango miji na zisizorahisisha ulinzi na usalama wa mpaka huo. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Shirika la Nyumba la Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wahakikishe kuwa wanatoa miradi ya ujenzi kwa mkandarasi mwenye sifa na vigezo vyta kukamilisha kazi kwa wakati muafaka.

(b) Serikali itoe kipaumbele cha kuendeleza maeneo ya masoko yaliyopo mipakani kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi na kuleta mwonekano mzuri wa hali halisi ya nchi yetu (*image*) kwa nchi nyingine tunazopakana nazo. Aidha, Mamlaka husika zihakikishe maeneo ya mpakani yanajengwa kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi na inayorahisisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu.

(c) Serikali itenge bajeti maalumu kwa ajili ya kutengeneza na kukarabati barabara zote za ndani zilizo karibu na mipaka hiyo bila kuathiri mikakati ya kitaalamu katika ulinzi na usalama wa mipaka hiyo.

(d) Serikali izingatie makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu zoezi la kupitia upya na kuhakiki mipaka. Aidha, Serikali ihakikishe inakamilisha zoezi hilo ndani ya muda uliowekwa (*time frame*).

(e) Serikali ichunguze wale wasioendeleza vitalu vilivyoko katika maeneo ya mipaka na kwingineko, vichukuliwe na kugawiwa kwa watu wenyewe uwezo wa kuiendeleva. Lengo ni kuyafanya maeneo ya ardhi yawe endelevu na kuzuia yasitumike kama malisho ya mifugo na watu kutoka nchi jirani.

(f) Serikali iangalie namna bora ya kuimarisha ulinzi katika maeneo yenye mwingiliano wa mipaka. Aidha, mazungumzo maalum yafanyike kwa lengo la kubadilisha matumizi ya ardhi ili maeneo hayo yatolewe kwa Jeshi la Ulinzi la Taifa ili kurahisisha kuimarisha ulinzi katika mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni ya Kamati. Wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Fungu 3 na Fungu 48, Kamati iltoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa Kamati ulifanyiwa kazi. Aidha, maoni mengine yanaendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa kazi kikamilifu kutoptana na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kutenga fedha za ndani za miradi ya maendeleo kama iliviyoshauriwa wakati wa kupitisha bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Matokeo

yanaonekana katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo jumla ya shilingi bilioni 30.5 zimetengwa ilikililinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 25.4 zilizotengwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 20.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20 ni fedha za ndani na shilingi 10.5 ni fedha za nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imetambua kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kuongeza bajeti ya miradi ya maendeleo ya Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kutoka shilingi milioni 300 zilizotengwa 2017/2018 mpaka shilingi milioni 500 zilizotengwa 2018/2019. Lengo ni kuwawezesha Wakala kutekeleza kazi zake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za nyumba na vifaa vya ujenzi. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya Wakala kadri fedha zinapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mabaraza 97 ya Ardhi na Nyumba. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutimiza lengo lake kwa kuwa na Mabaraza ya aina hiyo kwa Wilaya, hususan kwa kuzingatia vigezo vya umbali, jiografia husika na wingi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali itoe kibali cha ajira ili Wizara iweze kuajiri watumishi kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya uhaba wa rasilimali watu inayokabili Mabaraza 44 yaliyoanzishwa kati ya 97 ambayo bado hayajaanza kufanya kazi kutokana na changamoto hiyo. Aidha, fedha za kutosha zitengwe ili kuyawezesha Mabaraza hayo kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kupunguza msongamano wa migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa utekelezaji wa kazi za Wizara. Mpango wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeainisha kutekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuimarisha usalama wa milki za ardhi;
- (b) Kuboresha takwimu za kijigrafia nchini;
- (c) Kuendeleza utafiti wa vifaa nya ujenzi wa nyumba bora zenyenye gharama nafuu kwa ajili ya uendelezaji makazi;
- (d) Kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi; pamoja na
- (e) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika miji kadhaa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliviyowekwa na Wizara kwa kuwa vipaumbele hivi vinaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2018/2019 na vinalenga dira, dhima na madhumuni ya Wizara hususan katika kuimarisha usalama wa miliki za ardhi, kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi pamoja na kuboresha utendaji wa kazi na utoaji wa huduma katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa makadirio wa mapato na matumizi. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48, inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 120 kutokana na vyanzo mbalimbali nya mapato katika sekta ya ardhi. Kiasi hiki ni ongezeko la takriban shilingi bilioni 8, sawa na asilimia 7.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 112.5 zilizokadiriwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa kasi ya urasimishaji makazi mijini pamoja na punguzo la ada ya mbele (*premium*) kutoka asilimia 2.5 hadi asilimia 1 ya thamani ya ardhi katika maendeleo ya urasimishaji makazi mijini. Zoezi hili lina lengo la kuwawezesha wamiliki wengi wa ardhi, hususan mijini, kumudu gharama za kumilikishwa ardhi na hata hivyo kuwawezesha Serikali kumilikisha ardhi zaidi na kuongeza makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 3 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inatarajia

kukusanya jumla ya shilingi milioni 22 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato, hususan makusanyo ya kodi ya nyumba Tabora, uuzaji wa vitabu vya miongozo ya upatikanaji ya matumizi ya ardhi na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Aidha, Tume inatarajia kupata kiasi cha shilingi milioni 680 kutoka kwa wadau wa kimkakati. Ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali ihakikishe inasimamia mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ipasavyo ili kuweza kufikia malengo ya makusanyo ifikapo Juni, 2019 na kuongeza Pato la Taifa kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matumizi. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48, inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 65.9. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 35.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 30.5 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa ujumla bajeti inayoombwa imepungua kwa shilingi bilioni 2.6 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo pungozo hilo ni sawa na asilimia 3.9. Kamati inaona kwamba pungozo hilo linaweza kusababisha Wizara kushindwa kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, imeongezeka kwa shilingi bilioni 5.1 ambalo ni ongezeko la asilimia 20.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25.4 iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili la fedha za miradi ya maendeleo ni kwa ajili ya kuongeza kasi katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu 3, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara inaomba Bunge liidhinishe jumla ya bilioni 7 ili ziweze kutumika kutekeleza Mpango wa Bajeti ya Tume. Katika bajeti hiyo shilingi bilioni 2 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 5 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti unaonesha kuwa bajeti inayoombwa ni ongezeko la shilingi bilioni 4.9 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2017/2018 ya shilingi bilioni

2.1. Ongezeko hili limetokana na kutengewa fedha za miradi kiasi cha shilingi bilioni 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine yaliyojitokeza wakati wa kuchambua na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii masuala mbalimbali yalijitokeza na kuhitaji kujadiliwa kwa kina ili kuweza kuleta uelewa wa pamoja na kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Masuala haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Kumekuwa na taarifa kwamba Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) linalekeea kufilisika kutokana na kuwa na madeni makubwa kuliko mali zake;

(ii) Kumekuwa na kasi kubwa ya uongezeko la ujenzi wa makazi holela mijini linalosababishwa na kasi kubwa la ongezeko la idadi ya watu mijini; na

(iii) Kumekuwa na changamoto ya mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu na taarifa mbalimbali za ardhi, hali inayochangia kuongezeka kwa migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Kamati ilagiza Wizara kuleta mbele ya Kamati taarifa tatu zifuatazo:-

(i) Taarifa kuhusu hali halisi ya maendeleo ya utendaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*);

(ii) Taarifa kuhusu miradi ya urasimishaji makazi na kuzuia makazi holela mijini; na

(iii) Taarifa kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (*Integrated Land Management Information System*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliwasilisha taarifa hizo mbele ya Kamati na zikajadiliwa kwa kina. Aidha, Kamati

ilifanya ziara ya siku tatu kutembelea baadhi ya miradi ya NHC, Mradi wa Urasimishaji Makazi Jijini Dar es Salaam pamoja na kukagua utekelezaji wa Mradi wa Mfumo Uganishi wa Taarifa za Ardhi ili kulinganisha taarifa zilizowasilishwa na hali halisi ilivyo. Kutokana na taarifa zilizowasilishwa pamoja na ziara iliyoanywa, Kamati imebaini yafuatayo:-

(a) Shirika la Nyumba la Taifa. Kamati imebaini kuwa kutokuwepo na Bodi ya Menejimenti ya Shirika la Nyumba la Taifa kunazorotesha utendaji wa Shirika na kulipunguzia kasi ya utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati imeridhishwa na taarifa ya ukaguzi wa shirika uliofanywa na CAG inayotoa taswira halisi ya hali ya Shirika kuliko taarifa zilizokuwa zimesambaa. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kuliwezesha Shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama ifuatavyo:-

(i) Kuchukua hatua za haraka kumaliza mgogoro wa kiungozi uliopo katika Shirika ikiwa ni pamoja na kuteua Bodi na Menejimenti ya Shirika;

(ii) Kukamilisha tathmini ya hali ya ukwasi wa Shirika ili liruhusiwe kuendelea kukopa kwa ajili ya kuendeleza miradi yake;

(iii) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Nyumba; na

(iv) Serikali kutekeleza ahadi yake ya kukutana na wapangaji wa Shirika la Nyumba wa muda mrefu, hasa wastaifu ili waweze kumaliza mgogoro wa upangaji.

(b) Urasimishaji wa makazi. Kamati imebaini kuwepo kwa gharama kubwa za upimaji na urasimishaji wa makazi zinazosababisha wananchi wengi kushindwa kulipia hati zao. Mfano katika Kata ya Kilungule B-Kimara, katika ya hati 6,000 zilizotengenezwa ni hati 170 tu ndiyo zimechukuliwa na wamiliki na nyingine kushindwa kuchukuliwa kutokana na gharama kubwa.

(c) Mfumo Uganishi wa Taarifa za Ardhi (*Integrated Land Management Information System*). Kamati imeridhishwa na hatua za utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, yapo maeneo machache yanayohitaji kuboreshwa ili kufanya mradi huu uwe endelevu baada ya muda wa mradi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa jumla. Sekta ya ardhi inakabiliwa na changamoto kubwa ya kuongezeka kwa mipango ya ardhi, ujenzi holela na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kunusuru sekta hii muhimu.

(a) Kuendelea kuzisimamia na kutekeleza kikamilifu sheria zote za ardhi ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma za ardhi. Aidha, sheria zillzopitwa na wakati ziletwe Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho;

(b) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria mbalimbali za ardhi ili kupunguza migogoro;

(c) Kuyaimarisha Mabaraza ya Ardhi yaliyopo kwa kuyapatia vitendea kazi vya kutosha sambamba na kuajiri wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza Mabaraza hayo;

(d) Kuimarisha Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kwa kuunganisha Wakala huu na Chuo cha Ardhi ili uweze kufanya utafiti kwa ufanisi zaidi;

(e) Kushirikisha wananchi kikamilifu katika kutekeleza programu ya urasimishaji makazi.;

(f) Kuhakikisha kuwa fidia stahiki kwa ajili ya ardhi iliyotwaliwa kwa matumizi ya maendeleo inalipwa ipasavyo; na

(g) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuwezesha Tume

kuongeza kasi ya upimaji na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilisha taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye *Hansard* kama yalivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Angeline Mabula; Makatibu Wakuu na wataalam wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano walioutoa katika Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge; Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge; Ndugu Dickson Bisile, Mkurugenzi Msaidizi; Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Haika Mtui na Gerald Magilli na Msaidizi wa Kamati, Ndugu Jane Ndulesi kwa kuhudumia vyema Kamati pamoja na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,  
MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA  
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI  
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### **SEHEMU YA KWANZA**

#### **MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

##### **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Fungu - 48** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **Fungu - 03** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Fasili ya 7 (1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inabainisha majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za kisekta ikiwemo Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa ni:-

(a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosimamia (ikiwemo Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi);

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya wizara inazosimamia;

(c) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za wizara hizo; pamoja na

(d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu mengine yaliyoorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 98(1),(2) na Nyongeza ya Nane iliyo chini ya kanuni ya 118, fasili ya 7 (1) (a) ya kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 zimeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha uliotangulia sambamba na kufanya uchambuzi wa bajeti ya wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa tarehe 17 hadi 20 Machi, 2018 Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha kati ya tarehe 22 hadi 26 Machi, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yaani **Fungu 03** – Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi ya Ardhi na **Fungu 48** – Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inafafanua mambo makubwa manne (4) yafuatayo:-

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa maendeleo na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ikijumuisha;-

(i) Makusanyo ya Mapato 2017/18;

- (ii) Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
  - (iii) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
  - (iv) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018
- (b) Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; ukijumuisha;-
- (i) Makisio ya Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
  - (ii) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
  - (iii) Mambo mengine muhimu yaliyojitokeza wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019
- (c) Maoni na Ushauri wa Kamati; na
- (d) Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, mpangilio huu unakusudia kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja ili Bunge liweze kuamua kuhusu maombi ya fedha ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### **SEHEMU YA PILI**

#### **2.0 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YALIYOTEKELEZWA**

- 2.1 **Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika** katika uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge mnamo mwezi Aprili, 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya Mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati pia ilitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujuu hali halisi iliyopo Serikalini katika kutekeleza bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwaleta wananchi maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati vilevile ilijielekeza katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi kufikia mwezi Machi 2018 ikilunganishwa na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2017.

Lengo la kufanya ulinganisho wa namna hii ni kuiwezesha Kamati kupima juhudzi za Serikali na umakini wa mipango yake katika kukusanya Maduhuli ipasavyo. Taarifa zilizotumiwa na Kamati zilitokana na vyanzo mbalimbali hususan Taarifa zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi 2018, mahojiano na majadiliano na wadau mbalimbali yaliyofanyika kwa pamoja yalichangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

## 2.2      **Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilikadiria kukusanya Maduhuli ya jumla ya Shilingi Bilioni **112,050,000,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyohusiana na shughuli za sekta ya ardhi. Hadi kufikia Machi 2018 jumla ya Shilingi **61,095,727,625.15**

zilikusanya. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **54.5** ya maoteo kwa mwaka. Aidha kwa upande wa **fungu 03**-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilikadiria kukusanya Jumla ya shillingi **700,000,000** kutoka katika kodi ya pango la nyumba Tabora, mauzo ya vitabu vya mipango ya matumizi ya ardhi na wadau wa maendeleo ya ardhi (*strategic Partners*).

Hadi kufikia Februari 2018, Tume ilikusanya kiasi cha shilingi **406,106,092**. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **58** ya lengo lilitokusudiwa. Mchanganuo wa mapato yatokanayo na vyanzo mbalimbali vya Sekta ya Ardhi pamoja na wadau wa kimkakati unaonekana katika Jedwali **Na.1** hapa chini:-

**Jedwali: 1 Mchanganuo wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

FUNGU	MAKADIRIO	MAKUSANYO	% YA JUMLA YA MAKUSANYO
48- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	112,050,000,000	61,095,727,657.15	54.5%
03- Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi	700,000,000	406,106,092	58%

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 2017/2018

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilichambua taarifa ya makusanyo kwa kulinganisha makadirio yaliyokusudiwa na makusanyo halisi yaliyofikiwa hadi mwezi Machi 2018 na kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo kwa fungu **48** na fungu **03** ni wa kuridhisha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya lengo lilitokusudiwa katika Mwaka wa Fedha 2017/18. **Aidha kamati inaisitiza Wizara isimamie mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ili kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka ifikapo Juni, 2018.**

## 2.3      Upatikanaji wa Fedha za kutoka Hazina

### 2.3.1    Fungu 48-Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleoya makazi

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shillingi **68,655,082,926/=** na kupewa ongezeko la shilingi **milioni 117**

kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa na kupelekea bajeti ya Wizara kuwa shilingi **68,772,286,608.92**. Kati ya fedha hizo shilingi **Bilioni 43.4** ni za matumizi kawaida na shilingi **Bilioni 25.4** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Hadi kufika Februari, 2018 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Billioni **34.4** sawa na asilimia **50.1** ya bajeti iliyoishinishwa na Bunge. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:- **bilioni 12.2** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Billioni 9.3** Mishahara, **Bilioni 5.8** mandeleo (Local) **Bilioni 6.9** maendeleo (Foreign).

### **2.3.2 Fungu 03-Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi- **fungu 03** Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi 2,115,371,822** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **shilingi 1,135,550,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 979,821,822** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Hatahivyo, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Tume haikupata tengeo la fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufika Februari 28 Tume ilipokea jumla ya shilingi **933,158,667** sawa na asilimi **44.1** ya fedha iliyoishinishwa. Hadi kufikia Februari 28, 2018 Tume ilikua imeshatumia kiasi cha shilingi **904,308,303** ambayo ni sawa na asilimia **96.9** ya fedha iliopokelewa. Kati ya Fedha hizo shilingi **480,764,303** ni matumizi Mengineyo na shilingi **423,544,000** ni fedha za Mishahara.

**Jedwali Na.2** linaonyesha Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo Kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hadi Machi, 2018

**Jedwali Na.02-Upaikanaji wa Fedha kutocha Hazina hadi Machi 2018**

Fedha ziliizidhinishwa 2017/18			Fedha ziliizotolewa hadi kufikia Machi 2018		
Mishahara na Matumizi Mengineyo	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo	Mishahara na Matumizi Mengineyo	Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Nje za Miradi ya Maendeleo
43,372,286,608.92	16,400,000,000	9,000,000,000	21,584,956,712.92	5,830,000,000.00	6,998,186,360.00

**Chanzo:** Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa bajeti unaonyesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ni wa kuridhisha kwa mafungu yote mawili isipokuwa kwa shilingi **10,000,000,000** zilizozuiliwa (Protected items) kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kusimamia sekta ya ardhi ambazo hazikupokelewa kabisa. Kutopeleka fedha hizo kumezifanya Halmashauri kushindwa kusimamia sekta ya ardhi ipasavyo hivyo kuchangia ongezeko la migogoro ya ardhi nchini. **Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha hizo katika Halmashauri kama zinavyoidhinishwa na Bunge ili kuziwezesha Halmashauri kusimamia sekta ya Ardhi ipasavyo.**

#### **2.4 UKAGUZI WA BAADHI YA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara kukagua miradi ya maendeleo ilio chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika ziara hiyo Kamati ilitembelea mpaka wa Tanzania na Uganda na mpaka wa Tanzania na Rwanda iliyowekwa tangu enzi za ukoloni mwaka 1890. Mipaka hii iko katika hatua za kuboreshwa na kuimarishwa kutokana na ongezeko la watu, muingilio wa shughuli za kiuchumi katika maeneo ya mipakani.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Uganda Kamati ilitembelea alama ya mpaka ijulikanayo kama **BP 27** uliopo Kakunyu pembezoni mwa mto Kagera, **BP 41** iliyopo katika kijiji cha Kashenyi pembezoni mwa Ziwa Victoria, na **BP 30** iliyopo eneo la Bugango. Kamati ilielezwa kwamba fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha mipaka imekwishatolewa ila ilikuwa bado hajatumika kwa vile mpango kazi wa kuimarisha mipaka ulikuwa unakamilishwa Kamati imebaini tatizo kubwa la kutokuwepo barabara za kufikia alama za mipaka ambapo katika maeneo mengine kamati illilazimika kuvuka mpaka na kuingia upande wa Uganda ambako kulikuwa na barabara ya kuweza kufikia alama za mipaka.

Ukosefu wa barabara unafanya hata kazi ya kukagua alama za mipaka kuwa ngumu sambamba na ulinzi wa

mipaka yenyewe. Kamati inashauri zijengwe barabara za kuwezesha kukagua alama za mipka kwa urahisi.

Kwa upande wa Tanzania na Rwanda Kamati ilielezwa kuwa mpaka uliasisiwa na Uingereza kwa kushirikiana na Ubeligiji mwaka 1924. Mpaka huu uko katika eneo la kina kirefu ndani ya mto Kagera. Hadi kufikia Machi 2018 hakuna chochote kilichofanyika kuhusiana na zoezi la uimarishaji mpaka baina ya Tanzania na Rwanda. **Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe mpaka huu wa majini unaimarishwa kwa kuweka alama madhubuti.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika muendelezo wa ziara hiyo ya maeneo ya mpakani Kamati ilipata fursa ya kuonyeshwa mradi wa ujenzi wa jengo la biashara la shirika la nyumba la Taifa (NHC) uliopo Mtukula katika eneo la mpaka wa Uganda na Tanzania na kujiona ujenzi unaoendelea. Kamati ilielezwa jinsi mradi wa ujenzi wa kitega uchumi hicho ulivyousuasua kutokana na mkandarasi kutokamilisha kazi yake kwa wakati na hivyo kusitishiwa mkataba wake.

Aidha kamati ilishuhudia mandhari isiyordhisha, nyumba, maduka na majengo mengine yamejengwa bila kufata taratibu halisi za mipango miji na zisizorahisisha ulinzi na usalama wa mpaka huo. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Shirika la Nyumba la Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wahakikishe kuwa wanatoa miradi ya ujenzi kwa mkandarasi mwenye sifa na vigezo vya kukamilisha kazi kwa wakati muafaka.

(b) Serikali itoe kipaumbele cha kuendeleza maeneo ya masoko yaliyopo mpakani kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi na kuleta muonekano mzuri wa hali halisi ya nchi yetu (*Image*) kwa nchi nyingine tunazopakana nazo. Aidha, Mamlaka husika zihakikishe maeneo ya mpakani yanajengwa kwa kuzingatia Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi na inayorahisisha ulinzi na usalama wa mipaka yetu;

(c) Serikali itenye bajeti maalumu kwa ajili ya kutengeneza na kukarabati barabara zote za ndani zilizo karibu na mipaka hiyo bila kuathiri mikakati ya kitaalamu katika ulinzi na usalama wa mipaka hiyo;

(d) Serikali izingatia makubaliano yaliyofikiwa katika kikao cha wakuu wa nchi za Afrika kuhusu zoezi la kupitia upya na kuhakiki mipaka. Aidha serikali ihakikishe inakamilisha zoezi hilo ndani ya muda uliowekwa (*Time frame*)

(e) Serikali ichunguze wale wasioendeleza vitalu vilivyoko katika maeneo ya mipakani na kwingineko, vichukuliwe na kugawiwa kwa watu wenye uwezo wa kuviendeleza, lengo ni kuyafanya maeneo ya ardhi yawe endelevu na kuzuia yasitumike kama malisho ya mifugo na watu kutoka nchi jirani;

(f) Serikali iangalie namna bora ya kuimarishe ulinzi katika maeneo yenye muingiliano wa mipaka. Aidha mazungumzo maalumu yafanyike kwa lengo la kubadilisha matumizi ya ardhi ili maeneo hayo yatolewe kwa Jeshi la ulinzi la Taifa ili kurahisisha kuimarishe ulinzi katika mipaka ya nchi.

## 2.5 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kwa Fungu 03 na Fungu 48 Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Wizara hii. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa kamati ulifanyiwa kazi, aidha maoni mengine yanaendelea kufanyiwa kazi, lakini yapo maoni ambayo hayakufanyiwa kazi kikamilifu kutokana na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutenga fedha za ndani za miradi ya maendeleo kama iliviyoshauriwa wakati wa kupitisha bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Matokeo yanaonekeana Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/19 ambapo jumla ya Shillingi **30,537,602,400** zimetengwa ilikilinganishwa na bajeti ya shilingi **25,400,000,000** zilizotengwa Mwaka 2017/2018, ongezeko hili ni sawa na asilimia **20.2**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 20,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,537,602,400/=** ni fedha za nje.

Aidha, Kamati imetambua kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kuongeza bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi kutoka shilingi milioni 300 zilizotengwa 2017/2018 mpaka milioni 500 zilizotengwa 2018/2019. Lengo ni kuwawezesha Wakala kutekeleza kazi zake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za nyumba na vifaa vya ujenzi. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya wakala kadri fedha zinapopatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mabaraza 97 ya Ardhi na Nyumba. Hatahivyo Kamati inashauri Serikali kutimiza lengo lake la kuwa na Mabaraza ya aina hiyo kwa kila Wilaya hususani kwa kuzingatia vigezo vya umbali, jiografia husika, na wingi wa migogoro. **Hata hivyo kamati inashauri Serikali itoe kibali cha ajira ili Wizara iweze kuajiri watumishi kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya uhaba wa Rasilimali watu inayoyakabili mabaraza 44 yaliyoanzishwa kati ya 97 ambayo bado hayajaanza kufanya kazi kutokana na changamoto hiyo. Aidha fedha za kutosha zitengwe ili kuyawezesha mabaraza haya kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kupunguza msongamano wa migogoro ya Ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.**

## **2.6 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeainisha kutekeleza shughuli mbalimbali. Baadhi ya shughuli hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Kuimarisha usalama wa milki za ardhi;
- b) Kuboresha takwimu za kijigrafia nchini;
- c) Kuendeleza utafiti wa vifaa vyta ujenzi wa nyumba bora na zenyenye ghamama nafuu kwa ajili ya uendelezaji makazi;
- d) Kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi; pamoja na
- e) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika miji kadhaa hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Wizara kwakuwa vipaumbele hivi vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2018/2019 na vinalenga dira, dhima na madhumuni ya Wizara hususani katika kuimarisha usalama wa milki za ardhi, kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayohusu sekta ya ardhi pamoja na kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma katika sekta ya ardhi.

### **SEHEMU YA TATU**

- 3.0 **MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**
- 3.1 **Uchambuzi wa Makisio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Fungu 48** inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi **120,000,000,000/-** = kutopteka na vyanzo mbalimbali vyta mapato katika sekta ya ardhi. Kiasi hiki ni ongezeko la takribani **shilingi Billioni 8** sawa na asilimia **7.1** ikilinganishwa na shilingi **112.5** zilizokadiriwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa kasi ya urasimishaji makazi mijini pamoja na punguzo la ada ya mbele (Premium) kutoka **asilimia 2.5** hadi **asilimia 1** ya thamani ya ardhi katika maeneo ya urasimishaji makazi mijini. Zoezi hililina lengo la kuwawezesha wamiliki wengi wa ardhi hususan mijini kumudu gharama za kumilikishwa ardhi na hivyo kuiweshera Serikali kumilikisha ardhi zaidi na kuongeza makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **22,000,0000** kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato hususani makusanyo ya kodi ya nyumba Tabora, Uuzaji wa vitabu vya miongozo ya upangaji wa matumizi ya ardhi na uuzaaji wa nyaraka za zabuni.

Aidha Tume inatarajia kupata kiasi cha **shilingi 680,150,000** kutoka kwa wadau wa kimkakati. Ni mapendeleko ya **Kamati kwamba Serikali ihakikishe inasimamia mikakati ya makusanyo iliyojiwekea ipasavyo ili kuweza kufikia malengo ya makusanyo ifikapo Juni 2019, na kuongeza pato la Taifa kwa mwaka.**

### **3.1.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi **65,969,347,638** Kati ya fedha hizo shilingi **35,451,745,638/-** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **30,537,602,000/-** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kwa ujumla bajeti inayoombwa imepungua kwa shilingi **2,685,735,288** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo punguzo hilo ni sawa na asilimia **3.9**. Kamati inaona kwamba punguzo hilo linaweza kupelekea Wizara kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea .

Aidha kwa upande wa bajeti ya maendeleo bajeti imeongezeka kwa shilingi **5,137,602,000** ambayo ni ongezeko

la **asilimia 20.2** ikilinganishwa na shilingi **25,400,000,000** iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/18. Ogezeko hili la fedha za miradi ya maendeleo ni kwa ajili ya kuongeza kasi katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika** Kwa upande wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, (**Fungu 03**) katika Mwaka wa Fedha **2018/19** Wizara inaomba Bunge liidhinishe jumla ya shilingi **7,081,926,000/=** ili ziweze kutumika kutekeleza mpango na bajeti ya Tume.

Kati ya bajeti hiyo, shilingi **2,081,926,000/=** ni za Matumizi ya kawaida, na shilingi **5,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti unaonyesha kuwa bajeti inayoombwa ni ongezeko la shilingi **4,966,554,178** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka 2017/18 ya shilingi **2,115,371,822**. Ongezeko hili limetokana na kutengewa fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi **Billion 5**

### **3.1.2 MASUALA MENGINE MUHIMU YALIYOJITOKEZA WAKATI WA KUCHAMBUA NA KUPITISHA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HII KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii maswala mbalimbali yalijitokeza na kuhitaji kujadiliwa kwa kina ili kuweza kuleta uelewa wa pamoja na kuweza kuishauri Serikali ipasavyo. Maswala haya ni kama yafuatayo:-

- Kumekuwa na taarifa kwamba Shirika la nyumba la Taifa (NHC) linaelekea kufilisika kutoptaka na kuwa na madeni makubwa kuliko mali zake.
- Kumekuwa na kasi kubwa ya ongezeko la ujenzi wa makazi holela mijini linaosababishwa na kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu mijini.
- Kumekuwa na changamoto ya mifumo ya utunzaji wa kumbu kumbu na taarifa mbali mbali za ardhi

hali inayochangia kuongezeka kwa migogoro baina ya watumiaji mbali mbali wa ardhi hapa nchini.

Kutokana na changamoto hizo kamati iliajiza Wizara kuleta mbele ya Kamati Taarifa tatu zifuatazo:-

- a) Taarifa kuhusu hali halisi ya Maendeleo na Utendaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)
- b) Taarifa kuhusu Miradi ya Urasimishaji Makazi na kuzuia Makazi Holela Mijini,
- c) Taarifa kuhusu utekelezaji wa mradi wa mfumo unganishi wa tarifa za ardhi ( Intergrated Land Management Information System).

**Mheshimiwa Spika**, Wizara iliwasilisha Taarifa hizo mbele ya Kamati na zikajadiliwa kwa kina. Aidha Kamati ilifanya ziara ya siku tatu kutembelea baadhi ya miradi ya NHC, mradi wa urasimishaji makazi jijini Dar Es Salaam pamoja na kukagua utekelezaji wa Mradi wa Mfumo Uunganishi wa Taarifa za ardhi (ILMIS) ili kulinganisha tarifa zilizowasilishwa na hali halisi ilivyo. Kutokana na taairifa zilizowasilishwa pamoja na ziara iliyo fanywa Kamati imebaini yafuatayo:-

**a) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kutokuwepo kwa Bodi na menejiment ya Shirika kunazorotesha utendaji wa shirika na kulipunguzia kasi ya utekelezaji wa majukumu yake. Aidha Kamati imeridhishwa na taarifa ya ukaguzi wa Shirika uliofanywa na CAG inayotoa taswira halisi ya hali ya shirika kuliko tarifa zilizokuwa zimesambaa. Kamati inaishauri serikali kutekeleza yafuatayo ili kuliwezesha shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi:-

- i) Kuchukua hatua za haraka kumaliza mgogoro wa kiuongozi uliopo katika Shirika ikiwa ni pamoja na kuteua Bodi na Menejiment ya Shirika.

ii) Kukamilisha tathmini ya hali ya ukwasi wa shirika ili liruhusiwe kuendelea kukopa kwa ajili ya kuendeleza miradi yake

ii) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Nyumba.

iii) Serikali kutekeleza ahadi yake ya kukutana na wapangaji wa Shirika la Nyumba wa muda mrefu hasa wastaafu ili kumaliza mgogoro wa upangishaji wao.

**b) Urasimishaji Makazi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa gharama kubwa za upimaji na urasimishaji makazi zinazopelekea wananchi wengi kushindwa kulipia hati zao; Mfano katika Kata ya “Kilungule B-Kimara” kati ya hati 6000 zilizotengenezwa ni hati 170 tuu ndio zilimeshachukuliwa na wamiliki na nyingine kushindwa kuchukuliwa kutokana na gharama kuwa kubwa; Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

i) Kuongeza kasi ya utoaji hati kwa kupunguza gharama za upimaji na uaandaaji wa hati;

ii) Serikali ianzishe utaratibu bora na rahisi wa kulipia gharama za kupima na kumiliki ardhi. Kwa mfano ulipaji kwa awamu;

iii) Serikali iongeze kasi ya upimaji na urasimishaji wa makazi sambamba na kasi ya ongezeko la watu na ukuaji wa mijji;

iv) Elimu kwa umma juu ya urasimishaji na matumizi bora ya ardhi itolewe kwa wananchi; Mfano katika Halmashauri ya Ubungo kata ya “Kilungule A” wananchi wengi wameshapimiwa ardhi lakini bado hawajapewa hati wala hawajui taratibu za kupata hati miliki za ardhi zao;

c) Mfumo Uganishi wa Taarifa za ardhi (ILMIS).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na hatua za utekelezaji wa mradi wa mfumo unganishi wa tarifa za ardhi. Hata hivyo yapo maeneo machache yanayohitaji kuboreshwa ili kufanya mradi huu uwe endelevu baada ya muda wa mradi kukamilika kama ifuatavyo:-

i) Kusambaza Mfumo unganishi wa kuhifadhi taarifa za Ardhi kwa Halmashauri zote nchini;

ii) Kuwapatia mafunzo wataalamu wazawa kuhusu namna bora ya kuendesha Mfumo Uganishi wa Taarifa za Ardhi. (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*) kwa lengo la kupata wataalamu wetu wa ndani wa kuweza kuendesha mfumo huu baada ya mradi kukamilika;

iii) Kuhakikisha kuwa wafanyakazi na vibarua wanaofanyakazi chini ya Mradi wa Mfumo Uganishi wa Tarifa za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS- ILMIS*) wanalipwa stahili zao kwa wakati.

iv) Serikali iangalie uwezekano wa kutenga fedha za ndani kwa ajili ya mradi huu ili kuwa na uhakika wa uendelevu wake baada ya wafadhili kuondoka

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ardhi inakabiliwa na changamoto kubwa ya kuongezeka kwa migogoro ya ardhi, ujenzi holela, na kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo ili kunusuru sekta hii muhimu;-

a) Kuendelea kuzisimamia na kutekeleza kikamilifu Sheria zote za ardhi ili kuongeza ufanisi katika kutoa

huduma za ardhi. Aidha, sheria zilizopitwa na wakati ziletwe Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho;

b) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria mbali mbali za ardhi ili kupunguza migogoro;

c) kuyaimarisha Mabaraza ya Ardhi yaliyopo kwa kuyapatia vitende kazi vya kutosha sambamba na kuajiri wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya kuendeleza mabaraza ya ardhi.

d) Kuimarisha Wakala wa Utafiti wa Nyumba na vifaa vya vifaa vya ujenzi kwa kuiunganisha Wakala hii na Chuo cha Ardhi ili iweze kufanya utafiti kwa ufanisi zaidi;

e) Kushirikisha wananchi kikamilifu katika kutekeleza programu ya urasimishaji makazi;

f) Kuhakikisha kuwa fidia stahiki kwa ajili ya ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo inalipwa ipasavyo.; na

g) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuiwezesha Tume kuongeza kasi ya upimaji na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi,

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambaao Maoni, ushauri na ushirikiano wao umeweza kutsikilia kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Nape Moses Nnauye, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota, Mb-M/Mwenyekiti
3. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb
4. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya, Mb

5. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb
6. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Lucy Fidelis Owenya, Mb
9. Mhe. Jaffer Sanya Jussa, Mb
10. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb
11. Mhe. Omary Tebweta Mgumba, Mb
12. Mhe. Boniface Mwita Getere, Mb
13. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb
14. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
15. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
16. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb
17. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
18. Mhe. Risala Saidi kabongo, Mb
19. Mhe. Dkt Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb
20. Mhe. Dkt Stephen Lemomo Kiruswa, Mb
21. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb
22. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb
23. Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi, Mb
24. Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Mhe. William V. Lukuvi, (Mb)** Naibu Waziri, **Mhe, Angelina S. Mabula, (Mb)**, Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ushirikiano waliota kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na **Ndg. Stephen Kagaigai** Katibu wa Bunge, Ndg. **Athuman Hussein** Mkurugenzi wa wa Idara ya Kamati za Bunge, **Ndg. Dickson Bisile** Mkurugenzi Msaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. **Haika Mtui, Gerald Magili**, na Msaidizi wa Kamati Ndg. **Jane Ndulesi** kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Nape Moses Nnauye, Mb.

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,  
MALIASILI NA UTALII,**

28 Mei, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima Bulembo kwa niaba ya Mwenyekiti kwa wasilisho la taarifa ya Kamati. Taarifa ya Kamati ni nzuri, imesheheni mambo mengi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na tukio la kusikitisha la ndugu yetu lilitotokea juzi, kwa leo hatutakuwa na Wabunge wa kuichangia hoja hii. Hoja hii mtaanza kuichangia kesho baada ya kipindi cha maswali na itahitimishwa kesho hiyo hiyo ili ratiba ya shughuli za Bunge iendelee kama ilivyopangwa. (*Makofii*)

Jana Mheshimiwa Spika alitoa taarifa hapa na mtakapotoka nje hapo mtapewa ratiba ya kuaga mwili wa Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago ambapo shughuli hiyo itafanyika mara tu baada ya shughuli za Bunge kuahirishwa. Nawashukuru sana kwa utulivu wenu na kwa kumsikiliza mtoa hoja Mheshimiwa Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, lakini pia na taarifa ya Kamati iliyowasilishwa hivi punde.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, sina la ziada. Wale ambao mlikuwa na wageni na hawakutajwa katika orodha ile ya mwanzo nilitegemea majina hayo yangefika lakini sijayapata hapa. Kwa hiyo, sina taarifa ya wageni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 30 Mei, 2018, Siku ya Jumatano, saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.50 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 30 Mei, 2018, Saa Tatru Asubuhi)*